# UKIUSHI KATIKA TAFSIRI: UHAKIKI WA TAMTHILIA *NITAOLEWA NIKIPENDA*

**Na**

**Kamotho John Njoroge**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**OKTOBA, 2017**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa bila kibali cha mwandishi au / na Chuo Kikuu cha Moi.

………………………………… ………………………………….

Kamotho John Njoroge Tarehe

SSC/PGK/18/04

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

………………………………… ………………………………………

Dkt. Kandagor Mark Mosol Tarehe

Idara ya Kiswahili na Lugha

Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi,

ELDORET, KENYA

……………………………………. ……………………………………..

Dkt. Samuel M. Obuchi Tarehe

Idara ya Kiswahili na Lugha

Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi,

ELDORET, KENYA

# TABARUKU

*Kwa wazazi wangu Mama Teresiah Wangarĩ*

*Kamotho*

*na*

*Marehemu Mzee Joseph Kamotho Njoroge*

## IKISIRI

Utafiti huu umehusisha uchunguzi wa usuli wa sanaa ya tafsiri. Utafiti umechanganua kipengele cha ukiushi katika tamthilia *Nitaolewa Nikipenda* ambayo ni tafsiri ya Kiswahili ya tamthilia *Ngaahika Ndeenda*. Utafiti huu umefanya uchanganuzi linganishi wa lugha iliyotumiwa katika Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* iliyo katika lugha ya Gĩkũyũ na Matini Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* iliyotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Utafiti umelenga kuchunguza Matini Tafsiri ilivyokiuka kutoka Matini Chanzi. Utafiti umechunguza zaidi dhana kuwa Matini Tafsiri ni 'kivuli tu' cha Matini Chanzi na hivyo kuihukumu kama kazi sahihi au isiyo sahihi. Utafiti huu umetumia Nadharia ya Mawasiliano katika Tafsiri ya Nida ambayo ni nguzo ya kanuni na michakato muhimu katika zoezi la tafsiri. Vitabu vya wataalamu mbalimbali vinavyohusu Nadharia ya Tafsiri na ukiushi katika tafsiri vimesomwa na mawazo yao kunakiliwa. *Ngaahika Ndeenda* na *Nitaolewa Nikipenda* vimesomwa kwa makini na kulinganishwa kwa mujibu wa lugha iliyotumiwa kwa kutumia maana kama kaida. Utafiti huu umechanganua ukiushi katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* na vilevile kujadili aina za ukiushi katika Tamthilia hii. Aidha umbuji kama kiungo cha ukiushi katika Matini Tafsiri ulitathminiwa. Tasnifu hii umejikita katika Nadharia ya Mawasiliano katika Tafsiri ya Nida ambayo husisitiza mawasiliano mwafaka kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi. Utafiti umefanywa kwa kuchambua vitabu vya wananadharia wa tafsiri mbali na kuchanganua maneno ya Matini Tafsiri kwa kuyalinganisha na maneno ya Matini Chanzi. Sampuli za maneno, sentensi na vishazi vimetambuliwa na kunakililiwa kwa utaratibu, kuonyesha vilivyowakilishwa katika Matini Chanzi ya Gĩkũyũ na chini yake vilivyohawilishwa katika Matini Tafsiri ya Kiswahili. Maneno, vishazi na sentensi hizi zimechanganuliwa kiulinganishi halafu mahitimisho kufanywa. Uchanganuzi wa data iliyoshughulikiwa umethibitisha kuweko kwa ukiushi katika Matini Tafsiri. Ukiushi wowote uliopatikana katika Matini Tafsiri umeainishwa katika aina mbalimbali za ukiushi mathalani ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kisintaksia na ukiushi wa kisemantiki. Athari ya maana ya ujumbe katika Matini Chanzi na Matini Pokezi imechunguzwa pia. Utafiti umezingatia dhima ya mtafsiri kama msanii na jinsi anavyokiuka maana iliyoko katika Matini Chanzi wakati anapotafsiri. Ni matumaini yangu kuwa utafiti huu utawafaa wanafunzi na wasomi ambao watatafitia mbinu za tafsiri katika kazi za kifasihi.

# ABSTRACT

This study involves analyzing the background of the art of translation. The study analyzes the element of deviation in the play *Nitaolewa Nikipenda* which is a Kiswahili translation of the play *Ngaahika Ndeenda.* It carries out a comparative analysis of the language used in the Source Text *Ngaahika Ndeenda* which is in Gĩkũyũ and that of the Target Text *Nitaolewa Nikipenda* which is in Kiswahili. The study aims at analyzing how the Target Text deviates from the Source Text. The study goes beyond considering Target Text as "a mere shadow″ of the Source Text thus judging it as an appropriate or inappropriate representation. The Theory of Dynamic Equivalence in Translation expounded by Nida which lays foundation for rules and procedures necessary in the practice of translation is employed. Books from various experts who have written about Translation Theory and deviation in translation are read and their views compiled. *Ngaahika Ndeenda* and *Nitaolewa Nikipenda* are critically read and compared in the context of the language used using meaning as the norm. This study analyzes deviation in the Target Text of *Nitaolewa Nikipenda* and also discusses types of deviation in the Target Text. Besides, creativity as an ingredient of deviation in the Target Text was assessed. This study uses the Theory of Dynamic Equivalence in Translation by Nida which emphasizes on effective communication between the Target Text and the Target Audience. This study involves analyzing works of translation theorists besides analyzing words in the Target Text by comparing them with those in the Source Text. Samples of words, sentences and phrases are identified and copied with the Source (Gĩkũyũ) Text coming first followed below it by the Kiswahili translated text. These words, phrases and sentences are analyzed comparatively and conclusions made. An analysis of the collected data reveals existence of deviation in the Target Text. All forms of deviation found in the Target Text are categorized into phonological, syntactic and semantic forms of deviation. The effect of the meaning of the message in the Source Text and the Target Text is studied too. The study recognizes the role of the translator as an artist and how she/he deviates from the meaning intended by the Source Text. It is my hope that this study will benefit learners and scholars who will research on translation skills on literary works.

# YALIYOMO

IKIRARI ........ ii
TABARUKU ........ iii
IKISIRI ........ iv
ABSTRACT ........ v
MAELEZO YA AKRONIMU ........ ix
MAELEZO YA ISTILAHI ........ x
SHUKRANI ........ xi
SURA YA KWANZA ........ 1
MISINGI YA UTAFITI ........ 1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ........ 1
1.2 Historia Za Waandishi Wa Matini Chanzi Na Matini Tafsiri ........ 3
1.2 Suala la Utafiti ........ 4
1.3 Malengo ya Utafiti ........ 5
1.4 Nadharia Tete ........ 5
1.5 Upeo wa Utafiti ........ 6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 8
1.7 Msingi wa Kinadharia ........ 10
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ........ 14
1.9 Hitimisho ........ 21
SURA YA PILI ........ 23
MAPITIO YA MAANDISHI ........ 23
2.0 Utangulizi ........ 23

2.1 Dhana ya Ukiushi katika Tafsiri ........ 23
2.2 Ubunifu kama Kiashiria cha Ukiushi katika Tafsiri ........ 25
2.3 Athari ya Umilisi wa Mtafsiri ........ 28
2.4 Utamaduni Kama Kiashiria cha Ukiushi ........ 29
2.5 Ujuzi na Uzoefu katika Taaluma Husika ........ 30
2.6 Tofauti za Kiisimu baina ya Lugha Zinazohusika ........ 31
2.7 Aina ya Hadhira anayoilenga Mtafsiri ........ 32
2.8 Hitimisho ........ 33
SURA YA TATU ........ 34
AINA ZA UKIUSHI KATIKA MATINI TAFSIRI ........ 34
3.0 UTANGULIZI ........ 34
3.1 Mukhtasari wa Tamthilia ........ 34
3.2 Muundo wa Matini Chanzi na Matini Tafsiri ........ 36
3.3 Ukiushi wa Kifonolojia ........ 37
3.4 Ukiushi wa Kisintaksia ........ 40
3.5 Ukiushi wa Kisemantiki ........ 54
3.6 Hitimisho ........ 71
SURA YA NNE ........ 73
UMBUJI KAMA KIUNGO CHA UKIUSHI ........ 73
4.0 Utangulizi ........ 73
4.1 Umbuji Katika Ukiushi ........ 73

4.2 Tasifida kama Kiashiria cha Ukiushi ........................................................ 75
4.3 Matumizi ya Maneno ya Matini Chanzi bila Kuyatafsiri........................................ 78
4.4 Ubunifu wa Mtafsiri ........................................................................................ 80
4.5 Uziada kama Kiashiria cha Ukiushi ................................................................. 82
4.6 Uaminifu wa Matini Tafsiri............................................................................. 84
4.7 Hitimisho ...................................................................................................... 85
SURA YA TANO ................................................................................................. 87
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................... 87
5.0 Muhtasari wa Tasnifu ..................................................................................... 87
5.1 Mchango wa Utafiti ........................................................................................ 88
5.2 Mapendekezo ................................................................................................. 92
MAREJELEO ....................................................................................................... 95
KIAMBATISHO.................................................................................................... 99

# MAELEZO YA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| MA: | Matini Asilia |
| LC: | Lugha Chanzi |
| LP: | Lugha Pokezi |
| L1: | Lugha ya Kwanza |
| L2: | Lugha ya Pili |
| TT: | Tamthilia Tafsiri |
| TA: | Tamthilia Asilia |
| MC: | Matini Chanzi |
| ML: | Matini Lengwa |
| MT: | Matini Tafsiri |
| HL: | Hadhira Lengwa |
| HA: | Hadhira Asilia |
| TC: | Tamthilia Chanzi |

## MAELEZO YA ISTILAHI

| | | |
|---|---|---|
| Ukiushi | : | Kukaidi sheria na kaida za uandishi. |
| Utandawazi | : | Mfumo wa kiuchumi na kimawasiliano unaoyafanya mataifa ya ulimwengu yakurubiane na kuingiliana katika nyanja mbalimbali. |
| Uziada | : | Maelezo ambayo siyo ya lazima kukamilisha taarifa. |
| Umilisi | : | Ujuzi wa kanuni zinazotawala lugha fulani. |
| Umahiri | : | Ustadi wa kuitumia lugha kwa ufasaha na usahihi. |
| Uhawilishaji | : | Uhamishaji wa maana ya ujumbe katika tafsiri. |
| Ubunifu | : | Hali inayotokana na kitendo cha kubuni au kufinyanga wazo fikirani kwa kuwa na uwezo wa kutumia kanuni chache kuunda na kuelewa vipashio vingi. |
| Umbuji | : | Dhana yenye maana ya uzuri wa kazi ya kifasihi andishi kwa kufuata kaida zilizokubaliwa na wahakiki ili kupimia uzuri huo. |

## SHUKRANI

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliochangia kukamilika kwa utafiti huu na tasnifu hii kwa njia moja au nyingine. Naanza kwa kukishukuru Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, kwa kunisajili kama mwanafunzi wa shahada ya kwanza na kisha mzamili, mbali na kunipa mazingira mwafaka yaliyoniwezesha kuitekeleza kazi hii. Nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Kandagor na Dkt. Obuchi kwa mwongozo wao mwema katika utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Nawashukuru kwa moyo wa dhati wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret waliopo sasa na waliohamia katika vyuo vikuu vingine ama kwa kunifunza au kunipa mashauri na mawaidha mema ambayo yamenifaa sana maishani. Nawashukuru Prof. Ogechi na Prof. Mwamzandi kwa msingi imara walionipa katika maswala ya utafiti. Namshukuru mhadhiri niliyemuenzi na kumheshimu sana marehemu Prof. Shitemi kwa mashauri yake ya busara. Mungu amrehemu.

Shukrani zisokifani ziwaendee wafanyakazi wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika na wale wa Kitivo kizima cha Sanaa na Sayansi za Kijamii (SASS) wakiwemo wahazili na wahudumu wengine kwa kunipa motisha na matumaini kila nilipohisi kukata tamaa katika kazi hii ngumu ya utafiti na uandishi wa tasnifu hii.

Nawashukuru wazazi wangu wapendwa Mama Teresiah Wangarĩ Kamotho na marehemu Mzee Joseph Kamotho Njoroge kwa kujitolea kunisomesha. Ninawashukuru ndugu zangu wote wa kiume na wa kike kwa maombi na mashauri yao ya busara. Nashukuru jamaa zangu kwa utulivu na uvumilivu kila nilipokosekana nyumbani nikijizamisha katika kazi hii. Mke wangu Caro na wanangu Tracy, Soni na Jose, sijui nisemeje! Niliwahini mapenzi ya mume na baba kwa ajili ya kazi hii. Mungu awabariki kwa kunielewa na kunivumilia.

Subira yenu ilinitia motisha. Juu ya yote, namshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu Jalali ambaye neema na baraka zake zimeniwezesha kuitekeleza kazi hii. Jina lake lisifiwe daima milele. AMINA.

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Tafsiri ni sanaa, taaluma na vilevile utanzu muhimu sana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Sababu ni kwamba matangamano na maingiliano baina ya jamii mbalimbali zinazozungumza au kutumia lugha mbalimbali yameongezeka sana kutokana na utandawazi. Katika mchakato huu wa utandawazi, uhawili wa mawazo na maarifa kutoka lugha moja hadi nyingine hauepukiki. Venuti (1992) anasema kuwa zoezi la kutafsiri lipo nyakati zote miongoni mwetu ingawa halipewi hadhi inayostahili. Anaongeza kuwa watafsiri nao wamedidimiza sifa ya taaluma ya tafsiri kwa kuhusika zaidi na miradi ya kutafsiri makala ili kupata riziki huku wakipuuza maswala ya kujadili nadharia, mbinu na mikakati inayofaa kuzingatiwa katika zoezi la tafsiri au kuhakiki tafsiri zilizopata kuandikwa.

Taaluma ya tafsiri ina historia ndefu. Inakisiwa kuwa katika mwaka wa 3000 (Kabla ya Kristo), Elephantine, Mfalme wa Misri aliona maandishi ya lugha mbili tofauti ambayo yalikuwa yakizungumzia maudhui ya makala moja. Mfalme huyo alitambua kwamba maandishi hayo yalikuwa tafsiri za makala moja. Kufikia mwaka wa 300 (Kabla ya Kristo), tafsiri na maarifa ya tafsiri zilitumika barani Yuropa kueneza tamaduni, maarifa na teknolojia kati ya mataifa ya Ulaya. Taifa la Uyunani kwa mfano liliathiri dola ya Warumi kimaisha kutokana na tafsiri. Kupitia kwa tafsiri, Warumi nao waliathiri tamaduni zingine za Ulaya.

Maendeleo ya kisayansi na kiviwanda katika karne ya kumi na saba na kumi na nane yaliongezea haja ya taaluma ya tafsiri. Bidhaa zilizouzwa katika nchi mbalimbali zilihitaji maelezo katika lugha mbalimbali. Aidha, taaluma ya tafsiri iliwezesha Wajerumani na Waingereza kutafsiri Biblia kutoka Kigiriki. Martin Luther alitafsiri Biblia ya Kigiriki kwa Kijerumani (1522 BK). Mfalme James wa Uingereza aliidhinisha tafsiri ya Kiingereza ya Biblia kutoka Kigiriki (1611 BK). Baadhi ya wataalamu kama vile Jumpelt (1961), Benjamin (1963) na Arendt (1970) walidai kuwa karne ya ishirini ndiyo "Karne ya tafsiri" yaani karne yenye matumizi mengi ya tafsiri kutokana na mabadiliko na maendeleo katika nyanja tofauti maishani. Hivi leo, maisha ya kila siku ulimwenguni yanahusiana kwa njia moja au nyingine na fani hii ya tafsiri. Habari tunazozipokea kwenye vyombo vya habari huhusisha fani ya tafsiri kutoka lugha tofauti tofauti. Wataalamu wengi wanadai kuwa tafsiri ni sanaa maalum ambayo Venuti (1992) anaiita “special art or craft” yaani “usanii au sanaa maalum”. Asher na Simpson (1994) wanaiita “Translatology” yaani “Elimu ya tafsiri”. Tafsiri humaanisha uchukuaji wa mawazo yaliyomo katika maandishi kutoka lugha moja na kuyaweka katika mawazo yanayolingana kuelekea kwenye lugha nyingine (Cartford 1965).

Wataalamu wengi mathalani Cartford, Newmark na Nida wanadai kuwa tafsiri ni kubadilisha makala kutoka hali moja hadi hali nyingine kwa kuhamisha maana kutoka lugha ya awali (L1) hadi kwenye lugha ya pili (L2). Watafsiri huzingatia muundo wa kisemantiki wa Matini Asilia na Matini Pokezi. Matokeo yake ni kwamba muundo na mitindo kati ya Lugha Chanzi na Lugha Lengwa huwa tofauti. Wilss (1982) na Dostert (1985) wanadai kwamba tafsiri ni harakati za kubadilisha makala kutoka maumbo ya lugha

ya kwanza hadi kwenye lugha ya pili. Newmark (1988) anasema kuwa mtafsiri hanakili tu kilichoandikwa bali hujiweka katika hali ya kuelewa kinachosemwa au kilichoandikwa ili akihamishe na kukieleza yeye mwenyewe hadi lugha pokezi. Hata hivyo, tafsiri ya namna hiyo haiwezi kuwa sawa kikamilifu kwa kuandikwa katika lugha halisi. Aghalabu, Matini Tafsiri huwa imekiuka au imepotoka kwa kiasi fulani kutoka Matini Chanzi kisarufi, kisemantiki, kiuakifishaji au kileksia. Cartford (1965) anaposema tafsiri ni uhawilishaji wa mawazo yanayolingana, ana maana kuwa si mawazo sawa kabisa kati ya maandishi ya Lugha Asili na Lugha Pokezi, kwani haiwezekani kuwa na usawa kamili kati ya Matini Chanzi na Matini Tafsiri.

Katika kuitafsiri tamthilia Nitaolewa Nikipenda kutoka kwa Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda*, ukiushi ulijitokeza katika Matini Tafsiri. Ukiushi huu ulijitokeza kutokana na tofauti za kiisimu, kitamaduni na kimazingira kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi. Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* iliandikwa kwa Gĩkũyũ na Ngũgĩ wa Thiong'o wakishirikiana na Ngũgĩ wa Mĩriĩ katika mwaka wa 1977 na kuchapishwa mwaka wa 1980. Matini Tafsiri ya Kiswahili ya *Nitaolewa Nikipenda* ilitafsiriwa na Clement Kabugi katika mwaka wa 1982. Waandishi wa MC (Ngũgĩ wa Thiong’o na Ngũgĩ wa Mĩriĩ) vilevile walitoa Matini Tafsiri ya Kiingereza ya *I Will Marry When I Want* mwaka wa 1982 ambayo ni kimelea cha au tafsiri ya ile Matini Chanzi ya Gĩkũyũ.

## 1.2 Historia Za Waandishi Wa Matini Chanzi Na Matini Tafsiri

Ngũgĩ wa Thiong’o na Ngũgĩ wa Mĩriĩ walishirikiana na wafanya kazi na wakulima wadogo wadogo kuubuni mchezo wa kuigiza wa *Ngaahika Ndeenda*. Waandishi wa Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* walitwikwa jukumu la kubuni mchezo huu wa kuigiza na kamati kuu ya kituo cha kitamaduni cha Kamĩrĩĩthũ, Limuru. Mchezo huu

ulikusudiwa kukuza utamaduni, kutumbuiza wakazi na kuonyesha maisha yao yalivyokuwa wakati huo. Mchezo huu wa kuigiza ulitazamwa na wakazi wengi wa eneo hilo mwishoni mwa mwaka wa 1977. Mtafsiri wa MT, Clement Kabugi alikuwa mwalimu wa Lugha na Fasihi ya Kiswahili. Ameandika vitabu vya kufundishia lugha ya Kiswahili katika kiwango cha sekondari nchini Kenya. Kabugi ni mzungumzaji asili wa lugha ya Gĩkũyũ, jambo lililomwezesha kuitafsiri tamthilia Ngaahika Ndeenda kwa Kiswahili. Hii ni kwa kuwa ni hitaji la kimsingi kuwa mtafsiri awe na umilisi wa kutosha wa Lugha Chanzi na Lugha Pokezi ili kufanikisha kazi yake.

Katika kukabiliana na vikwazo na matatizo mbalimbali yanayoletwa na tofauti za kitamaduni na kimazingira kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi, tafsiri hutumia mbinu mbalimbali. Baadhi ya mbinu hizi ni uaminifu, ubadalia, tafsili na ukwepi. Baker (1992), Fawcett (1997). Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza kama mtafsiri anakiuka maneno, vishazi, nahau na viakifishi anapokuwa akiitafsiri Tamthilia *Ngaahika Ndeenda* hadi tamthilia *Nitaolewa Nikipenda.*

## 1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu umehusika na aina mbalimbali za ukiushi uliojitokeza katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* kama ilivyotafsiriwa kutoka Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda*.Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* iliandikwa kwa Gĩkũyũ na Ngũgĩ wa Thiong’o wakishirikiana na Ngũgĩ wa Mĩriĩ (1977) na kuchapishwa mnamo mwaka wa 1980. Waandishi wa Tamthilia Chanzi walitoa tafsiri nyingine ya Kiingereza ya *I Will Marry When I Want* mwaka wa 1982.

Utafiti huu umeangazia maneno, vishazi, sentensi, aya na viakifishi. Tumevichunguza vipengele hivi katika kutathmini iwapo mwandishi wa Tamthilia Tafsiri alivikiuka na kuviandika kinyume au tofauti na vilivyowakilishwa katika Matini Chanzi. Mifano yote ya ukiushi katika vipengele hivi kati ya Tamthilia Chanzi na Tamthilia Tafsiri imeorodheshwa, ikachunguzwa na kujadiliwa. Aidha, tumechunguza sababu ya ukiushi huo kujitokeza katika Matini Tafsiri. Hatukujua kama ukiushi umejitokeza katika Matini Tafsiri kabla ya kuuanza utafiti huu. Kwa ajili hii utafiti ulitaka kudhibitisha kama kweli ukiushi upo na iwapo umejitokeza katika Tamthilia Tafsiri tuliyoishughulikia. Hii ni kwa sababu wataalamu wengi wa taaluma ya tafsiri wanadai kuwa haiwezekani kuwa na tafsiri timilifu kabisa isiyo na dosari au makosa madogo ya kiukiushi.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

1. Kutathmini iwapo ukiushi unajitokeza katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda.*
2. Kuchanganua ukiushi unavyojitokeza katika Matini Tafsiri.
3. Kujadili aina za ukiushi ziliziko kwenye Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*.
4. Kutathmini umbuji kama kiungo cha ukiushi katika Matini Tafsiri.

### 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete kwamba:

1. Ukiushi umejitokeza katika tafsiri ya Kiswahili ya *Nitaolewa Nikipenda.*
2. Ukiushi unaojitokeza unamwezesha mtafsiri kuwasiliana na hadhira yake kwa njia mwafaka.

3. Aina mbalimbali za ukiushi zimejitokeza katika Tamthilia Tafsiri.
4. Umbuji kama kiungo cha ukiushi umejitokeza katika Matini Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda.*

## 1.5 Upeo wa Utafiti

Kwa kuwa utafiti huu umechunguza tafsiri ya tamthilia *Ngaahika Ndeenda* ya Gĩkũyũ na jinsi ilivyotafsiriwa katika Kiswahili kama *Nitaolewa Nikipenda*, dhana na Nadharia ya Tafsiri zimefafanuliwa mwanzo. Hii ni muhimu kwa kuwa Matini Tafsiri (MT) ni tafsiri ya Matini Chanzi (MC). Tamthilia Chanzi na Tamthilia Tafsiri zimesomwa kwa makini kama hatua muhimu katika utafiti huu.

Tumechunguza ukiushi ulivyojitokeza katika tamthilia *Nitaolewa Nikipenda* (TT) kama ilivyotafsiriwa kutoka tamthilia *Ngaahika Ndeenda* (TC) iliyoandikwa kwa Gĩkũyũ. Tumechunguza namna ukiushi umevyojitokeza na sababu ambazo zimepelekea ukiushi huo kujitokeza katika Matini Tafsiri. Aidha, aina mbalimbali za ukiushi ulioko mathalani ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kisemantiki na ukiushi wa kisintaksia (kisarufi) zimeainishwa na kutolewa mifano katika Tamthilia Chanzi na Tamthilia Tafsiri. Sababu ya utafiti huu kushughulikia ukiushi pekee na kuacha mbinu nyinginezo za tafsiri ni kutokana na kuwa baadhi ya mbinu hizi tayari zimeshashughulikiwa au zimeshatafitiwa. Shitemi (1997) alitafitia uaminifu katika tafsiri huku akiangazia tenzi za ushairi wa jadi. Aidha, Igendia (2003) alitafitia Mtindo katika Tafsiri ya Kiingereza ya *The Government Inspector* na tafsiri ya Kiswahili ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* kwa kuzilinganisha kimtindo. Tofauti na uchambuzi mwingine wa kifasihi unaochunguza wahusika, maudhui, ploti, dhamira na mtindo, utafiti huu uliangazia ukiushi kama ulivyojitokeza katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*.

Ukiushi huwa na athari katika vipengele vya kifasihi mathalani wahusika, maudhui, ploti dhamira na mtindo. Kwa upande wa wahusika, ukiushi huathiri sifa na hulka za wahusika pale ambapo wahusika wamepewa majina ya kimajazi. Katika Tamthilia Chanzi tuliyoishughilikia ya *Ngaahika Ndeenda*, wahusika karibu wote wamepewa majina ya kimajazi yaani majina yanayolingana na sifa za wahusika hao. Mtafsiri aliwapa wahusika hao majina yaleyale waliyopewa katika MC. Ukiushi ulijitokeza pale ambapo mtafsiri alimpa mhusika Jespheli jina lenye herufi 'ph' ambazo haziwezi kufuatana kulingana na kanuni za Lugha Pokezi (Kiswahili). Mtafsiri aliendeleza ukiushi huo kwa kuwapa wahusika majina yao asilia ya Gĩkũyũ badala ya kuyatafsiri au kuwapa majina ya kimajazi ya Kiswahili. Maudhui ya kazi za kifasihi na kazi zisizo za kifasihi yanaweza kuathiriwa na ukiushi wa mtafsiri pale ambapo ukiushi huo utaathiri maana ya ujumbe wa kazi husika. Ukiushi wa kisemantiki, kwa mfano ukiushi wa maana ya maneno, huathiri maudhui yaliyokusudiwa na mwandishi wa Matini Chanzi. Ploti ni msuko wa matukio katika kazi ya kifasihi. Msuko wa matukio utaweza kuathiriwa tu iwapo mtafsiri amebadilisha mtiririko wa matukio katika Matini Pokezi tofauti na ulivyo katika Matini Chanzi. Mtafsiri wa matini tuliyoishughulikia katika utafiti huu hakukiuka msuko wa matukio katika tafsiri yake bali alizingatia msuko ule ule ulioko kwenye Matini Chanzi.

Dhamira ya Mwandishi Asilia itaweza kuathiriwa endapo ukiushi wa mtafsiri utaathiri maudhui ya kazi-husika, iwe ya kifasihi au isiyo ya kifasihi. Mtindo katika kazi ama ya kifasihi au isiyo ya kifasihi utaweza pia kuathiriwa na ukiushi hasa pale ambapo mtindo wa uandishi na uakifishaji kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi huwa tofauti kwa mfano kati ya Kiingereza na Kifaransa. Tamthilia ya Kifaransa hutumia vistari vifupi wakati

tamthilia ya Kiingereza ama Kiswahili hutumia koloni (nukta mbili) katika mazungumzo (dayalojia) kuonyesha maneno yaliyotamkwa na mhusika.

Utafiti huu umejikita katika kulinganisha Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* na Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* kwa kudondoa maneno, sentensi, vishazi na viakifishi vilivyokiukwa na mtafsiri alipokuwa akiitafsiri MT kutoka MC. Vipenglele hivi vilivyokiukwa vimejadiliwa na kufafanuliwa ili kuonyesha jinsi ukiushi wa mtafsiri ulivyojitokeza. Aidha utafiti huu umejihusisha na kubainisha aina mbali mbali za ukiushi zilizojitokeza katika matini tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*. Mifano ya aina za ukiushi zilizoko kwenye Matini Tafsiri zimejadiliwa na kufafanuliwa..

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Mawasiliano katika tafsiri ya Nida (1964) inayojikita katika Mlingano Endelevu (Dynamic Equivalence) katika tafsiri. Kwa mujibu wa nadharia hii, utafiti huu umejihusisha na kuchunguza iwapo mawasiliano mwafaka yamepatikana kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Lengwa na iwapo athari kati ya MC na Hadhira Chanzi ni sawa na athari iliyopo kati ya MT na Hadhira Pokezi. Kwa kuwa utafiti huu umejihusisha na uchunguzi wa vitabu husika maktabani, zikiwemo tamthilia husika na vitabu vya mwanadharia wa tafsiri mathalani Nida (1964, 1969), Cartford (1965) na Newmark(1988), mbinu kuu inayohusika katika utafiti huu ni uchunguzi wa vitabu na kazi hizo maktabani. Utafiti wetu haujihusishi na mbinu nyinginezo za tafsiri zilizotumiwa na mtafsiri, ila tu ukiushi. Ukiushi ni ukiukaji wa sheria na kaida za uandishi.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Inawasiliwa kuwa utafiti huu utawasaidia watafsiri wa baadaye wa fasihi za lugha nyingine zilizotafsiriwa katika Kiswahili kubaini sababu ya kukiukwa kwa mambo fulani ama kaida

fulani za uandishi katika tafsiri. Aidha, utafiti huu utatusaidia kubainisha msamiati tatanishi unaotumiwa katika nyanja za tafsiri mathalani tofauti kati ya Matini Asilia na Matini Chanzi. Utafiti huu wa ukiushi katika tafsiri ni muhimu kwa sababu utaongezea maarifa ambayo tayari yako katika taaluma na sanaa ya tafsiri. Hii ni kwa sababu utafiti umebainisha ukiushi wa aina mbalimbali na vilevile kuchunguza sababu za ukiushi huo kujitokeza. Mchango kama huu katika fani ya tafsiri ni muhimu tukizingatia dhima kubwa ya taaluma ya tafsiri maishani. Utafiti huu utawafaidi wanaohusiana na taaluma ya tafsiri kwa njia moja au nyingine wakiwemo wanahabari, wasomi, waandishi na watafsiri kwa kuchangia katika ujuzi uliopo wa tafsiri na ukiushi unavyojitokeza katika tafsiri.

Mfano mmoja wa kuonyesha dhima ya tafsiri ni katika harakati zilizokuwako za kuunda katiba mpya nchini Kenya mwaka wa 2006-2008 ambapo wananchi walikuwa wanadai tafsiri ya Katiba Kielelezo katika lugha mbalimbali na hasa Kiswahili. Umuhimu wa taaluma ya tafsiri ulifanya Baraza la Mitihani la Kenya kuhusisha swali au zoezi la tafsiri kati ya Kiingereza na Kiswahili kuwa la lazima katika mtihani wa Kiswahili wa kidato cha sita kabla ya mfumo mpya wa elimu wa 8-4-4 uliozinduliwa mwaka wa 1985. Inafaa kuhusisha tafsiri katika mtihani wa kidato cha nne hivi sasa. Aidha zoezi la tafsiri huwa ni la lazima katika mfumo wa masomo wa kimataifa.

Kwa muhtasari, inatarajiwa kwamba utafiti huu kuhusu ukiushi katika tafsiri utachangia katika kuikuza na kuiendeleza taaluma ya tafsiri ambayo dhima yake inazidi kuongezeka kila uchao, hasa kutokana na utandawazi. Venuti (1992) anatoa mfano wa Misri na Ufaransa katika miaka ya 1830 ambapo tafsiri kati ya Kifaransa na Kiarabu ilitumiwa kuchapuza maendeleo nchini Misri.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu, umeongozwa na *Nadharia ya Mawasiliano katika Tafsiri* (Nida 1964) ambayo imetusaidia na kutuwezesha kuufanya uchambuzi linganifu wa Matini Tafsiri kwa kuilinganisha na Matini Chanzi. Ulinganishi huu wa Matini Chanzi na Matini Tafsiri umemwezesha mtafiti kuchunguza jinsi ukiushi unavyojitokeza mbali na kutaka kujua kile kinachopelekea ukiushi huo. Nida amehusika pakubwa katika uandishi wa Tafsiri ya Biblia ya *Good News Bible.* Anaelezea aina mbili za mlingano katika tafsiri; Mlingano Rasmi (Formal Equivalence) na Mlingano Endelevu (Dynamic Equivalence). Mlingano Endelevu unasisitiza mawasiliano mwafaka kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi na vilevile kuweko kwa athari sawa ya ujumbe kati ya hadhira ya Matini Asilia na hadhira ya Matini Tafsiri (Matini Pokezi).

Mlingano Rasmi kwa upande mwingine unasisitiza usawa wa kimsamiati, kisarufi na kimuundo kati ya Matini Chanzi na Matini Tafsiri. Mlingano Rasmi unaweza kukosa kuleta mawasiliano mwafaka kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi na ndipo tumekita utafiti huu katika Mlingano Endelevu ambao unasisitiza mawasiliano mwafaka kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi. Mawasiliano haya kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi ndiyo yanayosababisha pawe na athari sawa ya ujumbe kati ya Hadhira Asilia na Hadhira Pokezi. Ni Mlingano Endelevu unaoifanya hadhira ya Matini Tafsiri ipate athari sawa ya ujumbe kama vile hadhira ya Matini Chanzi. *Nadharia ya Mawasiliano katika Tafsiri* ina msingi wake katika Nadharia ya Tafsiri. Akimnukuu Mwansoko (1996), Igendia (2003) anadai kuwa Nadharia ya Tafsiri ni jumla ya maarifa yaliyopo na yanayopatikana kuhusu mchakato wa kutafsiri, kuanzia misingi na kanuni za jumla hadi miongozo, mapendekezo na vidokezo muhimu. Nadharia ya Mawasiliano katika Tafsiri ya Nida (1964,) kwa upande

wake, inapendekeza kuwepo kwa mawasiliano mwafaka kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Lengwa. Aidha, Nadharia ya Mawasiliano katika Tafsiri ya Nida inapendekeza kuwepo kwa athari sawa kati ya Matini Chanzi na Hadhira Asilia na Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi.

Nadharia ya Tafsiri ndiyo nguzo na mhimili wa shughuli ya tafsiri na msingi wa kazi zote za kitafsiri. Nadharia hii ni maelekezo juu ya vipengele vya kitafsiri vinavyofaa kuzingatiwa na kila mtafsiri anapokabiliwa na kazi ya kutafsiri. Mwasisi wa Nadharia yaTafsiri ni Nida (1964). Msimamo huu unaungwa mkono na Larson (1983) kuwa tafsiri ni kubadilisha makala kutoka hali moja hadi hali nyingine. Ubadilishaji huo unahusu uhamishaji wa maana kutoka lugha ya awali (L1) hadi kwenye lugha ya pili (L2) kwa kuzingatia muundo wa kisemantiki. Matokeo ya uhamishaji huu wa maana ni kwamba maumbo kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi huwa tofauti.

Akikubaliana na kauli ya Nida (1964) kuwa Mlingano Endelevu (Dynamic Equivalence) katika tafsiri ni zaidi ya mawasiliano sahihi ya habari kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi, Newmark (1988) anajadili kuwa hoja ya kuwepo athari sawa ya ujumbe kwa Hadhira Asilia sawa na kwa Hadhira Pokezi ndiyo kaida ya kimsingi kabisa inayofaa kuzingatiwa na watafsiri wote licha ya kuwa ni vigumu kukisia au kupima kiwango cha athari ya ujumbe kwa hadhira husika. Katika utafiti wangu, nimetumia *Nadharia ya Mawasilianokatika Tafsiri* (Mlingano Endelevu) ya Nida na kuona jinsi mawasiliano yalivyo kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi na vilevile kuchunguza iwapo athari ya ujumbe wa Matini Chanzi kwa Hadhira Asilia inalingana na athari ya ujumbe wa Matini Tafsiri kwa Hadhira Pokezi. Hata hivyo, haiwezekani kuwa na tafsiri iliyo sawa kabisa na Matini Chanzi. Cartford anajadili kwamba, “Kutafsiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika

maandishi kutoka lugha moja (Lugha Chanzi) na kuyaweka katika mawazo yanayolinganalingana kuelekea lugha nyingine (Lugha Lengwa)."

Newmark (1982) anasema kuwa Nadharia ya Tafsiri ilianzishwa katika miaka ya 1960 kutokana na wingi wa makosa katika tafsiri zilizokuwa zimechapishwa na vilevile kuweko kwa ongezeko kubwa la asasi zinazoshughulikia nyanja za tafsiri. Aidha, kulikuwepo na istilahi katika taaluma mbalimbali hasa za sayansi na teknolojia zilizoleta haja ya kuzisanifisha ili kufanikisha tafsiri kati ya lugha tofauti tofauti. Kwa mujibu wa Mwansoko (1996), Nadharia ya Tafsiri basi si nadharia kama zile za kisayansi bali ni maelekezo ya mambo yanayofaa kuzingatiwa na mtafsiri anapojishughulisha na zoezi la tafsiri. Jukumu la Nadharia ya Tafsiri ni kuamua na kupendekeza taratibu mwafaka za kutafsiria makala za namna mbalimbali.

Wilss (1982) anadai kuwa tafsiri ni harakati ya kubadilisha makala kutoka kwenye maumbo ya lugha ya kwanza hadi kwenye lugha ya pili. Ingawa ninakubaliana na dai hili, si lazima maumbo ya lugha yabadilike katika kila kifungu cha tafsiri. Wakati mwingine, umbo katika Makala Asilia na Makala Tafsiri yanaweza kulingana katika kiwango cha sentensi lakini ni nadra kwa maumbo hayo kulingana katika matini nzima. Akichangia dhana na Nadharia ya Tafsiri, Newmark (1988) anajadili kuwa hakuna tafsiri yoyote inayoweza kuwakilisha mawazo yaliyomo katika makala halisi. Kwa hivyo, jukumu la mtafsiri si kunakili kinachosemwa au kilichoandikwa bali ni kujiweka katika hali ya kuelewa kinachosemwa au kilichoandikwa ili akihamishe katika hali ya kuweza kukieleza yeye mwenyewe. Hili hata hivyo si rahisi kulifikia kwani kila lugha na jamii huwa na mfumo wake tofauti kiisimu, kitamaduni, kihistoria na kimazingira. Kwa hivyo ni vigumu kutafsiri mawazo ya jamii moja katika lugha ya jamii nyingine bila kupoteza, kupotosha

au kukiuka maana. Nadharia ya Tafsiri inapendekeza basi kuwa ujumbe katika MC na MT ulingane. Hata hivyo, ingawa si lazima tafsiri iwe sawa kabisa kati ya MC na MT, ni jukumu la mtafsiri kuleta ulinganifu mkubwa iwezekanavyo kati ya MC na MT licha ya matatizo ambayo hayawezi kuepukika.

Ingawa utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Nida ya Mawasiliano katika Tafsiri, nadharia ya Leech (1969) imechangia katika utafiti huu. Leech anadai kuwa kile kinachofanya ushairi kupendeza ni ukiushi wake kutoka kwa lugha ya kawaida na badala yake kutumia lugha mbadala kudhihirisha umbuji. Kinachotofautisha utafiti wetu na nadharia ya Leech ni kuwa utafiti huu unazingatia ukiushi katika tafsiri ya maandishi nathari (tamthilia) wala sio ushairi. Hata hivyo, mawazo ya Leech yamesaidia katika uchanganuzi wa baadhi ya nyimbo katika tamthilia. Aidha uainishaji wa ukiushi katika utafiti huu unakaribiana na ule wa Leech.

Katika utafiti huu, nimechunguza jinsi ujumbe katika Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* unalingana na ujumbe ulioko katika Matini Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*. Ulinganifu wa ujumbe katika tamthilia hizi mbili; ya Gĩkũyũ na ya Kiswahili, unadhihirisha kuwa dhamira ya waandishi wa TC na dhamira ya mtafsiri wa kazi hiyo zitawiana. Aidha, ulinganifu wa ujumbe katika Tamthilia Chanzi na Tamthilia Tafsiri umesababisha maudhui katika tamthilia hizi mbili yaoane. Nimetilia maanani hoja kwamba si lazima tafsiri iwe sawa kabisa kati ya MC na MT kutokana na tofauti za kiisimu na kifonetiki kati ya LA na LP. Tofauti za kitamaduni kati ya hadhira za tamthilia hizi mbili ziliathiri tafsiri. Kwa mfano, semi za Lugha Chanzi zimetofautiana na semi za Lugha Pokezi. Ni mapendekezo ya *Nadharia ya Mawasiliano katika Tafsiri* ya Nida iliyotuongoza katika utafiti huu kuwa mtafsiri ajaribu kadiri awezavyo kuleta ulinganifu unaowezesha mawasiliano mwafaka

zaidi iwezekanavyo kati ya Matini Chanzi na Matini Tafsiri. Tuliangazia namna ukiushi ulivyokidhi au kuathiri hoja hii ya ulinganifu na jinsi ukiushi huu ulivyoathiri mawasiliano katika tafsiri tuliyoishughulikia.

### 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Watafiti mbalimbali wameshughulikia uwanda wa tafsiri. Baadhi yao ni kama vile Nida (1964), Cartford (1965) na Newmark (1988). Hawa walishughulikia Nadharia ya Tafsiri kwa kutoa mwongozo kuhusu jinsi na hatua za kuzingatia na kufuata katika shughuli ya kutafsiri makala kutoka Lugha Chanzi hadi kwenye Lugha Pokezi. Hii haimaanishi kwamba hapakuwepo na maingiliano miongoni mwa lugha mbalimbali kabla ya wananadharia hao. Zoezi la kutafsiri ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine lilikuwepo tangu jadi ila hakukuwa na nadharia maalum iliyozingatiwa kutafsiri makala kati ya lugha mbalimbali.

Cartford (1965), Larson (1984) na Newmark (1988), ni baadhi ya wataalamu ambao wamejadili *Nadharia ya Tafsiri*. Aidha, wengine wamejadili mikakati mbalimbali inayotumiwa katika taaluma ya tafsiri mathalani Baker (1992), na Fawcett (1997). Tulionelea kuwa wataalamu hawa wote wametoa mchango mwafaka katika taaluma ya tafsiri kwani vidokezo na maelekezo yao yatawapa watafsiri wa baadaye maarifa ambayo yatawawezesha kuandika tafsiri bora na zenye usahihi zaidi. Mtafsiri anaweza kuamua kukiuka maana za baadhi ya maneno au semi za Lugha Chanzi ikiwa maneno au semi hizo zitaleta maana isiyokuwepo, isiyoeleweka, isiyokubalika au maana potoshi katika Lugha Pokezi. Hii ni kwa sababu jamii lugha mbalimbali ulimwenguni zina mila, tamaduni, miktadha na itikadi tofauti-tofauti.

Nimeonelea kuwa uwanda wa ukiushi katika tafsiri haujafanyiwa utafiti mwingi na wa kutosha.Ninadai hivyo kwa sababu ni adi kupata vitabu vya kiada na tasnifu za wasomi zenye anwani zinazolenga moja kwa moja mada au dhana ya ukiushi ni adimu . Hata hivyo, baadhi ya wataalamu wamegusia suala la ukiushi japo hawakulizamia kwa kina kwani haikuwa mada ya utafiti wao. Waandishi wengi wameitafitia dhana ya tafsiri kwa upana na wengine wametafitia nyanja zinginezo za tafsiri. Suala la utafiti halijashughulikiwa na tafiti za awali hasa kuhusiana na ukiushi katika tafsiri za kazi za kisanaa zinazotumia lugha asilia za nchi ya Kenya kwani ni kazi chache za kifasihi zilizokwisha kuandikwa kutumia lugha asilia za nchi hii. Aidha ni kazi chache zaidi za Lugha Asilia za Kenya ambazo zimetafsiriwa katika lugha nyinginezo.

Katika miaka ya 1990 na 2000, watafiti wengine mathalani, Mwansoko (1992), Venuti (1992), Baker (1992), Shitemi (1997) na Igendia (2003) wameishughulikia taaluma ya tafsiri. Newmark (1988) anadai kuwa tafsiri ni sanaa inayohusisha juhudi za kujaribu kuwakilisha ujumbe au taarifa iliyoandikwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Anaongeza kuwa mtafsiri anafaa kusoma na kuielewa makala na kuiainisha kabla ya kuamua mbinu atakazotumia kuitafsiria makala hiyo kwa lugha nyingine.

Ukiushi katika tafsiri hutokea makala yanapodhihirisha mtindo rasmi au sajili maalumu, badala ya lugha ya kawaida na kuwasilisha urasimu au umaalumu kwa njia badalia (Shitemi 1997). Ukiushi hutokana na mambo ya kimsingi yanayotokana na dhihirisho la mtafsiri kwenda kinyume au kutoa maana ambayo si kisawe cha maana asilia hata kama ni kwa faida yake au ya Hadhira Lengwa. Aidha, ukiushi unaweza pia kutokana na tofauti katika umilisi na tajriba za mtafsiri za kisaikolojia kwa upande wa uamilifu wa lugha kama chombo cha mawasiliano, na uhalisia na umilisi wa kimaudhui na kimantiki katika ujumbe

husika na unavyosawiriwa katika Matini Chanzi.Ukiushi wa ukawaida katika tafsiri huweza pia kusababishwa na ubunifu na ubinafsi wa mtafsiri, na dhamira zake katika kutafsiri. Umbuji wa kisanii unapokiuka turathi za Hadhira Asilia na kudhihirisha upekee wa utungo katika Matini Pokezi hutokana na ukiushi wa mbinu za utunzi zinazotumiwa na mtafsiri.

Huddleston (1976), anadai kuwa maelezo ya ki-ukiushi si makosa yanayotokea kwa bahati mbaya wala si matokeo ya udhaifu wa mtafsiri, bali yanatumiwa kimakusudi kabisa ili kuzikiuka maana, kanuni au mila kwa ajili ya mawasiliano mwafaka zaidi kwa ajili ya Hadhira Lengwa. Haitoshi tu kulinganisha MA na MT bali ni muhimu pia kutalii ulimwengu mpana ambamo makala hizi ziliandaliwa (Shitemi 1997). Utafiti wetu wa ukiushi katika tafsiri ulikuwa ni njia moja ya kuihakiki MT kwa kuzingatia utimizaji wa dhamira ya mtafsiri katika kuwasiliana na Hadhira Pokezi na pia kuzingatia vimiliki alivyoazimia kuvishughulikia. Shitemi (1997) ametafitia suala la uaminifu katika tafsiri kwa nia iyo hiyo huku akijikita katika uhakiki wa tafsiri za ushairi wa jadi wa Kiswahili.

Igendia (2003) anapendekeza  kuwa ukiushi katika tafsiri sio makosa, upotovu au udhaifu wa mtafsiri bali ukiushi unaweza kuwa ni ubunifu makusudi wa mtafsiri uliofanywa kwa kuongozwa na mazingira na utamaduni wa Lugha Pokezi. Akimnukuu Mwansoko (1996), Igendia anadai kuwa mambo yanayodhibitiwa na utamaduni na yanayohitaji ubunifu ni pamoja na msamiati wa ekolojia (kwa mfano majina ya misimu), violwa (kwa mfano maneno ya sayansi na teknolojia), ulaji (majina ya vyakula vinavyoliwa tangu asubuhi hadi jioni), vinywaji (kwa mfano majina ya vinywaji na vileo), nguo (kwa mfano aina za nguo zivaliwazo na watu) na siasa (kwa mfano istilahi za kisiasa).

Leech (1969) anasema kuwa sababu zinazowafanya watafsiri kukiuka baadhi ya kaida ni kuyazidisha mawasiliano, kuizidisha makini yake na pia kumchochea mtafsiri anayehusika ili atafakari juu ya umuhimu wa ukiushi huo. Hata hivyo, Igendia alichukua mwelekeo tofauti na utafiti huu wetu kwa kuwa tumeuchukua ukiushi kama kiashiria cha ubunifu katika tafsiri. Hii ni kwa sababu mtafsiri ana uhuru wa kuwasiliana na Hadhira Pokezi yake akiongozwa na Lugha Tafsiri, utamaduni na mazingira ya Hadhira Pokezi (Asher na Simpson (1994). Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa, ni wazi kwamba mtafsiri huzikiuka sheria, kanuni na kaida za uandishi ili athari inayopatikana katika Matini Tafsiri ilingane na ile iliyopatikana katika Matini Chanzi kwa kutumia maana ya ujumbe kama kaida.

### 1.8.1 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika maktaba mbalimbali nchini ambapo maandishi ya wataalamu mbalimbali wa tafsiri yalipitiwa. Katika uchunguzi huu wa maktabani, tulividurusu vitabu vilivyoandikwa juu ya ukiushi katika tafsiri. Aidha, kamusi mbalimbali zilirejelewa ili kulinganisha vishazi, sentensi na maneno yaliyotumiwa katika Tamthilia Chanzi na yale yaliyotumiwa katika Tamthilia Tafsiri. Vilevile, vitabu mbalimbali vya kiada na kitaaluma vinavyozungumzia dhana na nadharia ya tafsiri na ukiushi katika tafsiri vilisomwa na mawazo yao kunakiliwa.

Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* ilisomwa kwa kina na kisha Tamthilia Tafsiri ya Kiswahili ya *Nitaolewa Nikipenda* ikasomwa kwa makini huku kaida zozote za uandishi zilizokiukwa na mtafsiri Kabugi zikinukuliwa katika daftari na kupigiwa mistari katika Matini Chanzi na katika Matini Tafsiri.

Tunabainisha hapa kuwa Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* ilitafsiriwa kutoka Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda*. Tamthilia Tafsiri ya Kiingereza ya *I Will Marry When I Want* vilevile ilitafsiriwa kutoka Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda*. Ithibati iliyoko kuonyesha kuwa *Nitaolewa Nikipenda* na *I Will Marry When I Want* ni tafsiri mbili za Matini Chanzi moja ni kuwa tafsiri zote mbili zilichapishwa mwaka wa 1982, miaka miwili baada ya Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* iliyochapishwa mnamo 1980. Aidha, vitabu vya kihistoria vinavyoelezea historia ya waandishi wa Tamthilia Chanzi (Ngũgĩ wa Thiong'o na Ngũgĩ wa Mĩriĩ) na mtafsiri Clement Kabugi aliyetafsiri tamthilia hiyo kwa Kiswahili vilichunguzwa ili kujua mazingira ya kijumla yaliyowaathiri na kuwapelekea Ngũgĩ wa Thiong'o na Ngũgĩ wa Mĩriĩ kuandika Tamthilia Chanzi na Clement Kabugi kuitafsiri kwa Kiswahili. Miongozo ya kihakiki ya wasomi tofauti kuhusu tamthilia hizi ama katika Gĩkũyũ au Kiswahili iliweza kuchangia kupata data muhimu katika utafiti huu. Vitabu teule vya wananadharia na wataalamu mbalimbali wa tafsiri pamoja na tasnifu za wasomi wa taaluma ya tafsiri zilisomwa ili kupata mawazo yao kuhusu dhana, Nadharia ya Tafsiri na dhana ya ukiushi katika tafsiri.

Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndenda* imesomwa yote kwa mfululizo kama hatua ya kwanza. Hatua hii imefuatwa na ile ya kuisoma Matini Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* pia kwa mfululizo. MC na MT zimesomwa tena kwa makini huku tukipigia mistari maneno, vifungu na viakifishi vyote vilivyokiukwa na mtafsiri. Mistari hiyo imepigwa chini ya maneno, vifungu na viakifishi vyote vyenye ukiushi katika tamthilia zote mbili; TC na TT, ili kufanyia ulinganishi. Mbali na kutambua ukiushi uliopo na ulivyojitokeza katika tamthilia Nitaolewa Nikipenda kama ilivyotafsiriwa kutoka *Ngaahika Ndeenda*, tumeainisha kila aina ya ukiushi. Kwa kuwarejelea wataalamu na waandishi mbalimbali

wa taaluma ya tafsiri mathalani Nida, Cartford, Larson, Newmark, Shitemi na wengineo, tumechunguza sababu ya mtafsiri kukiuka sheria na kaida za uandishi alipokuwa akitafsiri tamthilia hiyo kutoka LC (Gĩkũyũ) hadi LP (Kiswahili). Tumechunguza, vilevile, jinsi semi za kitamaduni zilivyotafsiriwa kutoka LC hadi kwenye LP ili kuthibitisha jinsi ukiushi unavyojitokeza katika kuitafsiri MT kutoka MC.

### 1.8.2 Vifaa vya Utafiti

Kwa kuwa utafiti huu umejikita zaidi katika uchunguzi wa vitabu mbalimbali maktabani, vifaa tunavyotumia katika utafiti huu ni kamusi mbalimbali za Kiswahili pamoja na vitabu mbalimbali teule vya kiada vilivyoandikwa na wananadharia, wataalamu, wasomi na waandishi mbalimbali wa taaluma ya tafsiri. Aidha tumevitumia vitabu mbalimbali vyenye maelezo kuhusu semi, nahau, na methali za lugha (au jamii) ya Gĩkũyũ ambayo ndiyo Lugha Chanzi na pia vya Lugha Pokezi ya Kiswahili. Aidha, imemhitaji mtafiti kuwa na nakala za Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* na Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* kwa kuwa ndizo zilizohitaji kulinganishwa ili kuona jinsi mtafsiri alivyokiuka kanuni na sheria mbalimbali za uandishi alipokuwa akitafsiri TT kutoka TC.

Kazi nyinginezo za waandishi wa Matini Chanzi zimesomwa na kurejelewa ili kujua mtindo wao wa uandishi. Ngũgĩ wa Thiong’o kwa mfano, ana kazi (riwaya, tamthilia na hadithi) nyinginezo nyingi ambazo ziliweza kutuangazia zaidi kuhusu Tamthilia Chanzi tuliyoishughulikia ya *Ngaahika Ndeenda*. Tafsiri ya Kiingereza ya *I Will Marry When I Want* ya Ngũgĩ wa Thiong’o na Ngũgĩ wa Mĩriĩ iliyochapishwa mnamo 1982 ni mfano wa kazi ya waandishi husika iliyobidi mapitio. Isitoshe, vitabu vinavyoelezea historia za waandishi wa MC vimetusaidia kuwaelewa waandishi hawa, historia zao na uandishi wao. Aidha kalamu, karatasi na madaftari yametumika katika kuhifadhi data iliyopatikana.

Tarakilishi imetumika vilevile katika kukusanya habari kuhusu tafsiri na ukiushi katika tafsiri kutoka kwenye mtandao. Tarakilishi imetumika pia kurekodi na kuhifadhi data tuliyoishughulikia.

### 1.8.3 Uchanganuzi wa Data

Baada ya kuzisoma MC (*Ngaahika Ndeenda)* na MT (*Nitaolewa Nikipenda)* kwa mfululizo, tumenakili katika daftari mifano ya maneno, sentensi, vishazi, semi, aya na viakifishi vilivyokiukwa na mtafsiri. Mistari imepigwa kwa wino katika Matini Chanzi na katika Matini Tafsiri chini ya vipengele vyote vyenye ukiushi. Tumeitolea maelezo na ufafanuzi mifano yote iliyotolewa ili kuonyesha jinsi ukiushi ulivyojitokeza na namna ukiushi huo ulivyoathiri maana ya ujumbe wa Matini Tafsiri ikilinganishwa na Matini Chanzi.

Tumetanguliza kwa kuzisoma kwa makini Tamthilia Chanzi na Tamthilia Tafsiri kutoka ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho huku tukichunguza na kuangalia kila neno, sentensi, aya au kiakifishi. Data imepatikana pale tumepata kuwa mwandishi wa Tamthilia Tafsiri amekiuka kaida za sheria za uandishi kwa kukiuka maana halisi ya neno, sentensi, kishazi, aya au kiakifishi tofauti na ilivyowasilishwa katika Tamthilia Chanzi. Ukusanyaji wa data hiyo ya ukiushi wa aina yoyote uliotokea katika TT umefanywa kwa kuandika na kuonyesha jinsi ilivyoandikwa katika Matini Chanzi na chini yake jinsi ilivyotafsiriwa katika Matini Pokezi. Herufi MC imetumiwa kuwakilisha Matini Chanzi (Tamthilia Chanzi) na MT imetumiwa kuwakilisha Matini Tafsiri yaani Tamthilia Tafsiri. Aidha, tumeonyesha kila ukurasa mnamojitokeza kila mfano wa ukiushi katika Matini Tafsiri na vilevile kila ukurasa katika Matini Chanzi ambapo tafsiri imetolewa. Nambari za kurasa

hizi zimeandikwa mwisho wa kila mfano na kuwekewa mabano ili kufanya iwe rahisi kufanya urejelezi.

Tumelinganisha na kulinganua vipengele vyote vyenye ukiushi uliopatikana katika maneno, vishazi, sentensi na katika viakifishi. Tumechunguza vievile ukiushi ulivyojitokeza katika methali, nahau na katika nyimbo kwenye Tamthilia Tafsiri kwa kuwarejelea wataalamu na waandishi mbalimbali wa taaluma ya tafsiri. Tumeelezea kila mfano wa ukiushi uliojitokeza kwa kuwarejelea waandishi mbalimbali wa taaluma ya tafsiri. Tumegawanya mifano yote ya ukiushi ulioko katika TT katika kategoria mbalimbali mathalani ukiushi wa kifonolojia, wa kisemantiki, wa kisintaksia, ukiushi wa nyakati, na kadhalika. Kwa kuhitimisha, mtafiti alitathmini ufanisi wa mtafsiri katika lengo lake kuu ambalo ni kuwasilisha maana na ujumbe ulioko kwenye MC na kuuweka katika MT. Hili lilifanywa kwa kuthibitisha kama dhamira, maudhui, mbinu za kisanaa na msuko wa matukio unalandana kati ya Matini Chanzi na Matini Pokezi na iwapo pia maana na ujumbe katika tamthilia hizo mbili unalingana.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia misingi ya utafiti kwa kuelezea usuli wa utafiti. Katika usuli wa utafiti, tumechunguza na kujadili historia ya taaluma ya tafsiri. Tumefafanua suala la utafiti na vilevile kuelezea malengo ya utafiti pamoja na nadharia tete zilizouongoza utafiti huu. Pia tumeshughulikia upeo wa utafiti mbali na kuelezea umuhimu wa utafiti huu. Katika sura hii vilevile, tumeshughulikia msingi wa kinadharia kwa kujadili nadharia kuu inayotuongoza katika utafiti huu. Tumetalii na kuchunguza yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na hatimaye tukajadili mbinu zinazotumiwa katika utafiti huu. Isitoshe

tumeshughulikia vifaa vilivyotumiwa katika utafiti wetu na tukatamatisha kwa kufafanua jinsi uchanganuzi wa data unavyofanyika katika huu utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Kwa kuwa utafiti huu umeshughulikia ukiushi katika tafsiri, tumechunguza dhana ya ukiushi katika tafsiri na vilevile kuchambua sababu zilizopelekea ukiushi huo kujitokeza katika Matini Tafsiri. Baadhi ya mambo yanayopelekea ukiushi kujitokeza katika tafsiri ni; ubunifu na ubinafsi wa mtafsiri, umilisi wake wa Lugha Chanzi na Lugha Pokezi, tofauti za kitamaduni kati ya lugha husika, ujuzi na uzoefu wa mtafsiri katika taaluma inayoshughulikiwa, tofauti za kiisimu kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi na vile vile aina ya hadhira anayoilenga katika tafsiri.

## 2.1 Dhana ya Ukiushi katika Tafsiri

Ukiushi ni hali ya kukaidi au kutotii sheria za kaida za uandishi. Ukiushi unatokana na kitendo 'kiuka' chenye maana ya kupotoka, kukengeuka au kupechuka yaani kusema au kutafsiri katika Matini Tafsiri maana ambayo si kisawe cha ilivyo katika Matini Chanzi. Mwasisi wa dhana ya ukiushi katika tafsiri ni Huddleston (1976). Mtafsiri huwa amekiuka maana dhamiriwa anapoandika katika Matini Tafsiri neno, kishazi, sentensi au kiakifishi ambacho si kisawe cha ilivyo katika Matini Chanzi. Shitemi (1997) anadai kuwa ingawa ukiushi unaweza kutumiwa katika tafsiri kwa njia ya kuleta ubunifu, ukiushi unaweza kuleta upotoshi usipotumiwa kwa uangalifu. Anatoa mfano wa tungo nyingi za ushairi wa jadi wa Kiswahili zilizopotoshwa na ukiushi na udhaifu wa wasawidina katika kukumbuka kunakili tungo na matatizo katika kutafsiri tungo hizo kutoka hati za Kiarabu.

Akichangia kuhusu ukiushi katika tafsiri, Venuti (1992) anadai kwamba Matini Asilia hudumu milele tofauti na Matini Tafsiri ambayo haidumu milele. Anasema kuwa Matini Asilia huwasilisha tajriba, hisia na maelezo ya Mwandishi Asilia ilhali Matini Pokezi ni kimelea tu cha Matini Asilia ambayo huwasilisha mawazo ya Mwandishi Asilia. Kwa hivyo Matini Tafsiri si halisi na ndio maana haipewi hadhi sawa na Matini Chanzi bali hushushwa hadhi. Venuti anajadili kuwa Matini Tafsiri inaweza kuwa imesheheni ukiushi wa mtafsiri unaotokana na maoni yake, mihemko, hisia, maelezo na tajriba zake. Kwa hivyo, Matini Tafsiri si kiwakilishi halisi cha mawazo ya Mwandishi Asilia bali cha mawazo ya mtafsiri. Akimnukuu Rabassa, Venuti (1992) anaongeza kuwa tajriba ya mtafsiri inaweza kumfanya kupendelea kutumia maneno fulani badala ya maneno fulani mengine yenye maana sawa. Tulikubaliana na maoni ya mtaalamu huyu lakini tukazingatia hoja kuwa ukiushi katika tafsiri hauwezi kuepukika kwa ujumla na ni sharti ujitokeze katika muktadha ambapo hadhira za Lugha Chanzi na Lugha Pokezi zina tamaduni, mazingira miktadha na mifumo tofauti ya kiisimu.

Newmark (1988) anasema kuwa ukiushi katika matini za kifasihi hutokana na mambo mawili. Kwanza, ukiushi humwezesha mtafsiri kukiuka lugha ya kifasihi kwa kurejelea lugha ya kawaida. Lengo la mtafsiri katika ukiushi wa aina hii ni kuboresha mawasiliano kati yake na hadhira yake au kati ya Matini Pokezi na Hadhira Lengwa. Pili, ukiushi katika kazi za kifasihi humwezesha mtafsiri kutoa ufafanuzi katika kiwango cha urejelezi. Nia ya mtafsiri katika ukiushi wa namna hii ni kumwezesha kuwasiliana na hadhira yake kwa njia mwafaka na kuhakikisha kuwa maana ya ujumbe unaowakilishwa umeeleweka barabara. Anaongeza kuwa ukiushi hujitokeza pale ambapo Lugha Pokezi haina jazanda iliyotumiwa katika Lugha Chanzi.  Katika hali kama hiyo, mtafsiri ana uhuru wa kukiuka jazanda hiyo

kwa kutumia nyingine yenye maana sawa lakini inayofahamika katika Lugha Pokezi. Tulikubaliana na mawazo haya ya Newmark kwani ukiushi unaopatikana katika tamthilia tulizoshughulukia za *Ngaahika Ndeenda* (TC) na *Nitaolewa Nikipenda* (TT) ambazo ni matini za kifasihi zilionyesha ukweli huo. Ukiushi wa mtafsiri Kabugi uliazimia kufanya hadhira ya Matini Pokezi kuuelewa ujumbe wa tamthilia hiyo kwa njia mwafaka.

Wales (1991) anaufafanua ukiushi kama tofauti za kuirejesha habari kutoka kwa kaida. Anaongeza kuwa tofauti hizi zinategemea ukiukaji wa kanuni za kawaida za muundo wa kiisimu: kifonolojia, kisintaksia, kileksia au kisemantiki. Utafiti wangu umetofautiana na wa Wales kwani nimeuona ukiushi kama kiashiria cha ubunifu na waweza kutokea katika tanzu zingine kama vile tafsiri ya tamthilia tuliyoishughulikia ya *Nitaolewa Nikipenda*. Ukiushi katika tafsiri hutokana na mambo mbalimbali yakiwemo; ukosefu wa umilisi wa kutosha kwa upande wa mtafsiri, tofauti kati ya mila, desturi na utamaduni wa Hadhira Asilia na Hadhira Pokezi, ubunifu na ubinafsi wa mtafsiri, tofauti za kihistoria kati ya Matini Chanzi na Matini Tafsiri na ujuzi na udhibiti wa mtafsiri wa taaluma inayoshughulikiwa katika matini husika.

## 2.2 Ubunifu kama Kiashiria cha Ukiushi katika Tafsiri

Dhana ya ubunifu katika tafsiri inatokana na kitendo cha kubuni kinachomaanisha kuunda kitu kwa mara ya kwanza (Bakhresa 1990). Ubunifu basi ni ufinyanzi wa msanii unaomfanya kuunda wazo au hali kutokana na kuyatia mawazo yake fikirani. Tafsiri ni utendaji bunifu. Kwa mujibu wa Gui (1995) katika makala 'Asili ya Tafsiri ni Bunifu', tafsiri ni bunifu kwa sababu mtafsiri sharti ayaunde mawazo ya LC hadi yawe katika muundo wa LP. Isitoshe, Mchakato wa kuitafuta nakili ya Lugha Tafsiri na neno au kirai cha LC mara nyingi huwa bunifu. Nida (1996) anajadili kuwa tafsiri si sayansi wala

taaluma huru bali ni teknolojia bunifu ya kuhawilisha wazo lililoandikwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Snell-Hornby (1995) anaelezea kuwa kanuni za lugha humpa mtafsiri uwezo mkubwa wa kubuni, na hata wakati mwingine kuongeza kaida za kubuni. Ubunifu basi, kama mkakati katika zoezi la kutafsiri hautumiwi tu na mtafsiri wa makala au matini iliyo katika maandishi bali pia na mtafsiri wa ujumbe au habari ambayo haikuandikwa (mkalimani).

Akisisitiza umuhimu wa ubunifu wa mtafsiri katika mchakato mzima wa tafsiri, Lawson (1982) anasema kuwa haiwezekani kwa mitambo inayotumiwa kutafsiri kuweza kutoa tafsiri timilifu kama awezavyo kufanya mtafsiri mmilisi wa lugha (L1 na L2) kwani mitambo haiwezi kuwa na ubunifu. Tangia mwongo wa 1930, majaribio mengi yamefanywa ulimwenguni kuwezesha tafsiri kutumia mitambo (mashine). Hata hivyo hili halijawezekana kikamilifu kwa kuwa mitambo haina sifa ya ubunifu wala haiwezi kuelewa vyema muktadha wa matumizi wa neno fulani. Alijadili kuwa mtafsiri hana budi kuvunja kaida na sheria za Lugha Chanzi na kuongeza ubunifu wake aidha kisintaksia au kileksia.

Newmark (1988) anadai kuwa mtafsiri hulazimika kuwa mbunifu (creative) anapokabiliwa na ukosefu wa namna au jinsi ya kutafsiri dhana fulani katika lugha nyingine. Anafafanua hali au sababu saba zinazolazimu ubunifu wa mtafsiri katika mchakato wa tafsiri. Kwanza mtafsiri hutumia ubunifu ikiwa majina au maneno ya kitamaduni yametumika katika Matini Chanzi. Pili, mtafsiri hutumia ubunifu kupata kisawe chake katika Lugha Pokezi. Tatu, anaweza kutumia ubunifu iwapo majina au maneno ya kitamaduni yenye maana tofauti kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi yametumiwa katika Matini Chanzi. Nne, mtafsiri hutumia ubunifu kubainisha maana ya maneno kama hayo yenye utata.Tano, bunifu hauna budi kutumiwa na mtafsiri iwapo kuna matumizi ya istilahi ya Lugha Chanzi

ambayo haieleweki katika Lugha Pokezi. Inamlazimu mtafsiri kuwa mbunifu na kutafuta namna ya kuielezea istilahi hiyo hata kama ni kwa tafsili. Vinginevyo, ubunifu wa mtafsiri utaweza kuhitajika pale ambapo matumizi ya mfumo wa kisarufi katika Matini Chanzi haulingani na mfumo wa kisarufi wa Lugha Pokezi. Katika hali kama hiyo, mtafsiri hulazimika kutumia ubunifu wake kuifinyanga sarufi ya Lugha Pokezi ili kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa.

Sita, mtafsiri hana budi kutumia ubunifu wake mwenyewe iwapo kuna matumizi ya jazanda, semi, methali na nahau za Lugha Chanzi ambazo hazifanani na za Lugha Pokezi. Aidha matumizi ya neno lililobuniwa na mwandishi wa Matini Chanzi humkanganya mtafsiri na hivyo kumlazimisha kuwa mbunifu na kubuni na yeye pia neno lenye kuwasilisha maana ya neno hilo geni. Saba, mtafsiri kutumia ubunifu kama mkakati katika tafsiri ikiwa kuna matumizi ya neno la Lugha Chanzi lisilo na kisawe cha moja kwa moja katika Lugha Pokezi. Katika hali kama hiyo, mtafsiri hulazimika kubuni neno litakaloleta maana sawa na neno hilo la Lugha Chanzi.

Ubinafsi kama kiashiria cha ukiushi katika tafsiri hutokea pale ambapo dhamira ya mtafsiri katika kuitafsiri kazi husika, hutofautiana na dhamira ya Mwandishi Asilia. Katika hali kama hiyo, mtafsiri huipotosha maana iliyokusudiwa na Mwandishi Asilia ili kukidhi mahitaji na dhamira yake yeye binafsi. Katika kuipotosha maana inayodhamiriwa na Matini Chanzi, mtafsiri hujifaidi yeye mwenyewe kwa kutimiza malengo yake japo kwa kuihasiri Hadhira Pokezi ya matini yake. Mfano mmoja wa ukiushi unaotokana na ubinafsi wa mtafsiri ni katika tafsiri ya Mwalimu Nyerere ya *Mabepari wa Venisi* kutoka Matini Chanzi ya Shakespeare ya *The Merchant of Venice*. Katika mfano huu, Nyerere ametafsiri neno <u>Merchant</u> kwenye anwani kama <u>Mabepari</u> badala ya kutumia neno *Mfanya biashara*

ili kukidhi mahitaji na dhamira yake binafsi ya kuupiga vita mfumo wa kiuchumi wa kibepari nchini Tanzania. Mtafsiri huyu ametumia ukiushi huu ili kuupigia debe mfumo wa kiuchumi wa ujamaa humo nchini ambao aliupendelea.

## 2.3 Athari ya Umilisi wa Mtafsiri

Umilisi ni uwezo wa mtumiaji au mzungumzaji lugha wa kuielewa lugha husika kwa ufasaha wa kutosha. Sykes katika Picken (1983) anajadili kuwa uelewaji wa Lugha Chanzi ni zana muhimu kwa mtafsiri yeyote anayeazimia kuitafsiri matini ya lugha hiyo kwa lugha nyingine. Ili kuifanikisha tafsiri kutoka Lugha Chanzi hadi Lugha Pokezi, mtafsiri hana budi kuwa na umilisi wa kutosha wa Lugha Chanzi. Kama itawezekana, mtafsiri anafaa kuwa na umahiri wa Lugha Chanzi na Lugha Pokezi. Anafafanua mtaalamu huyu kuwa umilisi wa mtafsiri hujitokeza katika uwezo wake wa kuwa na utambuzi wa maana ya maneno yaliyoko kwenye Matini Chanzi na Utambuzi wa uteuzi wa maneno hayo na mtindo wa matumizi ya maneno hayo kama yalivyotumiwa na Mwandishi Asilia. Aidha umilisi wa mtafsiri hujitokeza katika utambuzi wake kuwa maneno kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi yanaweza kufanana lakini yasheheni maana tofauti. Vile vile, umilisi wa mtafsiri hujitokeza katika ujuzi wa miundo ya kisarufi ya Lugha Chanzi unaomwezesha kutambua miundo sahihi na miundo isiyo sahihi. Anajadili Picken pia kuwa uzoefu wa maisha (mazingira na utamaduni) ya jamii inayoitumia Lugha Chanzi yaani Hadhira Asilia hudhihirisha umilisi wa mtafsiri

Ukiushi hujitokeza katika tafsiri pale ambapo mtafsiri hupotosha maana ya ujumbe uliokuwa kwenye Matini Chanzi kwa kutokuwa na umilisi wa kutosha wa Lugha Chanzi. Ukiushi kama huu haujitokezi kwa makusudi bali hutokana na ukosefu wa umilisi wa mtafsiri. Umilisi wa kutosha wa Lugha Pokezi ni muhimu vilevile kwa mtafsiri. Ili

kufanikisha kazi ya tafsiri na kuepusha upotoshi, mtafsiri anastahili kuwa na ujuzi wa kutosha wa Lugha Pokezi. Mtafsiri anastahili kuwa na uwezo wa kuteua maneno ya Lugha Pokezi yanayoleta maana iliyoko kwenye Matini Chanzi, uwezo wa kutumia mpangilio sahihi wa maneno katika sentensi za Matini Tafsiri na vile vile uwezo wa kuakifisha Matini Tafsiri kwa usahihi kwa mujibu wa kanuni za Lugha Pokezi. Isitoshe, mtafsiri hana budi kuwa na uteuzi sahihi wa aina ya lugha itakayotumika katika aina mbalimbali za matini, uwezo wa kujieleza kwa ufasaha katika Lugha Pokezi na uwezo wa kujua matatizo yanayoweza kutokea katika uhawilishaji wa maana ya ujumbe katika Lugha Pokezi.

## 2.4 Utamaduni Kama Kiashiria cha Ukiushi

Utamaduni ni hali ya maisha ya jamii na huhusisha mambo mbalimbali ya jamii hiyo mathalani lugha, historia, mila na desturi, mavazi, itikadi za kidini, nyimbo, vyakula na kadhalika. Kama vile ambavyo mtafsiri anastahili kuwa na umilisi wa Lugha Chanzi na Lugha Pokezi, mtafsiri vilevile anatakiwa kujua utamaduni wa hadhira ya Lugha Chanzi na pia utamaduni wa Hadhira Pokezi anayoitafsiria. Hata hivyo, ni nadra kwa mujibu wa Robinson (1997) kwa mtafsiri kuwa na ufahamu kamilifu wa tamaduni za jamii-lugha zote mbili ambazo anazishughulikia katika tafsiri. Tofauti za kitamaduni kati ya Hadhira Asilia na Hadhira Pokezi husababisha ukiushi katika tafsiri. Katika Matini Chanzi tuliyoishughulikia ya *Ngaahika Ndeenda*, waandishi walitumia methali, nahau na nyimbo nyingi za kiasili za Lugha Chanzi ambazo zilileta ugumu katika kuzitafsiri katika Lugha Pokezi. Jambo hili lilisababisha ukiushi wa Matini Tafsiri kutoka kwa Matini Chanzi. Maneno mengine kwenye MC yalitumika katika muktadha na mazingira ya Hadhira Asilia na hivyo kumpa mtafsiri changamoto nyingi katika kuyahawilisha kwenye muktadha, utamaduni na mazingira ya Hadhira Pokezi. Umilisi wa Lugha Chanzi na Lugha Pokezi sio

ithibati ya ufahamu wa mtafsiri huyo wa tamaduni za lugha hizo mbili. Ukiushi usio wa kimakusudi hujitokeza katika tafsiri pale ambapo jamii-lugha mbili zina tamaduni tofauti ambazo mtafsiri hazielewi vya kutosha.

Tofauti za kitamaduni zinazoweza kuleta ukiushi katika tafsiri zinaweza kuweko hata katika jamii-lugha moja. Jamii-lugha moja inaweza kuwa na tamaduni zinazotofautiana na kuhitilafiana katika vipindi tofauti vya kihistoria. Utamaduni wa wanajamii-lugha katika karne moja unaweza kutofautina na utamaduni wa wanajamii-lugha iyo hiyo katika karne nyingine. Isitoshe, jamii-lugha moja inaweza kuwa na tamaduni tofauti zinazodhibitiwa na maeneo ya kijiografia. Utamaduni wa mwanajamii-lugha anayeishi mjini huenda ukatofautiana na wa yule anayeishi mashambani. Utamaduni huathiri ukiushi kwani mambo yanayokubalika katika utamaduni wa Hadhira Chanzi huenda yasikubalike katika utamaduni wa Hadhira Pokezi ambayo itayachukulia kuwa mwiko. Fauka ya hayo, baadhi ya maneno na matamshi ya Lugha Chanzi huenda yasikubalike katika utamaduni wa Lugha Pokezi na hivyo kumlazimu mtafsiri kuyakiuka. Vile vile, baadhi ya vitu au vifaa vilivyotajwa katika Matini Chanzi huenda havijulikani katika muktadha na mazingira ya Hadhira Pokezi na hivyo kumlazimisha mtafsiri kuvikiuka kwa faida ya hadhira yake. Kwa mfano viatu vya *Nginyĩra* katika uk 1 wa MC tuliyoishughulikia vilimtatiza mtafsiri kama tutakavyoona katika sura ya tatu.

### 2.5 Ujuzi na Uzoefu katika Taaluma Husika

Mbali na kuwa na umilisi wa lugha mbili zinazohusika katika tafsiri na ufahamu wa tamaduni husika, mtafsiri anastahili kuwa na ujuzi, uzoefu na tajriba ya kutosha katika taaluma anayoishughulikia katika tafsiri. Tajriba hupatikana kutokana na ujuzi na mazoezi ya kutosha. Ujuzi katika taaluma inayoshughulikiwa katika tafsiri utapunguza ukiushi wa

mtafsiri ambao ungeweza kutokea bila ya kutarajiwa. Kuna matini za aina nyingi mathalani matini za kifasihi, matini za kisayansi, za kisheria, za kidini, za kiuchumi ama kibiashara, za kiakademia kwa mfano za kihistoria na kadhalika. Ili kuepuka ukiushi ambao unaweza kutokea kiajali, mtafsiri anapaswa kuwa na ujuzi na uzoefu wa kutosha katika taaluma husika.

Ni muhimu kwa mtafsiri kuwa na ujuzi wa taaluma anayoishughulikia.Iwapo mtaalamu wa tafsiri atakabiliwa na matini inayohusu taaluma ambayo hana ujuzi au uzoefu wake, mtafsiri huyo anafaa kushirikiana na mtaalamu katika taaluma hiyo ili kufanikisha tafsiri hiyo (Picken 1983). Bila ushirikiano wa aina hiyo, mtafsiri ataishia kuandika tafsiri yenye ukiushi mwingi ambao utapotosha maana ya ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi wa Matini Chanzi, jambo ambalo litaathiri mawasiliano mwafaka kati ya MT na Hadhira Pokezi. Aidha athari ya ujumbe kati ya Hadhira Asilia na Hadhira Pokezi haitakuwa sawa kama alivyopendekeza Nida katika Nadharia ya Mlingano Endelevu, iwapo mtafsiri hatashirikiana na mtaalamu wa taaluma husika. Matini tuliyoishughulikia katika utafiti huu ni ya kifasihi. Mtafsiri wa tamthilia tuliyoishughulikia ni mjuzi na mzoefu wa taaluma ya fasihi kwa kuwa ni mwalimu wa lugha na fasihi. Ujuzi huu katika taaluma ya fasihi ulimwezesha kuepuka upotoshi au ukiushi ambao ungetokea bila yeye kutarajia.

## 2.6 Tofauti za Kiisimu baina ya Lugha Zinazohusika

Sababu nyingine ambayo husababisha ukiushi katika tafsiri ni tofauti za kiisimu kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi. Tofauti hizi za kiisimu zinaweza kusababisha ugumu katika kuihawilisha matini ya Lugha Chanzi kwenye Lugha Pokezi bila ya kukiuka sheria na kaida za Lugha Pokezi. Lugha Chanzi inaweza kuwa na miundo ya sentensi, nyakati na sheria za uakifishaji zisizolingana na za Lugha Pokezi, jambo ambalo litamfanya mtafsiri

kukiuka miundo, nyakati na viakifishi vilivyotumika kwenye Matini Chanzi kwa kudhibitiwa na kaida za Lugha Pokezi. Lugha ya Kifaransa kwa mfano haitofautishi kati ya wakati uliopo hali ya kuendelea na wakati uliopo hali ya mazoea. Jambo hili litamtatanisha mtafsiri wa matini ya Kifaransa kuelekea Kiswahili, jambo ambalo litasababisha ukiushi katika tafsiri. Aidha, uakifishaji wa tamthilia au dayalojia kati ya lugha hizi mbili ni tofauti. Kifaransa hutumia kistari kifupi kuonyesha maneno yaliyosemwa na mhusika fulani wakati ambapo Kiswahili hutumia koloni. Tofauti kama hizi kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi hupelekea kuweko kwa ukiushi katika tafsiri kwa kuwa mtafsiri hana budi kuzingatia kanuni za kiisimu za Lugha Pokezi anaposhughulikia kazi ya tafsiri.

## 2.7 Aina ya Hadhira anayoilenga Mtafsiri

Jambo lingine ambalo husababisha ukiushi katika tafsiri ni aina ya hadhira ambayo mtafsiri anaitafsiria au anailenga. Ikiwa kwa mfano mtafsiri anatafsiria hadhira ya watoto kazi ya kisanaa yenye uzito wa mawazo na yenye wingi wa methali na jazanda, mtafsiri huyo hatakuwa na budi kukiuka maana halisi ya methali na jazanda hizo. Hii ni kwa sababu hadhira hiyo ya umri mdogo haitaelewa mawazo mazito yanayobebwa na semi hizo za kifasihi. Oduori katika Shitemi na Ogechi (2008) anatoa mfano wa kutafsiria kazi za kifasihi za Ngũgĩ wa Thiong'o kwa hadhira kama hii ya watoto. Anasema mtaalamu huyu kuwa hadhira hiyo haiwezi kumudu kuielewa maana ya ujumbe katika kazi kama hizo zenye mawazo mazito mazito. Kwa sababu hii, mtafsiri hulazimika kutumia ukiushi wa kimakusudi ili kuirahisisha kazi hiyo ili hadhira kama hiyo ipate kuelewa. Tamthilia Chanzi tuliyoishughulikia ya *Ngaahika Ndeenda* imehusisha methali nyingi ambazo haziwezi kueleweka kwa hadhira yenye umri mdogo. Kwa hivyo, aina ya hadhira, umri na

kiwango cha ukomavu wa kimawazo wa hiyo hadhira huweza kumpelekea mtafsiri kukiuka baadhi ya maana ya maneno katika tafsiri.

## 2.8 Hitimisho

Tumebaini katika sura hii kuwa Nadharia ya Tafsiri ni jumla ya mapendekezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu mambo muhimu ya kuzingatiwa katika zoezi la tafsiri. Tumejadili sababu mbalimbali zinazopelekea ukiushi kujitokeza katika tafsiri. Aidha, tumeona kuwa ukiushi unaweza kuwa umejitokeza kama njia ya kuleta ubunifu. Hata hivyo, pakikosa uangalifu, ukiushi unaweza kupotosha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa Matini Chanzi.

# SURA YA TATU

# AINA ZA UKIUSHI KATIKA MATINI TAFSIRI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumetanguliza kwa kuelezea kwa kifupi kisa cha tamthilia Nitaolewa Nikipendaambayo ni tafsiri ya Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda.* Tumejadili muundo wa Matini Chanzi na Matini Tafsiri ili kuona iwapo mtafsiri alikiuka muundo wa Tamthilia Chanzi. Vilevile tumejadili ukiushi wa kifonolojia uliojitokeza katika Tamthilia Tafsiri. Tumechunguza na kujadili aina mbalimbali za ukiushi wa kisintaksia uliojitokeza katika Matini Tafsiri kwa mfano ukiushi katika mpangilio wa maneno katika sentensi, ukiushi wa alama za uakifishaji, ukiushi wa njeo na ubadilishaji wa kiungo cha neno katika sentensi. Tumetamatisha kwa kufafanua aina mbalimbali za ukiushi wa kisemantiki uliojitokeza katika Matini Tafsiri kwa mfano ukiushi katika maana za maneno, ukiushi katika maana za methali na ukiushi katika maana za nahau katika Matini Tafsiri.

## 3.1 Mukhtasari wa Tamthilia

Kĩgũũnda na mkewe Wangeci wako nyumbani kwao. Wanashangazwa na ahadi ya tajiri wao Kĩoi wa Kanoru kwamba atawatembelea Jumapili ijayo. Wanadhani kuwa nia ya tajiri Kĩoi ni kuwaomba kumuuzia kijishamba chao cha ekari moja unusu licha ya kuwa ana maelfu ya ekari. Siku ya ziara hiyo, Kĩoi, rafikiye Ndugĩre na wake zao wanawasili kwa Kĩgũũnda. Kumbe nia ya Kĩoi ni kuwashawishi Kĩgũũnda na mkewe ‘kuokoka’ na kufanya harusi ‘takatifu’ kanisani. Wanapoondoka wageni hao, Kĩgũũnda na mkewe wanajisaili kuhusu nia ya Kĩoi. Wangeci anadhani kuwa Kĩoi anataka wawe Wakristo ili mwanawe

Kĩoi (John) amwoe binti yao Gathoni. John Mũhũni na Gathoni wana uhusiano wa kimapenzi na John siku zote huja kumchukua Gathoni kwa gari.

Kĩgũũnda anamwomba Kĩoi msaada wa kifedha kwani hawezi kugharamia harusi yake na Wangeci. Kĩoi anamshauri Kĩgũũnda kutumia hati ya kumiliki kijishamba chake kama rehani ya kuchukulia mkopo kwenye benki kugharamia hiyo harusi. Kĩoi anakubali na kuanza matayarisho ya harusi. Gathoni anarejea nyumbani huku akilia. Anatoka ziarani pwani walikokwenda na mpenziwe John aliyetumwa na babake (Kĩoi) kumwangalilia shamba lake huko. Gathoni anafanya ziara hiyo licha ya kukatazwa na babake. Analia sasa kwa kuwa John ameamua kumwacha baada ya Gathoni kumfichulia kuwa ameshika mimba yake.

Kĩgũũnda na mkewe wanafululiza hadi kwa Kĩoi wakidai harusi yao iahirishwe ili John na Gathoni wafanye harusi kwanza. Kĩoi anawafukuzilia mbali akisema kuwa mwanawe hawezi kumwoa kahaba (Gathoni). Kĩgũũnda anajaribu kutumia nguvu kumshurutisha Kĩoi kutia sahihi karatasi ya kutoa ahadi kuwa Gathoni ataolewa na John. Kĩgũũnda anashindwa kulazimisha jambo hili, anafutwa kazi na hivyo kushindwa kulipa mkopo wa benki. Kishamba chake kinatwaliwa na kuuzwa mnadani. Kĩoi ndiye anayekinunua. Kĩgũũnda anaishia kupoteza kibarua, shamba lake na bintiye kwa kupania desturi na utamaduni wa kigeni kwa kutaka kufanya arusi kanisani na kutupilia mbali mila na desturi zake za Kiafrika. Anaishia kuwa mlevi sugu katika kituo cha biashara ambapo bintiye Gathoni pia huuza pombe haramu.

### 3.2 Muundo wa Matini Chanzi na Matini Tafsiri

Istilahi umuundo hutumiwa kumrejelea mwasisi wa isimu ya kisasa, Saussure japo elementi za wananadharia wa awali kama vile Humboldt na Leibniz zipo katika nadharia ya umuundo. Saussure alijadili kuwa kila lugha ina muundo wake maalum na kwamba vipengele vyake, iwe sauti, maneno au maana hutokana na uhusiano wa vipengele hivyo na vipengele vinginevyo vya lugha hiyo. Cotterell & Turner (1989) wanasema kuwa umuundo ni mwingiliano wa kinachosemwa na kinachomaanishwa au kinachorejelewa. Uhusiano huu ndio huunda msingi wa umuundo katika lugha. Maana ya neno au maneno katika lugha si sharti ibaki sawa wakati wote kwani hutegemea uamilifu wake na uhusiano wake na vipengele vinginevyo katika lugha hiyo (Taylor 1995). Mtafsiri amezingatia muundo wa Matini Chanzi kwa kugawanya mchezo huu wa kuigiza katika vitendo vitatu. Kitendo cha kwanza kina sehemu moja pekee. Kitendo cha pili kina sehemu mbili nacho kitendo cha tatu kina sehemu tatu. Mtafsiri Kabugi hajakiuka utaratibu na muundo huu katika Matini Tafsiri licha ya kuwa kurasa za vitendo na sehemu hizi zinahitilafiana kati ya Matini Chanzi na Matini Tafsiri. Tofauti na waandishi wa Matini Chanzi wanaoonyesha kitendo na sehemu ya mchezo katika sehemu ya juu, kulia katika kila ukurasa wa pili, mtafsiri hajazingatia jambo hilo kwani anaonyesha kitendo na sehemu mpya sio juu ya kila ukurasa wa pili bali pale kitendo au sehemu hiyo inapoanzia.

Waandishi wa Tamthilia Chanzi wametumia muundo wa kishairi katika tamthilia Ngaahika Ndeenda. Aya nyingi za tamthilia hii ni fupi na zina silabi chache. Muundo huu wa kishairi unayapa uzito wa kimawazo matamshi na kauli za wahusika wanayoyatamka maneno yenyewe. Hii ni tofauti na ilivyo katika muundo wa kinathari wa tamthilia ambao kwa kawaida hauonyeshi uzito wa mawazo katika matamshi ya wahusika. Mtafsiri Kabugi

hajakiuka muundo huu wa Matini Chanzi kwa kuwa ameipa Tamthilia Tafsiri muundo wa kishairi vilevile. Ni katika sehehu za maelezo ya tamthilia pekee ambapo lugha ya nathari imetumika katika tamthilia zote mbili; TC na TT.

### 3.3 Ukiushi wa Kifonolojia

Fonolojia ni taaluma ya kiisimu inayojishughulisha na mfumo wa sauti za lugha (TUKI 2000). Kila lugha huwa na mfumo wake wa kipekee wa sauti. Ukiushi wa kifonolojia ni aina ya ukiushi ambao humfanya mtafsiri kuenda kinyume na fonolojia ya Lugha Chanzi kwa kutumia fonolojia ya Lugha Pokezi. Aina hii ya ukiushi ilmejitokeza katika Matini Tafsiri katika majina ya wahusika. Mtafsiri wa MT amewapa wahusika majina yaleyale waliyopewa na mwandishi wa MC. Mengi ya majina haya yamekiuka fonolojia ya Lugha Pokezi ya Kiswahili kwa kuwa yamehusisha matumizi ya irabu ĩ na ũ ambazo hazipo katika fonolojia ya lugha ya Kiswahili kwa mfano katika jina la mhusika Kĩgũũnda na Gĩcaamba. Fonolojia ya Kiswahili inatofautiana na ya lugha ya Gĩkũyũ kwa namna mbalimbali. Kwa upande wa sauti za vokali (irabu), Kiswa hili kina irabu tano; a, e, i, o, u. ilhali lugha ya Gĩkũyũ ina irabu saba nazo ni a, e, i, ĩ, o, u, ũ. Waandishi wa Tathilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* wamezingatia kwa kikamilifu fonolojia ya lugha ya Gĩkũyũ kwa kuzingatia sauti za lugha hiyo. Hata hivyo mtafsiri wa tamthilia hiyo kwa Kiswahili amekiuka fonolojia ya Lugha Pokezi ya Kiswahili kwa kuingiza katika Matini Tafsiri sauti za lugha chanzi ya Gĩkũyũ katika Matini Tafsiri ambayo ni ya Kiswahili. Mfano ni matumizi ya irabu i na u katika Matini Tafsiri. Huu ni ukiushi wa kifonolojia kwa kuwa irabu na sauti za irabu hizi hazitumiki katika lugha pokezi ya Kiswahili.

Fonolojia ya lugha chanzi ya Gĩkũyũ ina sauti zifuatazo za konsonanti:/b/, /g/, /h/, /k/, /m/, /n/, /r/, /t/, /w/, /y/, /mb/, /nd/, /ng/, /ng'/, /c/, /ny/ na /th/. Lugha pokezi ya Kiswahili ina

sauti za konsonanti /b/ /ch/, /d/, /dh/, /f/, /g/, /gh/, /h/, /j/, /k/, /kh/, /l/, /m/, /n/, /p/, /r/, /s/, /sh/ /t/, /v/, /w/, /y/ na /z/, , Aidha Kiswahili hakina sauti /c/ katika mfumo wa fonolojia yake kama ilivyo katika Gĩkũyũ. Ni dhahiri kuwa mtafsiri hajawapa wahusika majina mapya katika Tamthilia Tafsiri ila amedumisha majina hayo kama yalivyo katika Matini Chanzi. Jedwali 1 linaonyesha majina ya wahusika katika tamthilia hiyo.

**Jedwali 1**

| Jina la mhusika / Uhusika | Nafasi yake katika tamthilia |
|---|---|
| Aahabu Kĩoi wa Kanoru | : Kabaila mkubwa mwenye mashamba na biashara. |
| Ni Mkristo na ameokoka. | |
| Jespheli Kĩoi | : Mkewe Kĩoi na ameokoka vilevile. |
| Ikuua wa Nditika ila | : Rafiki yao. Wameshirikiana katika biashara nyingi |
| hajaokoka | |
| Samwel Ndugĩre Ameokoka. | : Tajiri aliyeongokewa na mambo, rafikiye Kĩoi. |
| Helina Ndugĩre | : Mkewe Samwel. Ameokoka vilevile. |
| Kĩgũũnda Mũrĩma | : Mfanya kazi katika shamba la Kĩoi |
| Wangeci Kĩgũũnda | : Mkewe Kĩgũũnda. Ni falahi (mkulima mdogo). |
| Gathoni Kĩgũũnda | : Bintiye Kĩgũũnda. |
| Gĩcaamba Kĩhooto | : Mfanya kazi katika kiwanda cha viatu. |
| Njooki Gĩcaamba | : Mkewe Gĩcaamba. Ni mkulima mdogo. |
| Cekiurĩko | : Mlinzi nyumbani kwa Kĩoi |
| Kiongozi wa waimbaji | : Wa dini ya Wamathĩĩna (wenye dhiki). |
| Boi | : Mpishi nyumbani kwa Kĩoi. |
| Kikundi cha waimbaji wa nyimbo za dansi. | |

Majina ya wahusika watatu pekee ndiyo yameathiriwa na tofauti za kifonolojia kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi nayo yametafsiriwa ifuatavyo kutoka MC kuelekea MT;

| **MC** | **MT** |
|---|---|
| 1 Njethibeeri wa Kĩoi | Jespheli Kĩoi |
| 2. Herina Ndugĩre | Helina Ndugĩre |
| 3. Mbooi | Boi |

Wahusika wengi katika Matini Chanzi wamepewa majina ya kimajazi. Mtafsiri Kabugi hajayatafsiri majina ya wahusika. Hata hivyo, badala ya kuyahamisha majina haya moja kwa moja kama yalivyo, mtafsiri ametafsiri majina ya wahusika wawili ambao ni Cekiurĩko (Mlinzi) na Mũrĩĩu (Mlevi). Sababu ya mtafsiri kuamua kutafsiri majina ya wahusika hawa wawili ni kuwa mwanzo, majina Cekiurĩko na Mũrĩĩu si majina halisi ya wahusika wenyewe bali ni majina ya majazi yanayoashiria hulka na tabia za wahusika wenyewe. Mhusika Cekiurĩko ni bawabu au mlinzi wa nyumbani kwa bwanyenye Kĩoi ilhali Mũrĩĩu ni mhusika mwenye tabia ya kulewa ovyo. Mtafsiri ametambua bayana kuwa asipokiuka kaida na kuyatafsiri majina ya wahusika hawa wawili, Hadhira Pokezi ya lugha ya Kiswahili itatatanika na kukosa kuelewa hasa hulka zinazowakilishwa na majina ya wahusika hawa.

Newmark (1988) anajadili kuwa kwa kawaida, majina ya watu hasa majina ya pili (ya kiasili) hayapaswi kutafsiriwa ila tu iwapo jina hilo linakusudiwa kuwasilisha sifa fulani ya mhusika anayerejelewa na jina hilo. Jina la kwanza la mhusika linaweza kutafsiriwa na ndipo mtafsiri Kabugi alilitafsiri jina la mhusika Njeethibeeri kuwa Jespheli na Herina

kuwa Helina katika MC na MT mtawalia. Ni muhali kuelezea hapa kuwa wahusika wote katika tamthilia hii wamepewa majina ya kimajazi. Tunadai hivi kwa sababu majina waliyopewa wahusika wote yanalingana na sifa na tabia zao. Mtafsiri amezingatia jambo hilo kwani amewapa wahusika majina yale yale waliyopewa katika Matini Chanzi; majina yanayoafiki hulka na sifa za wahusika hao.

### 3.4 Ukiushi wa Kisintaksia

Sintaksia ni taaluma ya kiisimu inayojishughulisha na mpangilio wa maneno katika virai na mpangilio wa virai katika sentensi. Anafafanua Mathews (1997) kuwa sintaksia ni uhusiano wa kisarufi kati ya maneno na vipengele au viungo vinginevyo katika hiyo sentensi. Ukiushi wa kisintaksia katika tafsiri hujitokeza wakati ambapo kuna upotoshi wa mtafsiri unaomfanya kutozingatia sintaksia ya Matini Chanzi na badala yake kubadilisha na kutumia sintaksia tofauti katika Matini Tafsiri. Katika aina hii ya ukiushi, mtafsiri hukiuka sintaksia ya Matini Chanzi na kuandika tafsiri ambayo inahitilafiana na sarufi ya Matini Chanzi. Ukiushi wa kisintaksia hujitokeza katika tafsiri endapo mpangilio wa maneno katika Matini Tafsiri ni tofauti na ulivyo katika Matini Chanzi au wakati (njeo) unaotumika katika vitenzi unatofautiana kati ya Matini Chanzi na Matini Tafsiri.

Aidha, ukiushi wa kisintaksia utakuwa umetumika pale ambapo uakifishaji katika Matini Tafsiri unahitilafiana na uakifishaji huo ulivyo katika Matini Chanzi au iwapo pana tofauti ya umoja na wingi kati ya MC na MT. Isitoshe, ubadilishaji wa kiungo cha neno lililotumiwa katika Matini Chanzi kwa mfano kuweka nomino badala ya kielezi hupelekea kutokea kwa ukiushi wa kisintaksia katika tafsiri. Ukiushi wa kisintaksia hujitokeza pia mtafsiri anaporekebisha tahajia katika MC kwa kuiandika kwa usahihi katika MT. Hata

hivyo, tumeonelea kuwa ni makosa kuchukulia kuwa ulinganifu wa moja kwa moja upo katika faridi zote za msamiati au miundo ya sentensi baina ya lugha zozote mbili.

Ukiushi wa kisintaksia hujitokeza pale ambapo mtafsiri hukosa kuzingatia mpangilio wa maneno wa Matini Chanzi na badala yake kubadilisha mpangilio huo katika Matini Tafsiri. Katika kitendo cha kwanza, ukiushi wa kisintaksia wa kukiuka mpangilio wa maneno katika sentensi umejitokeza katika maelezo ya sentensi ya kwanza kabisa ya tamthilia hii kama ifuatavyo:

**Mfano 1**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) *Gwa Kĩgũũnda Mũciĩ.* (uk 11)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) *Nyumbani kwa Kĩgũũnda.* (uk 11)

Katika Matini Chanzi, mpangilio wa sentensi una kihusishi, nomino halafu kielezi ilhali katika Matini Tafsiri sentensi imefuata mpangilio wa kielezi, kihusishi na kuishia na nomino. Ukiushi wa kisintaksia wakati mwingine hauepukiki katika tafsiri kwa kuwa lugha tofauti hufuata au huwa na muundo au mpangilio tofauti wa maneno katika sentensi. Lugha zingine huwa na mfumo huru (legevu) mathalani Kifaransa ilhali lugha zingine mathalani Kiingereza huwa na mfumo imara usiobabilishwa. Ninakubaliana na uamuzi wa mtafsiri Kabugi kuanza kisa hiki kwa *'Nyumbani kwa Kĩgũũnda.'* badala ya *'Kwa Kĩgũũnda nyumbani'* kwa kuwa ndiyo sarufi sahihi ya Lugha Pokezi (Kiswahili). Mfumo wa sentensi kati ya Lugha Chanzi (Gĩkũyũ) na Lugha Pokezi (Kiswahili) ni tofauti.

Ukiukaji wa mpangilio wa maneno katika Matini Chanzi na badala yake kuyawasilisha vinginevyo katika Matini Tafsiri umejitokeza katika mfano ufuatao:

**Mfano 2**

MC (*Ngaahika Ndeenda)* Kĩgũũnda: ….*.nĩ ũhoro urĩa.* (uk 88)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: ….kwa sababu ya ile habari (uk 82)

Katika mfano huu, nomino *'ũhoro'* imetanguliza kivumishi kirejeshi *'ũrĩa'* katika MC lakini katika MT, kivumishi kirejeshi 'ile' kimetangulia nomino 'habari'. Mtafsiri Kabugi alikiuka sarufi ya MC kutokana na tofauti za kisarufi na kiisimu kati ya Lugha Chanzi ya Gĩkũyũ na Lugha Pokezi ya Kiswahili. Hata hivyo, ninaafikiana na uamuzi na uteuzi huu wa mtafsiri kwa kuwa kuandika vinginevyo ni sawa na kuikaidi sarufi ya Lugha Pokezi ya Kiswahili ambayo inahitaji kivumishi kirejeshi au kivumishi kionyeshi kitangulie nomino katika sentensi.

### 3.4.1 Ukiushi wa Alama za Uakifishaji

Ukiushi wa kisintaksia katika alama za uakifishaji hujitokeza pale ambapo mtafsiri hutumia katika Matini Tafsiri alama za uakifishaji zinazotofautiana na zile zilizotumiwa na Mwandishi Asilia katika Matini Chanzi. Alama za uakifishaji tulizoshughulikia na ambazo zimekiukwa na mtafsiri ni kikomo, herufi kubwa, alama ya hisi na alama ya kuulizia. Katika matamshi ya kwanza kabisa ya mhusika Wangeci mchezo unapoanza, mtafsiri ameakifisha visivyo kauli ya mhusika huyu tofauti na ilivyo katika Matini Chanzi. Ukiushi huu wa alama ya uakifishaji umejitokeza ifuatavyo:

**Mfano 3**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Wangeci:*……….Nĩ kĩ gĩtũmaga ũmĩrore ũguo*

*Ta ĩrĩ ya ĩka ngiri igana?* (uk 11)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Wangeci: ……Kwa nini unaitazamatazama kwa

furaha nyingi namna hiyo.

Kama kwamba ni ya ekari elfu moja? (uk 11)

Katika mfano huu, waandishi wa MC hawajaweka alama yoyote ya uakifishaji baada ya neno *ũguo*, yaani mwishoni mwa msitari wa kwanza. Hata hivyo, mtafsiri amekiuka jambo hili na badala yake akaweka alama ya kikomo mwishoni mwa msitari huo yaani baada ya neno hilo. Ukiushi huu wa mtafsiri umeleta madhara kwenye tafsiri kwa kuwa ulimesababisha kubuniwa kwa sentensi isiyo sahihi au yenye dosari kwa kuwa haiwezekani kuwa na sentensi kama ‘Kama kwamba ni ya ekari elfu moja’. Mfululizo huu wa maneno unaweza kudhaniwa kuwa sentensi sahihi na kamilifu kimaana na kimantiki, jambo ambalolinaweza kuleta utata. Ni katika mfano uu huu wa ukiushi ambapo mtafsiri amepotosha kabisa maana ya maneno ya Matini Chanzi kwa kuandika kuwa hiyo hati ya kumiliki shamba ni ya *ekari elfu moja*. Ukweli ni kwamba katika Matini Chanzi imeandikwa *ĩĩka ngiri igana* ambayo tafsiri yake katika Kiswahili ni *ekari elfu mia moja* au *ekari laki moja.* Ukiushi wote huu wa mtafsiri umepotosha maana ya ujumbe ulioko kwenye Matini Chanzi kwa kuipotosha sarufi ya Lugha Pokezi na vilevile kuandika maneno ambayo si kisawe cha maneno ya Matini Chanzi.

Ukiushi huu wa mtafsiri wa kuakifisha Matini Tafsiri tofauti na Matini Chanzi umesababisha kuibuka kwa sentensi zisizo sahihi ambazo zimeathiri maana ya ujumbe uliokusudiwa na Waandishi Asilia. Sentensi zisizo sahihi zilizojitokeza katika MT kutokana na ukiushi huo ni ‘Kwa nini unitazamatazama kwa furaha nyingi namna hiyo’ na ‘Kama kwamba ni ya ekari elfu moja?’ Sentensi ya kwanza si sahihi kwani haina alama ya kuulizia ilhali sentensi ya pili si kamilifu wala haina mantiki. Kwa sababu hiyo, ukiushi huu katika uakifishaji umeleta athari hasi katika Matini Tafsiri.

Mfano mwingine wa ukiushi wa alama za uakifishaji umejitokeza ifuatavyo:

**Mfano 4**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Kĩgũũnda: Ndini cionganio kũrĩa cionganio,

Igaitwo gũũkũ gwitũ? (uk 17)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Dini zikiokotwa po pote

Huletwa hapa kwetu. (uk 16)

Katika mfano huu, ukiushi wa alama za uakifishaji umejitokeza mara mbili. Alama ya kituo/koma imekiukwa katika msitari wa kwanza katika Matini Tafsiri kwa kuwa mtafsiri hajaiweka alama hiyo kama ilivyowekwa katika Matini Chanzi. Pili, mtafsiri ameamua kuweka alama ya kikomo mwishoni mwa msitari wa pili kinyume na na ilivyo katika Matini Chanzi ambapo Waandishi Asilia wameweka alama ya kuulizia mwishoni mwa msitari huo. Kuweka alama ya kikomo katika Matini Tafsiri kuwakilisha alama ya kuulizia iliyoko katika Matini Chanzi ni ukiushi. Ukiushi huu unaleta maana tofauti kabisa katika ujumbe unaodhamiriwa na Wandishi Asilia. Jambo hili linaleta athari tofauti kwa hadhira za MC na MT. Athari inayoletwa na matumizi ya alama ya kuulizia katika MC ni kubwa kuliko ya matumizi ya kikomo katika Matini Tafsiri kwa kuwa alama ya kuulizia iliyotumiwa katika Matini Chanzi inamtashtiti msikilizaji na kuibua hisia zinazochochea kutafakari kwa kina zaidi. Ukiushi huu wa alama za uakifishaji umeathiri maana ya ujumbe uliokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi.

Ukiushi mwingine katika alama za uakifishaji umejitokeza katika mfano ufuatao:

**Mfano 5**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) : …………… “Christ is the head………” (uk 112)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) “ KRISTO NDIYE MKUU…..” (uk 104)

Mtafsiri amekiuka Matini Chanzi kwa kutumia herufi kubwa katika Matini Tafsiri kuwasilisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo katika Matini Chanzi. Mtafsiri angedhihirisha uaminifu kwa Matini Chanzi kwa kuakifisha maneno hayo kwa herufi ndogo kama ilivyowasilishwa katika Matini Chanzi. Kupitia ukiushi huu wa kutumia herufi kubwa badala ya herufi ndogo, mtafsiri ameweka msisitizo kwenye maneno husika na hivyo kuleta athari kubwa zaidi kwenye maneno husika kuliko ilivyo katika Matini Chanzi.

### 3.4.2 Ukiushi wa Matumizi ya Njeo katika Tafsiri

Njeo ni kategoria ya kisarufi ambayo huwakilisha muda au wakati ambapo tendo hufanyika (TUKI). Bakhressa (1992) anajadili kuwa njeo ni nafasi au muda wa kufanya jambo. Njeo au wakati ni mgawanyiko makusudi wa muda ambao kusudi lake kuu ni kuonyesha wakati kitendo kinapotendeka. Hugawanywa katika nyakati tatu kuu ambazo ni wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao (Mathews 1997). Ukiushi wa matumizi ya njeo hujitokeza pale ambapo mtafsiri hutumia nyakati (njeo) tofauti na nyakati zilizotumiwa na mwandishi wa Matini Chanzi katika sentensi. Mwandishi wa tafsiri anafaa kuzingatia na kutumia nyakati sawa na zilizotumiwa na mwandishi asilia. Katika Matini Tafsiri tuliyoishughulikia katika utafiti wetu, tumetambua mifano ifuatayo ya ukiushi wa matumizi ya nyakati:

**Mfano 6**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Mũkũi: <u>*Nĩ aagiria*</u> *twake kanitha*.......... (uk 16)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kiongozi: <u>Hutuzuia</u> kujenga kanisa............... (uk 16)

Katika mfano huu wa ukiushi wa nyakati, waandishi wa MC wametumia wakati uliopo hali timilifu wakiwa na maana ya ‘ametuzuia’. Mtafsiri Kabugi amekiuka wakati huo na badala yake kutumia wakati uliopo hali ya mazoea kwa kutumia neno 'hutuzuia'. Huu ni ukiushi dhahiri wenye nia ya kutilia nguvu kauli ya mzungumzaji (Kiongozi) kwa kuonyesha kuwa kitendo husika (cha kuzuia ujenzi wa kanisa) hurudiwa na kutokea si mara moja bali mara nyingi. Kwa kutumia ukiushi huu wa njeo na hali, mtafsiri ameweka msisitizo ambao umeufanya ujumbe wa matini yake kubainika zaidi kwa Hadhira Pokezi na hivyo kuboresha mawasiliano kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi.

Ukiushi mwingine wa nyakati umejitokeza ifuatavyo:

**Mfano 7**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Kĩgũũnda: *Ngwendaga kũmenya kana no ũtuonere mbeeca.* (uk 91)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Ningetaka kujua kama unaweza kutukopesha pesa. (uk 84)

Katika mfano huu, waandishi wa Matini Chanzi wametumia wakati uliopita kwa maana ya 'Nilitaka kujua'. Mtafsiri amekiuka nyakati kwa kuwa katika tafsiri yake, ametumia wakati uliopo hali ya masharti kwa kutumia neno 'ningetaka'. Tunaonelea kuwa mtafsiri amekiuka maana kwa kusudi la kuwasilisha ujumbe wa waandishi wa Matini Chanzi kwa utendeti zaidi ili kufanikisha mawasiliano mwafaka zaidi kati ya matini yake na Hadhira Pokezi. Kwa kutumia wakati uliopo hali ya masharti katika Matini Tafsiri badala ya wakati uliopita kama ilivyo katika Matini Chanzi, mtafsiri ameiweka bayana kauli ya mhusika mkuu Kĩgũũnda kuwa hakuwa amekata tamaa ya kupata msaada wa kifedha aliouhitaji sana

kutoka kwa mwajiri wake (Kĩoi). Kutokana na ukiushi huu wa njeo na hali, mtafsiri amefaulu kuufanya ujumbe dhamiriwa kueleweka kwa njia mwafaka zaidi kwa kuboresha mawasiliano kati ya mtafsiri, matini yake na hadhira ya Matini Pokezi.Mfano mwingine wa ukiushi wa kisarufi unaohusisha ukiukaji wa njeo inayotumika katika Matini Chanzi ni huu uliopo katika ukurasa wa kwanza wa mchezo huu wa kuigiza:

**Mfano 8**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Wangeci : *Taitondii ĩyo ũmĩũragia ndũũ?*
*Nĩ kĩĩ gĩtũmaga ũmĩrore ũguo*....... (uk 11)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Wangeci: Mbona unaifurahia hiyo hati ya kumiliki ardhi? Kwa nini unaitazamatazama kwa furaha nyingi namna hiyo. (uk 11)

Katika mfano huu, waandishi wa Matini Chanzi wametumia wakati uliopo hali ya mazoea kwa kuonyesha kuwa anayezungumziwa (Kĩgũũnda) huwa na tabia ya kuitazamatazama hiyo hati ya kumiliki ardhi. Tendo hili la kuitazama hati hiyo ya kumiliki ardhi hutendeka mara nyingi yaani hurudiwarudiwa. Ni tendo ambalo hufanyika mara kwa mara kwa mujibu wa Matini Chanzi. Mtafsiri wa hii tamthilia kwa Kiswahili amekiuka maana dhamiriwa kwa kubadilisha njeo katika Matini Tafsiri. Hii ni kwa sababu mtafsiri ametumia nyakati tofauti katika matini yake. Anapotumia maneno 'unaifurahia' na 'unaitazamatazama' mtafsiri ametumia wakati uliopo wakati usiodhihirika.

Kitendo anachokizungumzia mtafsiri kinatendeka wakati uliopo tu. Aidha hajaibua dhana kuwa kitendo kinachozungumziwa cha kuitazama hiyo hati ya kumiliki ardhi hutendeka mara kwa mara na hurudiwarudiwa mara nyingi. Hili ni dhihirisho bayana kuwa ukiushi wa kisintaksia upo katika Matini Tafsiri. Kupitia ukiushi huu katika njeo, mtafsiri

amepotosha maana iliyokusudiwa na waandishi wa Tamthilia Chanzi kwa kukosa kutilia mkazo kuwa Kĩgũũnda alikuwa na tabia ya kuitazamatazama hiyo hati ya kumiliki ardhi. Kutokana na ukiushi huu, athari ya maana ya ujumbe kati ya hadhira ya Matini Chanzi na hadhira ya Matini Tafsiri ni tofauti na hii inamaanisha kuwa hapakuwa na mawasiliano mwafaka kati ya Matini Chanzi na hadhira ya Matini Tafsiri.

### 3.4.3 Ubadilishaji wa Kiungo cha Neno

Kiungo cha neno ni istilahi inayotumiwa kurejelea aina ya neno kwa kuzingatia aina nane za maneno mathalani nomino, vitenzi na vielezi. Ubadilishaji wa kiungo cha neno ni aina ya ukiushi wa kisarufi ambapo mtafsiri hutumia kiungo cha neno ambacho ni tofauti na kile kilichotumiwa katika Matini Chanzi. Kwa mfano mwandishi wa MC anaweza kuwa ametumia kitenzi katika sentesi fulani. Tungetarajia mtafsiri kufuata mkondo huo kwa kutumia kitenzi vilevile. Hata hivyo mtafsiri anaweza kukiuka sarufi kwa kutumia badala yake nomino mahali pa au kuwakilisha kitenzi. Kuna viungo vinane katika lugha zote ulimwenguni; nomino, vitenzi vivumishi, vielezi, viwakilishi, vihusishi, viunganishi na vihisishi. Mtafsiri anapobadilisha kiungo kimoja kwa kiungo kingine katika tafsiri, huwa amehusisha aina hii ya ukiushi. Ukiushi wa kisarufi wa aina hii umejitokeza ifuatavyo katika matini tulizoshughulikia:

**Mfano 9**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Kĩgũũnda:*.....Kwaria nĩ kwendana*,…… (uk 48)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda:..Mazungumzo ni mapenzi,…… (uk 44)

Katika mfano huu, waandishi wa Matini Chanzi wametumia vitenzi viwili; *kwaria* na *kwendana vyenye* maana ya kuzungumza na kupendana. Badala ya kutumia vitenzi Kama walivyofanya waandishi wa MC, mtafsiri amekiuka kanuni hiyo na badala yake kutumia nomino mbili 'Mazungumzo' na 'mapenzi' kuwakilisha hivyo vitenzi. Ninaonelea kuwa ukiushi huu hujaathiri maana ya ujumbe uliokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi kwa kuwa maana iliyodhamiriwa bado inaeleweka barabara.

Mfano mwingine wa ukiukaji wa kiungo cha neno lililotumika katika Matini Chanzi ulijitokeza ifuatavyo:

**Mfano 10**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Mũtoongoria : *Caitani wa nduma-inĩ*

*Nĩ araangwo!* (uk 16)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kiongozi : Shetani wa giza

Na akanyagwe! (uk 16 )

Katika mfano huu, tunaona kuwa waandishi wa Matini Chanzi wametumia kielezi kwa neno *Nduma-inĩ* lenye maana ya gizani kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo mtafsiri wa tamthilia hiyo kuelekea Kiswahili amekiuka kisarufi kwa kubadilisha kiungo cha neno kilichotumiwa katika Matini Chanzi. Tunadai hivi kwa kuwa tafsiri anayoitoa mtafsiri ya neno Giza si kielezi bali ni nomino. Mtafsiri amekiuka sarufi kwa kuwakilisha kielezi kwa nomino katika tafsiri yake ya *Nitaolewa Nikipenda*. Hata hivyo, tunaonelea kuwa ukiushi huu wa mtafsiri haujaathiri vibaya maana ya ujumbe halisi uliodhamiriwa na waandishi asilia. Hii ni kwa kuwa maana ya ujumbe uliokusudiwa ingali inaeleweka vyema licha ya ukiushi huo kuwepo.

### 3.4.4 Ubadilishaji wa Umoja kwa Wingi

Hii ni aina ya ukiushi wa kisarufi ambapo mtafsiri hukiuka kaida ya umoja na wingi kwenye tafsiri kwa kutafsiri nomino iliyo katika umoja katika MC kwa nomino ya wingi katika MT. Vinginevyo, anaweza kutafsiri nomino iliyo katika wingi katika MC kwa nomino iliyo katika umoja katika MT. Aina hii ya ukiushi imejitokeza katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

**Mfano 11**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Wangeci : …*Irũrũ ici kaĩ ciatuĩkire wĩra?* (uk 12)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*)Wangeci :…Hii pombe imekuwa kama kazi? (uk 12)

Katika mfano huu, waandishi wa Matini Chanzi wamerejelea aina nyingi za pombe kwa kutumia maneno '*Irũrũ ici'* ambazo Wangeci analalamikia kuwa zimewapotosha baadhi ya jamaa. Hii ina maana kwamba waandishi wa Matini Chanzi wametumia kauli ya wingi kurejelea pombe. Hata hivyo, mtafsiri amekiuka jambo hilo kwa kutafsiri katika umoja kwa kutumia maneno 'Hii pombe' anaporejelea pombe zilezile zilizorejelewa na waandishi asilia. Huu ni ukiushi wa kisarufi wa kukiusha wingi kwa umoja. Ukiushi huu hata hivyo haujathari kubwa katika uwasilishaji wa maana iliyokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi kwani licha ya kupotosha maana hasa iliyodhamiriwa, kwa kubadilisha nomino pombe kuelekea umoja, maana ya ujumbe inaeleweka kwa Hadhira Pokezi ya Matini Tafsiri ya lugha ya Kiswahili.

Mfano mwingine wa ukiushi wa kisarufi kuhusu umoja na wingi umejitokeza katika mfano ufuatao:

**Mfano 12**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Mũtoongoria: *Arĩa matarĩ wako kana* *cieya*, (uk 15)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kiongozi: Wasio na pa kujenga au kikata (uk 15)

Katika mfano huu, waandishi wa Matini Chanzi wametumia nomino ya wingi (*cieya)*. Mhusika anayezungumza, (Kiongozi wa dhehebu la mafukara) alikuwa akielezea umasikini walio nao waumini au wafuasi wa dhehebu hilo lake. Hii ndio sababu wanakuja kwa Kĩgũũnda kumwomba mchango wake katika haraambe yao ya kujenga kanisa. Licha ya waandishi wa Matini Chanzi kutumia nomino ya wingi kurejelea vikata ambavyo wafuasi hawa hawana, mtafsiri alikiuka kanuni kwa kutumia nomino ya umoja (kikata). Inawezekana kuwa mtafsiri amekiuka sarufi ya wingi kimakusudi ili kutilia mkazo umasikini mwingi waliokuwa nao washiriki wa dhehebu hili la mafukara kwa kuonyesha au kumaanisha kuwa hawakuwa na hata kikata kimoja cha kujengea kanisa lao. Ukiushi huu kwa hivyo umekuwa na athari ya kutilia nguvu kauli ya mtafsiri ya kusisitiza umasikini wa waumini hao. Kwa hivyo ukiushi huu japo umepotosha maana dhamiriwa, umesaidia kutilia mkazo umasikini waliokuwa nao wafuasi wa *Dini ya Waamathĩna* (Dhehebu la wenye Dhiki). Ukiushi mwingine ambao umejitokeza katika mfano huu ni kuwa mtafsiri hajaweka alama ya kituo kikuu mwishoni mwa msitari huo, kama walivyofanya waandishi wa Matini Chanzi. Hata hivyo, ukiushi huu hujaathiri maana iliyokusudiwa na Waandishi Asilia.

### 3.4.5 Ukiushi katika Uchapishaji

Tumetambua katika utafiti huu kuwa kuna makosa mengi ya uchapishaji na makosa ya tahajia yaliyojitokeza katika Matini Tafsiri. Tunaona ni kwamba mtafsiri hakufanya udurusu na mapitio ya kutosha ya matini yake. Graham katika Picken (1983) anadai

kwamba mtafsiri anafaa kupitia, kudurusu na kuihariri Matini Tafsiri yake kwa uangalifu na kuhakikisha haina makosa yoyote ya uchapishaji au tahajia kabla ya kuichapisha. Hata hivyo, kuna makosa kadha ya uchapishaji na tahajia katika Matini Chanzi. Mtafsiri ameyakiuka makosa hayo kwa kuyarekebisha katika matini yake badala ya kuyarudia au kuyahawilisha. Kosa moja lililojitokeza katika ukurasa wa 37 wa MC ni kuwa waandishi Ngũgĩ na Ngũgĩ wameliendeleza jina la mhusika Wangeci visivyo kwani wameliandika kama Wongeci. Herufi ya pili ya jina la mhusika huyu inastahili kuwa 'a' bali si 'o'. Mtafsiri Kabugi amelikiuka kosa hili kwa kuliandika kwa usahihi katika ukurasa wa 34 wa MT.

Katika ukurasa wa 78, wa *Ngaahika Ndeenda*, waandishi wa Matini Chanzi wameliendeleza neno moja visivyo lakini mtafsiri akalikiuka na kulirekebisha kosa hilo kama ifuatavyo:

**Mfano 13**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Njooki: *Na wewaririe mũno.* (uk 78)
MT (*Nitaolewa Nikipenda)* Njooki: Na wewe *nawe umesema* sana. (uk 72)

Neno *'wewaririe'* si sahihi. Limeunganisha kimakosa maneno mawili; '*we'* na '*waririe'* yenye maana ya *'wewe umesema'* au *'wewe umezungumza'* ambayo yangefaa kutenganishwa. Mtafsiri amelikiuka kosa hili kwa kuliweka ipaswavyo katika ukurasa wa 72 wa Matini Tafsiri.

Kosa lingine la tahajia ambalo limetokea katika MC na mtafsiri Kabugi akalikiuka ni hili lifuatalo:

**Mfano 14**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gathoni: *Ngaahika Ndeenda.* (uk 24)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gathoni: Nitaolewa nipendapo. (uk 23)

Katika mfano huu, waandishi wa MC wametanguliza neno *'Ndeenda'* kwa herufi kubwa ilhali si nomino ya pekee wala neno hilo halijitokezi mwanzoni mwa sentensi kama inavyohitajika katika sarufi ya Kiswahili. Waandishi wa Matini Chanzi au mhariri wa Matini Chanzi angefaa kutumia '*n*' ndogo wala si *'N'* kubwa. Mtafsiri ameamua kukiuka kosa hilo na badala yake kulirekebisha. Licha ya mtafsiri Kabugi kukiuka makosa ya tahajia yaliyotokea katika Matini Chanzi kwa kuyarekebisha katika MT, makosa mengi ya tahajia yamejitokeza katika MT ya *Nitaolewa Nikipenda*. Hata kwenye hati-miliki, jina la mwandishi mmoja limeendelezwa visivyo kama ifuatavyo:

**Mfano 15**

©Ngug wa Thiong'o na Ngugi wa Mirii

Katika mfano huu, herufi 'i'katika jina la mwandishi Ngũgĩ wa Thiong'o imekiukwa. Aidha, majina hayo hayajaakifishwa kikamilifu kwani alama za wimbi hazikuwekwa juu ya baadhi ya vokali kama vile 'u' na 'i' kama inavyopaswa kuwa kwa mujibu wa kanuni za uandishi za Lugha Chanzi ya Gĩkũyũ.

Katika ukurasa wa 12 wa MT, neno 'kisisi' limeendelezwa visivyo. Neno sahihi lingefaa kuwa 'kasisi'. Neno hilo liko katika wimbo ulioimbwa na Mlevi. Mtafsiri ameliendeleza neno hili visivyo.

**Mfano 16**

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Mlevi: Nitaoa nipendapo,

kisisi hajaoa. (uk 12)

Ninaonelea kuwa hili ni kosa la uchapishaji au uhariri wala si ukiushi wa kimakusudi wa mtafsiri. Aidha kosa la tahajia limejitokeza katika ukurasa wa 16 wa Matini Tafsiri ambapo neno 'kufifia' limeendelezwa visivyo. Neno hili limeendelezwa visivyo kwa kuichukulia herufi ‘f ’ kama vokali ‘ĩ’. Ukiushi huu wa uakifishaji unailetea hadhira ya Matini Tafsiri utata kwa kuwa neno lililochapishwa kwenye MT halieleweki. Kwa jumla, makosa mbalimbali ya uakifishaji yamejitokeza kwenye Matini Tafsiri. Tunaonelea kuwa makosa mengine ya tahajia katika MT huenda yamesababishwa na tofauti za kigrafolojia na kifonolojia kati ya Lugha Chanzi ya Gĩkũyũ na Lugha Pokezi ya Kiswahili. Gĩkũyũ, tofauti na Kiswahili, kina vokali mbili zaidi ya vokali a, e, i, o, u nazo ni ‘ĩ’ na 'ũ'. Mtafsiri amezitumia vokali hizi za lugha ya Gĩkũyũ katika majina ya baadhi ya wahusika katika Matini Pokezi ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ina vokali tano; a, e, i, o, u.

### 3.5 Ukiushi wa Kisemantiki

Semantiki ni taaluma ya kiisimu inayojishughulisha na maana na pia huitwa elimu-maana. Mathews (1997) anajadili kuwa taaluma hii ya maana huhusisha sio tu maana ya kileksia ya neno bali pia maana ya tamko kutegemea muktadha na matumizi yake katika fungu la maneno. Ukiushi wa kisemantiki ni aina ya ukiushi ambapo mtafsiri huandika neno ambalo maana yake si kisawe cha maana yake katika Matini Chanzi. Akizungumzia juu ya tafsiri ya kisemantiki, Mwansoko (1996) anasema mtafsiri hutafsiri kila neno katika sentensi jinsi lilivyo lakini kwa kufuata sarufi (miundo ya kisemantiki na kisintaksia) ya lugha lengwa. Tafsiri ya kisemantiki huwekea mkazo kwenye maana ya matini kama ilivyokusudiwa na

mwandishi. Kwa ajili hii, tumechukulia ukiushi wa kisemantiki kama ukiushi ambao humfanya mtafsiri kutafsiri neno au kishazi katika sentensi visivyo kwa kutozingatia maana au kwa kutotilia maanani maana halisi yaani kwa kukiuka maana iliyokusudiwa na mwandishi wa Matini Chanzi. Ukiushi wa kisemantiki umejitokeza katika sehemu nyingi za Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*. Hata hivyo, tutatoa mifano michache kutoka kila kitendo (cha kwanza hadi cha tatu) na kutoa ufafanuzi.

Katika maelezo ya kwanza mchezo huu wa kuigiza unapoanza, mtafsiri ameandika kuwa "...tunaweza kuona magurudumu ya gari hapo karibu na kitanda." (uk 11 wa MT). Hii si maana halisi iliyodhamiriwa na waandishi wa Matini Chanzi. Maana iliyokusudiwa si magurudumu bali ndala (viatu) zilizotengenezwa kwa gurudumu aumagurudumu kama inavyodhihirika katika Matini Chanzi: *"...tũkuona iratũ cia nginyĩra*...." (uk 11) yaani " tunaweza kuona viatu.......". Hizi ni kama ndala zinazovaliwa na Morani wa Kimaasai.

Katika ukurasa wa 29 wa MT, ukiushi wa kisemantiki umejitokeza kama ifuatavyo:

**Mfano 17**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Wangeci: *ĩĩni!* (uk 27)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Wangeci: Ndiyo. Mimi! (uk 29)

Hapa tunatambua kuwa mtafsiri amekiuka maana halisi ya neno ĩĩni!katika MC ambalo maana yake ni "Sii ndiyo!" ama "Au sio!" wala sio "Ndiyo, mimi !" ambayo tafsiri yake katika Lugha Chanzi ingekuwa "ĩĩ, niĩ !" Ni dhahiri kuwa mtafsiri amekiuka maana halisi ya neno hilo katika Matini Chanzi kimakusudi kabisa ili kusisitiza ujumbe na maana kwa sababu ya kukuza maudhui yanayokusudiwa na tamthilia hiyo.

Ukiushi wa kisemantiki umejitokeza katika kitendo cha pili kama ifuatavyo:

**Mfano 18**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Kĩgũũnda:...*kũraathimithia ũhiki witũ na Wangeci*.

(uk 67)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda:.kuthibitisha ndoa yetu na Wangeci. (uk 62)

Maana halisi ya neno *'kũraathimithia'* likitafsiriwa katika Lugha Pokezi ya Kiswahili ni 'kuombea baraka' ama 'kubariki' wala si 'kuthibitisha'. Mhusika aliyetamka maneno haya alikuwa akizunguzia suala la kufanya harusi kanisani ili ndoa yao na mkewe iweze kubarikiwa. Tukizingatia kuwa mtafsiri Kabugi ni mmilisi wa Lugha Chanzi ambayo ni lugha yake ya kwanza na vilevile Lugha Pokezi ya Kiswahili ambayo alikuwa ameifundisha na ni taaluma yake, ukiushi huu wa neno hili na kulitafsiri kama 'kuthibitisha' umekusudiwa kutilia mkazo maana iliyokusudiwa na waandishi asilia. Ndoa hii iliyokusudiwa 'kuthibitishwa' ndiyo iliyoleta mpomoko wote wa maisha ya Kĩgũũnda ambaye ndiye mhusika mkuu katika mchezo huu wa kuigiza. Tunaonelea kuwa kupitia ukiushi huu, mtafsiri amefaulu kuleta athari kwa Hadhira Pokezi ya matini yake sawa na ile iliyo kwenye hadhira ya Matini Chanzi ya tamthilia Ngaahika Ndeenda.

Aidha, ukiushi wa kisemantiki umejitokeza ifuatavyo katika Matini Tafsiri:

**Mfano 19**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gĩcaamba*: Rekeei tũthiĩ,* (uk 78)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Hebu tuagane, (uk 72)

Katika mfano huu, mtafsiri amekiuka maana ya maneno ya MC *"Rekeei tũthiĩ,"* ambayo maana yake katika Lugha Pokezi ni "Acheni twende," bali si "Hebu tuagane" kama ilivyoandikwa na mtafsiri katika MT. Mtafsiri Kabugi amekiuka maana iliyokusudiwa kimakusudi ili kubainisha maana ya tamshi hilo na kulifanya kueleweka vyema. Mtafsiri yamkini amehofia kuibua maana potovu ikiwa angetafsiri maana halisi ya *"Rekeei tũthiĩ,"* ambayo ni "Acheni twende," kwani Hadhira Pokezi ya Matini Tafsiri haingebaini kuwa kinachozungumziwa ni maagano kati ya watu wawili au makundi mawili ya wahusika.

Katika sehemu ya pili ya kitendo cha tatu, ukiushi wa kisemantiki umejitokeza ifuatavyo:

**Mfano 20**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Njeethibeeri*: Rekia rũhiũ rũu.* (uk 106)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Jespheli : Weka kisu chini (uk 98)

Maana halisi ya neno *'rũhiũ'* imekiukwa na mtafsiri kwa kuwa maana yake halisi katika Lugha Pokezi ya Kiswahili si kisu bali sime/simi/upanga au jambia. Maana ya neno 'kisu' katika Lugha Chanzi ya Gĩkũyũ ni *'kahiũ'* bali *si 'rũhiũ'*. Ninaonelea kuwa mtafsiri ameamua kutumia neno 'kisu' ili kuifanya hadhira kuelewa bila utata kuwa kinachozungumziwa ni aina ya ala au silaha ya vita. Tumezingatia kwamba kuna wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili wasioelewa ala kama sime, simi au jambia na pengine wangetatanishwa na kukosa kuelewa ujumbe wa mwandishi. Kwa sababu hii, tunaona kuwa mtafsiri alikiuka maana dhamiriwa na badala yake kuteua neno 'kisu' ambao ni msamiati unaojulikana na wazungumzaji wengi zaidi wa lugha ya Kiswahili.

Kuna mfano mmoja wa ukiushi wa kisemantiki katika kitendo cha tatu kama ifuatavyo:

**Mfano 21**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Wangeci*: Rekeei anjũrage arĩe nyama icio!* (uk 112)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Wangeci: Hebu mwacheni aniue ale nyama yangu! (uk 104)

Mtafsiri Kabugi amekiuka maana halisi ya neno *'icio'* ambalo maana yake katika Lugha Pokezi ya Kiswahili ni 'hizo' bali si 'yangu'. Mtafsiri kupitia ukiushi huu ametilia mkazo na kuonyesha uhasama ulioko kati ya wahusika wanaogombana katika tamthilia hii yaani Wangeci na mumewe Kĩgũũnda. Aidha, ni oni langu kuwa mtafsiri asingekiuka maana hiyo, maana kusudiwa ingefichika kwani angeandika, "Hebu mwacheni aniue ale nyama hizo." Hadhira Pokezi haingeelewa nyama inayorejelewa au nyama zinazorejelewa. Kutokana na ukiushi huu, mtafsiri ameleta mawasiliano mwafaka na hadhira ya Matini Tafsiri kwa kutumia neno 'yangu' badala ya 'hiyo' au 'hizo'.

### 3.5.1 Ukiushi wa Kisemantiki kwenye Methali

Massamba (1985) anadai kuwa methali ni picha ya maisha kwa ufupi, ukweli wa namna ya kuishi na watu wa jamii yako. Methali ni aina ya misemo inayotumiwa na wanajamii kupigia mifano, kuasa, kuonya au kushauri. Changamoto moja kubwa iliyomkabili mtafsiri Kabugi katika kuitafsiri tamthilia Ngaahika Ndeenda kwa Kiswahili ni kuweko kwa methali nyingi za Lugha Chanzi kwenye Matini Chanzi. Baadhi ya methali hizi za Gĩkũyũ zinaonekana zilimtatiza mtafsiri katika kuzihawilisha kwa urahisi katika Lugha Pokezi ya Kiswahili kwani zinahusiana na mazingira na utamaduni wa jamii ya Wagĩkũyũ inayoitumia lugha hiyo.

Mtafsiri ametatua tatizo la kuwepo ugumu katika kutafsiri methali za Lugha Chanzi kwa kutumia methali za Lugha Pokezi ya Kiswahili zenye maana inayokusudiwa na waandishi

wa Matini Chanzi. Inaposhindikana, mtafsiri anatumia tafsiri ya moja kwa moja (neno kwa neno) kuitafsiri methali husika. Wakati mwingine, anatumia tafsili yaani kutoa maelezo kwa kusudi la kuifafanua methali husika. Ifuatayo ni mifano ya methali ambazo maana ya maneno yake imekiukwa na mtafsiri kwa kusudi la kuwasilisha ujumbe na maana halisi iliyokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi. Katika mfano huu mtafsiri hajazingatia maana ya maneno halisi yaliyotumiwa na Waandishi wa Matini Chanzi. Badala yake ametumia maneno tofauti kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa na maneno ya waandishi wa Matini Chanzi.

**Mfano 22**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Kĩgũũnda: *Ti ithaga rĩene,*
*Rĩrĩa rĩerirwo rĩnogagia ngiingo.*
*Mũndũ ainaga na gatiirũ gaake.* (uk 11)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Hii si nguo ya kuazima,
Ambayo haisitiri matako
Kila ndege huruka kwa ubawa wake.(uk 11)

Takribani maana ya maneno yote ya methali tatu zilizotumika katika mfano huu yamekiukwa katika MT. Cha muhimu hata hivyo ni kuwa kila mojawapo ya methali hizi katika MT imetoa maana ile ile inayokusudiwa na waandishi wa MC kuwasilisha maudhui yanayodhamiriwa na tamthilia yenyewe. Isingekuwa ukiushi huu, methali hizo zingetafsiriwa ifuatavyo na hivyo kutatanisha maana kwa Hadhira Pokezi ya wasomaji wa Kiswahili:

* Hii si johari ya wenyewe,

*Iliyosemwa kuwa huichosha shingo.  ( la anayeitamani)

* Kila mtu hujivunia kipande chake.

Tumetambua kuwa kwa kuzitafsiri methali hizi kiukiushi, maana ya ujumbe wake imebainika kwa njia mwafaka zaidi kwa hadhira ya Matini Tafsiri na hivyo kuleta mawasiliano mwafaka kati ya MT na Hadhira Pokezi. Isitoshe, athari inayopatikana kutokana na ujumbe ulio kwenye methali hizo ni sawa kwa hadhira zote mbili za Matini Chanzi na Matini Tafsiri kutokana na ulinganifu wa maana unaopatikana.

Katika ukurasa wa 13, methali za Lugha Chanzi zimetafsiriwa kwa kutumia methali za Lugha Pokezi lakini zenye maana sawa na iliyokusudiwa katika Matini Chanzi. Mtafsiri amekiuka maana ya maneno yaliyo kwenye methali za Matini Chanzi.

**Mfano 23**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Kĩgũũnda: *Thĩĩna ndũrĩ njaamba na mũũgĩ ndooĩ ũrĩa akeerwo.*(uk 13)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Taabu ni laana; Tahadhari kabla ya athari. (uk 13)

Mtafsiri asingekiuka maana ya maneno yaliyo kwenye methali hizi mbili, angezitafsiri vifuatavyo; Taabu haina shujaa na mwerevu hajui atakavyoambiwa. Hii ina maana kuwa Hadhira Lengwa ya Matini Tafsiri ya Kiswahili haingeelewa kabisa maana inayokusudiwa kwa kuwa hakuna methali kama hizi katika Kiswahili. Ukiushi wa mtafsiri basi umeifaidi hadhira yake kwa kuwa umeweka bayana maana halisi ya methali inayodhamiriwa na waandishi wa Matini Chanzi.Ingawa tumeongozwa na Nadharia ya mawasiliano katika tafsiri ya Nida (1964) katika utafiti huu, mawazo ya Oduori katika Ogechi na Shitemi

(2008) yamefaa zaidi katika kulinganua jinsi mtafsiri Kabugi alivyozitafsiri methali za MC ya *Ngaahika Ndeenda* katika MT ya Kiswahili ya *Nitaolewa Nikipenda.* Mtaalamu huyu anasema ifuatavyo;

> "Katika kukuza ubora wa lugha mara nyingi panaulizwa, methali, kwa mfano, huweza kutafsirika? Jibu ni ndio. Itategemea mwelekeo utakaochukuliwa. Ikiwa kisawe cha methali hiyo kitaweza kupatikana, katika lugha pokezi basi kitumiwe.................Ikiwa ni vigumu kupata kisawe, basi (methali) inaweza kuelezwa lakini kwa kutopotosha maana. Hapa ndipo nadharia ya ulinganifu na usawazisho hutatiza baadhi ya watafsiri kwa maana ya kutaka kulinganisha neno na mpangilio baina ya lugha mbili."

Aidha, Obuchi katika Ogechi na Shitemi (2008) anadai kuwa wahakiki wengi wa kazi za fasihi huelekea kutumia zaidi ya nadharia moja katika harakati za kiuchambuzi. Katika kufanya hivyo, wahakiki hao hutambua ukweli kwamba hakuna nadharia ambayo ni gangasaba, kwa maana kwamba ina uwezo mkubwa wa kutosheleza mahitaji yote ya kiutafiti. Anaongeza kuwa mhakiki wa kazi ya fasihi ana uhuru wa kuteua mkondo ambao anaamini utamwezesha kuyafikia malengo yake. Kwa hivyo, uhakiki na uchambuzi wa tafsiri za methali za MC tunayoishughulikia kuelekea MT umeongozwa na nadharia ya uhamishaji katika uamilifu kama ilivyopendekezwa na Reiss (1971) wala si nadharia ya mawasiliano katika tafsiri ya Nida (1964). Wakati mwingine, mtafsiri Kabugi ametatizika jinsi ambavyo angezitafsiri baadhi ya methali zisizo na visawe vyake katika Lugha Pokezi. Hapo imemlazimu kukiuka maana ya maneno kwenye methali na badala yake kutumia maelezo ili kuwasilisha maana inayokusudiwa na waandishi wa MC kama katika mfano ufuatao:

**Mfano 24**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Wangeci: *Ningĩ <u>mathanwa</u> me <u>kĩondo</u> kĩmwe matiagaga*

*Gũkomorania.* (uk 25)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Wangeci: Aidha, vyuma vikiwa katika gunia moja

havikosi kugongana. (uk 24)

Katika mfano huu, maneno yaliyokiukwa maana yake ni *'mathanwa'*ambalo tafsiri yake ingekuwa 'shoka' bali sio vyuma. Aidha tafsiri sahihi ya neno *'kĩondo'* tafsiri ni 'kikapu' ama 'chondo' bali si 'gunia'. Hata hivyo maana ya ujumbe unaokusudiwa na waandishi asilia umewasilishwa vyema kwa Hadhira Pokezi ya Matini Tafsiri na hivyo kuleta athari sawa kwa hadhira za MC na MT kama anavyojadili na kupendekeza Nida (1964) katika Nadharia yake ya *Ulinganifu wa Mawasiliano.*

Methali zingine katika Matini Chanzi ambazo zipo katika Lugha Chanzi ya Gĩkũyũ lakini hazina tafsiri ya moja kwa moja katika Lugha Pokezi ya Kiswahili ni hizi zifuatazo:

**Mfano 25**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) *Kĩgũũnda: Kaĩ mũrũmĩrwo ndamenyaga igĩthira-ĩ?*

*Kaĩ ũũĩ kũruta nĩ gũcokia?* (uk 26)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Kweli mpewa hajui akiba ikimalizika.

Chovya chovya humaliza buyu la asali? (uk 25)

Katika mfano huu, mtafsiri amekiuka maana ya moja kwa moja ya maneno ya methali za Lugha Chanzi na kuwasilisha maana hizo kwa kutoa maelezo (Kweli mpewa hajui akiba ikiisha.) na kisha kwa kutoa methali ya Lugha Pokezi (Chovya chovya humaliza buyu la asali.) Kwa kufanya hivi, mtafsiri ameweza kuwasilisha ujumbe halisi uliokusudiwa, kwa hadhira yake bila utata kupitia ukiushi huo.

Katika kitendo cha pili, mtafsiri amekiuka maana ya maneno na kutafsiri methali ifuatavyo:

**Mfano 26**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gĩcaamba: *Gũtirĩ wĩĩriraga agĩthiĩ ta agĩcooka. Wĩĩmenyererendũkoorwo nĩ inya ũteng'ereire inyaanya.*(uk 67)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Majuto ni mjukuu. Jihadhari usiponyokwe na nne ukitarajia kupata nane. (uk 62)

Katika mfano huu, mtafsiri amekiuka kimakusudi maana ya maneno kwenye methali ya kwanza kwa kuitafsiri kuwa 'majuto ni mjukuu'. Tafsiri ya neno kwa neno ingekuwa 'hakuna anayejuta akienda kama akirudi'. Tafsiri hii ya neno kwa neno haingeleta maana yenye mantiki kwa Hadhira Pokezi ya lugha ya Kiswahili kwa kuwa ingekuwa tata. Kwa sababu hii, mtafsiri ameamua kukiuka maana ya maneno kwenye methali kwa kutumia methali ya Lugha Pokezi yenye kuwasilisha maana iliyokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi. Hata hivyo, kwa ajili ya ukosefu wa tafsiri ya methali ya pili katika Lugha Pokezi ya Kiswahili, mtafsiri ameamua kutoa maelezo ya moja kwa moja au neno kwa neno kutoka LC kuelekea LP yaani 'Jihadhari usiponyokwe na nne ukitarajia kupata nane.'Aidha, mtafsiri amekiuka kimakusudi maana ya maneno na kutafsiri methali ifuatavyo:

**Mfano 27**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gĩcaamba: *Na ya gwĩĩthuurĩra ndĩrĩ ihĩndĩ.* (uk 78)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Na kipendacho moyo ni dawa. (uk 72)

Tafsiri ya moja kwa moja ya methali hii katika Lugha Pokezi ya Kiswahili ingekuwa;

*'Na ya kujichagulia haina mfupa.'

Kwa kuhofia kupotosha maana halisi inayokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi, mtafsiri ameamua kukiuka maana ya maneno kwenye methali hii na badala yake kuibua na kutumia methali mbadala ya Lugha Pokezi yenye kusheheni maana ile ile iliyokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi. Kupitia ukiushi huu, mtafsiri anafaulu kuboresha mawasiliano kati yake na hadhira yake na vilevile kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi ya tamthilia Nitaolewa Nikipenda.

Katika kitendo cha tatu, ukiushi wa kisemantiki katika methali umejitokeza katika mfano ufuatao:

**Mfano 28**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gĩcaamba: *Ĩrĩ kũhũũma ndĩrĩ mũtĩ ĩtangĩgwaatĩrĩra.* (uk 107)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Mbio za sakafuni huishia ukingoni.(uk 99)

Ni bayana kuwa maana ya maneno katika njozi hii ya methali hailingani kamwe. Mtafsiri ametumia methali ya Lugha Pokezi yenye kuwasilisha maana inayokusudiwa katika MC. Mtafsiri amekiuka maana halisi ya maneno ya methali ya MC kwani kama angeitafsiri kuwa 'Akishachoka (mnyama wa pori), hakuna mti asioweza kuuegemea', msomaji wa MT yaani Hadhira Pokezi haitaelewa maana inayokusudiwa katika tamthilia hiyo. Isitoshe, mawasiliano kati ya mtafsiri na hadhira yake hayangekuwa mwafaka kumaanisha kwamba dhamira ya waandishi wa Matini Chanzi haingetimizwa ikiwa ukiushi huu wa mtafsiri haungekuwepo.

### 3.5.2 Ukiushi wa Kisemantiki katika Nahau

Nahau ni maneno yanayotumiwa pamoja kutoa maana fulani japo maneno hayo yakitumiwa kipwekepweke yanaweza kutoa maana tofauti (TUKI 1980). Ukiushi wa

kisemantiki katika nahau hujitokeza wakati ambapo mtafsiri hukiuka kuyatafsiri kipwekepweke maneno yaliyoko kwenye nahau ya Matini Chanzi. Badala yake, mtafsiri hulitafsiri wazo au ujumbe ulioko kwenye hiyo nahau kwa kutumia maneno tofauti ya Lugha Pokezi ambayo yanakidhi wazo au ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa Matini Chanzi. Wakati mwingine mtafsiri huweza kutumia nahau nyingine ya Lugha Pokezi yenye kusheheni maana ile ile iliyokusudiwa katika Matini Chanzi.

Tumegundua kuwa maana ya maneno katika nahau za MC aghalabu inakinzana na maana ya maneno ya nahau hizo katika MT. Kwa sababu hii, nadharia ya ulinganifu inatatizika katika uhakiki wa tafsiri za nahau katika matini hizi. Mtazamo wa kiuamilifu katika misingi ya dhana ya uhamishaji ilifaa zaidi hapa. Reiss (1971) anajadili kuwa ulinganifu wa maana ya maneno hauwezekani katika hali zote. Kwa mfano pale ambapo Matini Tafsiri inanuia kutekeleza jukumu tofauti na lile la Matini Chanzi tukizingatia kuwa jukumu la Matini Chanzi lilikuwa ni kuigizwa katika jukwaa la wazi, tofauti na Matini Tafsiri ambayo jukumu lake ni kuitafsiri Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* ili iweze kusomwa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Waandishi wa Tamthilia Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda* wametumia nahau kadha katika tamthilia hiyo. Mtafsiri Kabugi katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* amezitafsiri ama kwa kukiuka maana ya maneno yaliyotumiwa kwenye nahau zenyewe au kutumia badala yake nahau za Lugha Pokezi ya Kiswahili. Nahau hizi zinawasilisha maana ya ujumbe unaokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi iliyoko katika lugha ya Gĩkũyũ. Ifuatayo ni mifano ya baadhi ya nahau hizo kama zilivyowasilishwa katika MC na katika MT:

**Mfano 29**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Mũrĩĩu:.*Kana watuĩkire wohagwo na mũthuru ?* (uk 12)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Mlevi: …......Au umekuwa mkaa jikoni? (uk 12)

Ukiushi ulioko hapa ni kuwa maana ya MC ni, 'Ama umekuwa wa kufungwa leso (na mkeo ili usitoke nje)?' Ili kuwasilisha maana hasa inayokusudiwa na waandishi wa MC, mtafsiri amekiuka maana ya maneno katika hiyo nahau kwa kutumia maneno yanayowasilisha maana iliyokusudiwa ya 'kukaa jikoni' yaani kudhibitiwa (na mkewe). Maneno haya yalielekezwa kwa Kĩgũũnda aliyekuwa akikashifiwa na Mlevi kwa kutotoka naye ili waende naye ulevini. Ukiushi wa maneno katika nahau unatumika pia katika mfano ufuatao:

**Mfano 30**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gĩcaamba: *Githĩ mũndũ ti witũ na Ngai?* (uk 42)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Si anakaribia kuwa marehemu? (uk 40)
Katika mfano huu, mtafsiri amekiuka maana msingi ya maneno ya nahau hiyo ambayo maana yake haiafikiani na maneno ya nahau hiyo katika Matini Chanzi. Mtafsiri amekiuka maana ya maneno ya nahau hii kwa kutafsiri kuwa mhusika anayerejelewa alikuwa 'anakaribia kufa'.Katika kitendo cha tatu, ukiushi wa kisemantiki katika nahau unajitokeza ifuatavyo:

**Mfano 31**

MC (*Ngaahika Ndeenda*)Gĩcaamba: *Ngookĩra rĩrĩa Maara aateire nyina.* (uk 96)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Nitaamka alfajiri na mapema. (uk 88)

Waandishi wa Matini Chanzi wametumia nahau ya kiasili ya Lugha Chanzi yenye maana ya 'alfajiri na mapema' lakini haitafsiriki katika lugha ya Kiswahili moja kwa moja au neno kwa neno kwa sababu italeta maana potoshi kabisa. Nahau hii ni ya kiasili na inagusia utamaduni na mazingira ya jamii ya Lugha Chanzi. Hatukuelewa katika utafiti huu sababu ya waandishi wa Matini Chanzi kutanguliza jina *'Maara'* kwa herufi kubwa kana kwamba ni nomino ya kipekee kwani hatujapata kumsikia kiumbe ama mtu kama huyo katika historia. Ninaafiki kuwa mtafsiri kupitia ukiushi huu amefaulu kuwasilisha maana ya ujumbe wa waandishi wa Tamthilia Chanzi na hivyo kuleta athari sawa kwa hadhira ya MC na hadhira ya MT.

Mfano mwingine wa nahau ya jamii ya Lugha Chanzi iliyotafsiriwa kwa ustadi mkubwa katika MT ni huu ufuataao:

**Mfano 32**

MC (*Ngaahika Ndeenda*)Kĩgũũnda: *Toondũ nĩ guoka mbĩa hiũ.* (uk 103)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Kwa kuwa mambo moto moto yamezuka. (uk 96)

Katika mfano huu, *'nĩ guoka mbĩa hiũ'* ni nahau ya kiasili ya Lugha Chanzi na ikitafsiriwa moja kwa moja kwa kutafsiri maneno kipwekepweke italeta maana isiyoeleweka katika Lugha Pokezi ya Kiswahili. Nahau hii ikitafsiriwa moja kwa moja kutoka Lugha Chanzi hadi Lugha Pokezi itamaanisha, 'kumekuja panya moto', usemi ambao hauna mantiki yoyote katika Lugha Pokezi ya Kiswahili. Hii ndiyo sababu mtafsiri Kabugi anaamua kukiuka maana ya maneno katika nahau hii ili kuleta mawasiliano mwafaka kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi.

Mtafsiri ameamua kuwasilisha maana ya nahau hiyo ya Lugha Chanzi iliyoandikwa kwenye Matini Chanzi badala ya kuhawilisha maana ya maneno yaliyopo kwenye hiyo nahau. Kwa ajili ya ukiushi huu wa kisemantiki, mtafsiri anafaulu kuepuka utata ambao ungetokea endapo angetafsiri maneno ya nahau hiyo kipwekepweke. Anaepuka kuleta maana potoshi na isiyokubalika katika mazingira na muktadha wa Hadhira Pokezi ambayo labda haingeelewa na ingestaajabia wazo la "kuja kwa panya moto". Hadhira Pokezi ya lugha ya Kiswahili inayopatikana aghalabu katika ukanda wa Afrika Mashariki haina mazoea ya kutumia panya kama chakula. Kwa sababu hii, mtafsiri amekiuka maana ya maneno ya nahau hiyo ya MC kwa kutumia maneno ya nahau ya Lugha Pokezi kuwa 'kumezuka mambo moto moto' au ya dharura. Kwa kufanya hivyo mtafsiri amefanikisha mawasiliano mwafaka na Hadhira Pokezi.

### 3.5.3 Ukiushi katika Nyimbo kwenye Tamthilia

Holz-Manthari katika Nord (1997) anaelezea kuwa tafsiri inahusu uhamishaji baina ya tamaduni tofauti na katika uhamishaji huu anazingatia na kuibua dhana ya "vipasha ujumbe" kama vile maandishi, matumizi ya picha, sauti, miondoko au ishara za mwili. Anafafanua tafsiri kama kitendo changamano chenye nia maalum. Ingawa mtaalamu huyu hakuzingatia umuhimu wa Matini Asilia katika tafsiri, tunakubaliana na maoni yake kwa kuwa nyimbo nyingi na maigizo katika Matini Chanzi zinahitaji kutafsiriwa katika Matini Tafsiri.

Katika kitendo cha kwanza, ukurasa wa 13 wa MC na MT pana wimbo ulioimbwa na "wafuasi wa dini ya watu wasio na mashamba, wasio na pa kujenga au kikata na wasio na nguo." Watu hao waliongozwa kuimba wimbo huo na kiongozi wao. Pana ukiushi mwingi katika tafsiri ya wimbo huo katika MT kwa kuwa utaratibu wa mishororo minane ya

kwanza umekiukwa na ni tofauti kimaana na ilivyo katika MC. Yamkini mtafsiri amekosea na kuchanganya mishororo ya wimbo huo. Kwa sababu hii, ukiushi unaonekana umejitokeza kiajali. Idhibati iliyoko ni katika mishororo ya pili na tano inayosema, “Shetani azikwe na papandwe miti, apondwe na kaburi litiwe saruji.” mishororo ambayo inajitokeza katika mishororo ya baadaye zaidi katika Matini Chanzi.Katika wimbo wa *Nyangwecũ* ulio katika ukurasa wa 30, kitendo cha kwanza, ukiushi umejitokeza kwa kuwa mishororo miwili ifuatayo imedondoshwa na haijitokezi kamwe katika MT:

*Wangeci wa maitũ nĩtwarega-ĩ*
*Wangeci wa maitũ nĩtwarega-ĩ*

Tafsiri ya wimbo huu katika Lugha Pokezi ingefaa kuwa “Wangeci wa mama yetu tumekataa.”Katika ukurasa wa 44 wa MT, mtafsiri Kabugi ametumia uhuru wa mtafsiri kwa kufupisha viitikio vya wimbo huo, tofauti na ilivyo katika MC ili kufanya wimbo huo uimbike katika Lugha Pokezi. Hii ni aina ya ubunifu wa mtafsiri ambao kwa hakika unafanya wimbo huo na hasa mshororo huo uliofupishwa kuimbika. Mtafsiri amefupisha viitikio hivyo kama ifuatavyo:

**Mfano 33**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gĩcaamba: Ĩ *ngaiyĩrwo na marũa*. (uk 48)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: *'taondoka kwa barua.* (uk 44)
MC (*Ngaahika Ndeenda*)Gĩcaamba: *Ĩ ngwaria cia aruti a wĩra.* (uk 49)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: *'tasema ya vibarua*. (uk 45)

Tunapata katika mfano huu kuwa ukiushi huu wa mtafsiri wa kufupisha neno la kwanza la kiitikio unaufanya wimbo huu katika MT uimbike kwa mahadhi sawa na katika MC na hivyo kuleta athari sawa kwa Hadhira Pokezi kama vile kwa Hadhira Asilia.

Ukiushi wa kisemantiki (kimaana) umejitokeza katika wimbo ulioko katika ukurasa wa hamsini na mbili wa Matini Tafsiri ambapo neno 'kondoo' limetumiwa kama tafsiri ya neno la Lugha Chanzi *'managĩ'.* Maana ya kimsingi ya neno hili la Lugha Chanzi ni 'maajabu' wala si 'kondoo'. Mtafsiri amekiuka maana ya neno 'managĩ' kimakusudi ili kuleta mawasiliano mwafaka na Hadhira Pokezi. Mtafsiri asingekiuka maana halisi ya neno hilo hadhira ya MT ingekosa kuelewa maana msingi inayokusudiwa katika MC.

Hatimaye, mtafsiri Kabugi amekiuka uakifishaji katika wimbo ulioko katika ukurasa wa mwisho wa mchezo huu wa kuigiza. Katika mfano huu, Kiongozi wa wimbo huo anaita mbiu inayopokelewa na waimbaji. Ukiushi unavyojitokeza ni kuwa katika MC, Kiongozi anapoita hiyo mbiu, yaani *'Coro!',* kumewekwa alama ya hisi lakini katika MT, mtafsiri ameikiuka alama hiyo ya hisi na badala yake kutumia kikomo kama ifuatavyo:

**Mfano 34**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Mũkũi: *Coro!* (uk 117 – 118)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kiongozi: Mbiu. (uk 109 – 110)

Maana inayokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi iliathiriwa kwa kuwa katika MC, alama ya hisi kwenye maneno ya huyo Kiongozi inaonyesha hisia ya hasira waliokuwa nayo hao waimbaji. Ukosefu wa alama ya hisi katika MT unasababisha hadhira ya Matini Pokezi kukosa kuona hisia walizokuwa nazo hao waimbaji.Ninaonelea kuwa mtafsiri Kabugi aliamua kuipuuza alama hiyo ya hisi akiamini kuwa haingeathiri maana

iliyokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi. Hata hivyo, maana imeathirika kwa kuwa kila kiakifishi huwa na uamilifu wake katika uwasilishaji ujumbe.

Ukiushi wa alama za uakifishaji umejitokeza vilevile katika sehemu ya mwisho kabisa ya tamthilia. Katika wimbo huu wa ukombozi wa wafanyakazi, alama ya hisi imekiukwa katika Matini Tafsiri. Waandishi wa Matini Chanzi wameweka alama ya hisi mwishoni mwa mistari mingi lakini mtafsiri wa Matini Tafsiri akazikiuka kwa kukosa kuziweka alama hizo na badala yake kuziweka alama hizo za hisi katika Matini Tafsiri. Ukiushi huu umejitokeza ifuatavyo:

**Mfano 35**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Mũtongoria: Coro!

Oothe : Wa aruti a wĩra ni mũhuuhe! (uk 118)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kiongozi: Mbiu

Waimbaji: Ya wafanya kazi imepigwa. (uk 110)

Ukiushi huu wa alama ya hisi umeifanya Matini Tafsiri kuwa na athari tofauti na Matini Chanzi kwa kupunguza hisi katika Matini Tafsiri.

### 3.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumefafanua maana ya dhana ya ukiushi. Tumeelezea kwa kifupi kisa cha tamthilia husika. Tumechunguza na kuwajadili wahusika wanaoigizwa kwenye tamthilia kwa kusudi la kuangalia iwapo majina na sifa zao zimewakilishwa vilivyo katika Matini Tafsiri. Tumethibitisha kuwa wahusika wote wamesawiriwa kwa sifa na hulka zinazolingana katika matini zote mbili. Aidha, majina ya wahusika katika MT yanawiana na majina hayo katika MC.

Tumechambua muundo wa Matini Chanzi na Matini Tafsiri kuchunguza iwapo mwandishi wa MT alikiuka muundo wa Tamthilia Chanzi. Tumeona kuwa mtafsiri Kabugi amekuwa mwaminifu kwa Matini Chanzi kwa kuwa hajakiuka muundo wa hiyo tamthilia. Tumejadili katika sura hii aina tatu kuu za ukiushi uliojitokeza katika Matini Tafsiri yaani ukiushi wa kifonojia, wa kisintaksia na wa kisemantiki. Yote haya tumeyafanya kwa kutoa mifano kwenye tamthilia zote mbili mbali na kuonyesha kurasa mlimojitokeza mifano hiyo ya ukiushi. Isitoshe tumeelezea jinsi kila aina ya ukiushi inavyojitokeza mbali na kufafanua athari za kila ukiushi kwa hadhira lengwa. Aidha, tumechunguza na kuonyesha ukiushi wa makosa ya tahajia na uakifishaji umeotokea kwenye Matini Tafsiri.

# SURA YA NNE

# UMBUJI KAMA KIUNGO CHA UKIUSHI

## 4.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, tumejadili aina mbalimbali za ukiushi uliopo kwenye Matini Tafsiri mathalani ukiushi wa kifonolojia, wa kisintaksia na wa kisemantiki. Yote haya tumeyafanya kwa kutoa mifano kwenye tamthilia zote mbili (Matini Chanzi na Matini Tafsiri), kuilinganisha na kuonyesha kurasa mlimojitokeza mifano hiyo ya ukiushi. Aidha, tumeeleza jinsi kila aina ya ukiushi ilivyojitokeza mbali na kufafanua athari za kila mfano wa ukiushi kwa Hadhira Lengwa.

Katika sura hii ya nne, tumejadili uhusiano uliopo kati ya umbuji na ukiushi na kisha tumeonyesha jinsi umbuji katika ukiushi ulivyotumiwa na mtafsiri wa tamthilia Ngaahika Ndeendakuelekea *Nitaolewa Nikipenda.* Tumejadili aina nne za umbuji zilizotumiwa na mtafsiri nazo ni; matumizi ya tasifida, uhamishaji wa maneno ya MC bila kuyatafsiri, ubunifu wa mtafsiri na uziada.

## 4.1 Umbuji Katika Ukiushi

Umbuji ni taaluma ya kuchunguza uzuri katika sanaa ya fasihi andishi. Ni dhana yenye maana ya uzuri wa kazi ya kifasihi andishi kwa kufuata kaida zilizokubaliwa na wahakiki ili kupimia uzuri huo wa kazi ya kifasihi. Igendia (2003) anatoa kauli kuwa umbuji hutumiwa na mtafsiri kwa kusudi la kuivutia hadhira yake. Mtaalamu huyu anafafanua ifuatavyo:

> Umbuji ni kipengele cha mtindo kinachotumiwa katika sanaa ya fasihi tafsiri na ambacho kinamwezesha mtafsiri kuipa kazi husika utamu wake

> kimaana, kinachozingatia kaida zilizokubaliwa na ambazo zitaitumia lugha kama malighafi ya kuipimia kazi hiyo.
>
> (Igendia 2003:17)

Hata hivyo, mtafsiri huongozwa na muundo wa lugha, utamaduni na mazingira ya Hadhira Pokezi wakati anashughulikia umbuji katika kazi yake. Dhana ya umbuji inahusiana sana na mtindo. Mtafsiri anatakiwa kutalii mtindo wa Matini Asilia (au Matini Chanzi) ili kuuzingatia katika tafsiri. Umbuji ni ufundi anaotumia mtafsiri kuudhihirishia utamu wa lugha katika matini yake akiongozwa na mpangilio wa vitushi unaozunguka mgogoro pamoja na mabadiliko baina ya wahusika.

Sikuafikiana na wazo la Ryanga (1985) kuwa, nyingi za kazi zilizotafsiriwa lugha yake huwa ni ya kiwango cha chini. Hii ni licha ya kuwa tumepata makosa ya tahajia, ukiushi wa aina mbalimbali na hitilafu katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*. Mtafsiri ametumia ufasaha mwingi japo usifikie ule wa waandishi wa Matini Chanzi. Mtafsiri Kabugi amejaribu pakubwa kuyaendeleza maudhui ya ujumbe dhamiriwa bila ya kuupotosha. Mbali na makosa ya tahajia yaliyopo katika MT, mna makosa na 'dosari' nyingi zinazojitokeza katika MT ambazo hazijaathiri uthabiti wa mtafsiri katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye tafsiri. Kwa hakika, methali, nahau na nyimbo nyingi za kiasili katika Matini Chanzi, zimeleta ugumu katika kuzitafsiri. Hata hivyo, ninaonelea kuwa ujumbe wa Matini Tafsiri unakithi kuafiki ule ulioko kwenye Matini Chanzi.

Katika kuhawili ujumbe unaowasilishwa kwa hadhira ya MC, mtafsiri amefanikiwa kutumia umbuji unaompelekea kuibua ukiushi wa aina mbalimbali. Mtafsiri ametumia umbuji wake kuhusisha tasifida, ubunifu na uhusishi wa baadhi ya maneno na majina yaliyoko kwenye MC katika Matini Tafsiri. Kwa mfano mtafsiri amewasilisha baadhi ya

mapokezi ya maamkizi na miito moja kwa moja kutoka Lugha Chanzi kuelekea Lugha Pokezi badala ya kutafsiri. Wakati mwingine, mtafsiri ametumia umilisi wake dhabiti wa LC na LP kuwasilisha ujumbe wa MC kwenye MT. Mfano ni katika ukurasa wa sabini wa MT ambapo ameufasiri vyema wimbo husika kwa kuufupisha huku akihifadhi mahadhi yake asilia na wakati uo huo akiwakilisha ujumbe unaodhamiriwa na waandishi wa Matini Chanzi. Mishororo michache ya wimbo huo katika mfano ufuatao inadhihirisha dai hili:

**Mfano 36**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) *Twathiiaga tũkeneete*
*Tũgacooka tũkeneete*
*Rũgeendo rwitũ rũraarĩ rwega*
*Tũgĩthiĩ na tũgĩcooka.* (uk 76)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) *Tulikwenda kwa furaha*
*Tukarudi kwa furaha*
*Safari yetu ilikuwa nzuri*
*Kwenda huko na kurudi.* (uk 70)

Tulionelea kuwa mtafsiri alikuwa na imani kuwa kukosa kutafsiri baadhi ya maneno na badala yake kuyawasilisha kama yalivyo katika MC hakungeathiri mawasiliano yake na hadhira ya MT.

### 4.2 Tasifida kama Kiashiria cha Ukiushi

Senkoro (1982) anajadili tasifida ni tamathali ya usemi inayojihusisha na matumizi ya maneno au nahau ambayo hupunguza ukali au matusi badala ya kutumia neno au nahau yenye ukali au ya kimatusi. Maelezo haya ni muhimu kwa kuwa yameuchangia utafiti huu kwa upande wa dhana. Aidha, yametuongoza kuichunguza tasifida kama matumizi ya

maneno yanayoficha masimango wakati wa mchakato wa kutafsiri.Tunaona kuwa mtafsiri amekiuka baadhi ya maneno na maelezo ya MC kwa kutumia tasifida kupunguza ukali au matusi katika maneno ya MC. Hata hivyo, mtafsiri ametekeleza jukumu la kuwasilisha maana ya ujumbe wa MC kwa kuwasilisha maneno hayo na maelezo hayo kwa njia laini kama katika mifano ifuatayo:

**Mfano 37**

MC (*Ngaahika Ndeenda*)Gĩcaamba: *Angĩ macookaga kanitha <u>magĩthikwo</u>.* (uk 69)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Wengine hurudi kanisani <u>kwa hatima ya mazishi yao</u>. (uk 63)

Tunatambua kosa la uchapishaji au uendelezaji katika neno ‘hatima’ kwa kuwa mtafsiri ameliendeleza kama hitima, la sivyo, amelikiuka kimakusudi. Katika mfano huu, mtafsiri ametumia maneno yenye adabu na heshima kuwasilisha ujumbe husika, la sivyo angeyatafsiri kuwa 'Wengine hurudi kanisani <u>ili kanisa hilo lijishughulishe na mipango ya mazishi yao wakati watakapokufa</u>.' Mtafsiri anafaulu kupunguza ukali wa maneno ya MC kwa kutumia tasifida hii kama namna ya ukiushi. Matumizi mengine ya tasifida kama njia nyingine ya kukiuka maneno yenye ukali au matusi yametokea katika mfano ufuatao:

**Mfano 38**

MC (*Ngaahika Ndeenda*)Kĩgũũnda: *Kwĩĩragwo ũthuri wa gĩtonga <u>ndũnuungaga.</u>*(uk 105)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Watu husema mashuzi ya tajiri <u>hayachukizi</u>. (uk 98).

Katika mfano huu, mtafsiri amekiuka maana msingi ya neno la MC *'ndũnuungaga'* ambalo tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili ni "haunuki" au "hayanuki". Mtafsiri amewakilisha neno hilo kwa neno "hayachukizi" ambalo licha ya kuwasilisha maana dhamiriwa halina ukali kama ule uliopo kwenye neno la MC *"ndũnuungaga".* Ninaafikiana na matumizi ya tasifida hii kama kiashiria cha ukiushi licha ya kuwa tafsiri hiyo imepotosha maana ya neno la MC. Tasifida hii basi imemfaidi mtafsiri na Hadhira Pokezi ya MT ingawa imepotosha maana halisi inayokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi.

Mfano mwingine wa matumizi ya tasifida kama namna ya ukiushi katika tamthilia tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* ni katika mfano ufuatao:

**Mfano 39**

MC (*Ngaahika Ndeenda)* Gicaamba: *Araabutirwo wĩra na* .................... (uk 42)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Aliachishwa kazi na ….................. (uk 40)

Ni dhahiri kuwa kuna tofauti kati ya nahau 'kufutwa kazi' na 'kuachishwa kazi'. Kufutwa kazi ni kupigwa kalamu yaani kufukuzwa kabisa kazini. Kuachishwa kazi kuna maana kwamba mfanya kazi anayehusika anaweza kurudishwa kazini baada ya muda fulani. Maana halisi inayodhamiriwa na waandishi wa MC ni kufutwa kabisa au kupigwa kalamu. Mtafsiri katika mfano huu amepunguza makali ya neno hilo kwa kutumia nahau 'kuachishwa kazi', ambayo si kisawe cha 'kufutwa kazi'. Hii ni tasifida ambayo mtafsiri ameitumia kimakosa kwani pengine kwake yeye hakuona tofauti kati ya 'kufutwa kazi' na 'kuachishwa kazi' almuradi awasilishe au ahawilishe ujumbe wa MC. Mtafsiri amewasilisha maana isiyo sahihi katika tafsiri yake kwa kupunguza makali ya maana inayokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi ya 'kufukuzwa kabisa kazini'. Ukweli ni

kwamba maana ya nahau hii katika MC na MT katika mfano huu si sawa. Hata hivyo, tunaona kuwa mtafsiri amejaribu kuwasilisha habari iliyoko kwenye MC japo kwa kuleta upotoshi fulani ambao haujaathiri dhamira lengwa ya waandishi wa Matini Chanzi ya *Ngaahika Ndeenda.*

### 4.3 Matumizi ya Maneno ya Matini Chanzi bila Kuyatafsiri

Hii ni aina ya ukiushi ambapo mtafsiri huyahamisha maneno ya Matini Chanzi kwenye Matini Tafsiri bila ya kuyatafsiri. Badala ya kuyatafsiri maneno hayo kwa Lugha Pokezi, mtafsiri huyaandika kwa Lugha Chanzi kama yalivyo na kuyaakifisha maneno hayo kama yalivyoakifishwa kwenye Matini Chanzi. Ukiushi wa aina hii aghalabu hujitokeza katika tafsiri ya majina ya vitu (vifaa) vya kiasili vya jamii husika ambavyo havipo katika mazingira ya Hadhira Pokezi, majina ya wahusika au viingizi vya Lugha Chanzi. Katika aina hii ya ukiushi, mtafsiri anakataa kuyatafsiri baadhi ya maneno ya MC na badala yake kuyawakilisha kama yalivyo katika MC. Baadhi ya maneno ambayo hayajatafsiriwa bali yamebaki kama yalivyo katika MC ni majina ya wengi wa wahusika wakiwemo Kĩgũũnda, Wangeci, Gĩcaamba na Kĩoi. Aidha, baadhi ya maitikio ya maamkizi na maneno ya kuonyesha hisia (viingizi) yamewakilishwa katika Matini Tafsiri bila kutafsiriwa. Mifano ifuatayo inadhihirisha aina hii ya ukiushi wa kiubunifu katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*:

**Mfano 40**

MC (*Ngaahika Ndeenda*) Gathoni: *Yĩ-ĩ!*

Gathoni: *Yũũũ!* (uk 23)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gathoni: Yĩĩ–ĩ! (Japo mtafsiri hakuakifisha ifaavyo)

Gathoni: Yũũũũ– ũ! (uk 22)

Katika mfano huu, mtafsiri amewasilisha majibu ya maamkizi bila kutafsiri. Badala yake anaamua kuyaweka majibu hayo ya maamkizi kama yalivyo katika Matini Chanzi. Hata hivyo, majibu ya "Yii – i!" Katika MT ni potoshi kwani mtafsiri hajayaakifisha maamkizi hayo ipaswavyo. Amekiuka matumizi ya alama za mawimbi kwani hazijawekwa juu ya herufi "i" kama zilivyowekwa katika MC. Kwa vile mtafsiri alikuwa ameamua kulihamisha neno husika bila kulitafsiri, basi hangekuwa na budi ila kuliwasilisha kama lilivyo bila ya kubadilisha alama zozote za uakifishaji kama alivyofanya. Mtafsiri angetarajiwa kuliakifisha neno hilo kikamilifu kama "Yĩĩ – ĩ!" Hata hivyo, tunachukulia kuwa isingekuwa kosa la uakifishaji kuwepo, maana ya ujumbe kama kaida imehifadhiwa na mtafsiri na kwa hivyo, ukiushi huu hujazuia mawasiliano mwafaka kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi.

Mwitiko huu wa mwito, ambao mtafsiri ameamua kutoutafsiri umetokea tena katika ukurasa wa 25 wa Matini Tafsiri ambapo mhusika Gathoni anauitikia mwito wa mama yake (Wangeci) kwa 'Yũũũũ– ũ!' na 'Yĩĩĩ– ĩ !' katika MT. Huu ni ukiushi katika tafsiri kwani tungetarajia katika LP ya Kiswahili, Gathoni amwitikie mamake kwa maneno ya Lugha Pokezi ya Kiswahili kama', 'Naam!', 'Eeh !' au 'Bee !' katika MT. Tunaafikiana na mtafsiri Kabugi kuwa ukiushi huu haukuathiri pakubwa maana ya ujumbe dhamiriwa wa MC wala kuathiri maudhui na dhamira ya waandishi wa Matini Chanzi kwa kuwa msomaji anaweza kutambua kuwa huu ni mwitiko kwani unafuatana na mwito wenyewe.

Isitoshe, hisia ya mshangao katika Kiswahili huwasilishwa kwa maneno ya hisia mathalani 'Woooh!' 'Salaaale!' au 'Alhamdulilah!' Hata hivyo, mtafsiri Kabugi alikiuka hili na

kutumia maneno ya mshangao ya LC ya Gĩkũyũ ya *'Aaaa -uuuuuu – u !'* katika ukurasa wa 96 wa MT ambapo mhusika Wangeci anashangazwa na swala la bintiye Gathoni kupachikwa mimba na kuachwa na John Mũhũũni, mwana wa tajiri na mwajiri wao Ahabu Kĩoĩ wa Kanoru.

### 4.4 Ubunifu wa Mtafsiri

Ubunifu ni hali inayotokana na kitendo cha kubuni au kufinyanga jambo fulani akilini. Ryanga (1985) anajadili vigezo vinne vinavyofaa kuzingatiwa kabla ya kukubali kazi za kifasihi zilizotafsiriwa kutoka lugha nyinginezo kuelekea lugha ya Kiswahili. Vigezo hivyo ni ufahamu kamili wa ujumbe asilia na jinsi ya kuuelezea katika Lugha Pokezi, umahiri wa hisi za kisanaa, ujuzi fasaha wa lugha yaani Lugha Chanzi na Lugha Pokezi na ufundi katika mbinu na taratibu za sanaa na somo analolitafsiria au taaluma anayotafsiria.

Sykes katika Picken (1983) anasema kuwa mtafsiri anafaa kuwa na uzoefu wa kujua maisha (utamaduni, lugha, mazingira na miktadha) ya jamii inayotumia Lugha Chanzi au Lugha Asilia. Inatakiwa mtafsiri awe mwenyeji wa Lugha Chanzi, iwe lugha-mama kwake ili awe na umulisi tosha wa kuweza kuitafsiri. Aidha, ni sharti aijue kwa umilisi mkubwa Lugha Pokezi. Isitoshe, mtafsiri anapaswa kujua na kuwa mzoefu wa mada au taaluma husika anayoishughulikia kama vile fasihi, fizikia, uhasibu au uhakiki wa kifasihi la sivyo inatakiwa ashirikiane kwa karibu na mjuzi wa taaluma anayoishughulikia katika tafsiri. Tulikubaliana na Picken kwamba mtafsiri awe mwenye kupenda na kuifurahia taaluma anayoishughulikia bali isiwe kama kwamba anajilazimishia. Hii ni kwa kuwa matini anayoitafsiri si msururu tu wa maneno bali mtiririko wa mawazo halisi ya Mwandishi Asilia wenye lengo madhubuti la kuwasilisha ujumbe. Kutokana na uchunguzi wetu, ni dhahiri kuwa mtafsiri Kabugi amekithi mahitaji yote haya na kwa hivyo alikuwa na umilisi

na ufasaha wa kutosha wa kudhibiti uwasilishaji wa ujumbe wa MC kwenye MT. Licha ya yote hayo, ameongeza ubunifu wake kama katika mfano ufuatao ili kuhawilisha maana ya ujumbe wa Matini Chanzi kwenye Matini Tafsiri.

**Mfano 41**

MC (*Ngaahika Ndeenda)* Njooki: *Naawe ingĩnyiita Kĩoi ũcio ũraaganwo*
*Na maya manyiitaga tĩĩri aamenya*. (uk 109)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Njooki: Nikimshika huyo Kĩoi anayesifiwa
Kwa hii mikono yangu ivurugayo udongo
Atakiona kilichomtoa kanga manyoya. (uk 102)

Ni maoni kuwa mtafsiri ametumia ubunifu kwa kutoa ufafanuzi wa maneno ya MC. Kwa mfano, ametumia msemo “Atakiona kilichomtoa kanga manyoya” badala ya kusema “Atanitambua”. Kwa kufanya hivi, anawezesha mawasiliano mwafaka yaweko kati ya MT na HP. Kama mtafsiri angekuwa mwaminifu kikamilifu kwa MC, angetoa tafsiri ambayo haingewasilisha maana ya ujumbe dhamiriwa. Isingekuwa ukiushi wa mtafsiri uliomfanya kuzua ubunifu huu, angetoa tafsiri isiyo na mantiki au mashiko kama ifuatayo:

* Njooki: Nawe nikimshika huyo Kĩoi anayesifiwa
Na haya yanayoshika udongo atanijua.

Tumeona kuwa umbuji huu wa mtafsiri umemsaidia kuwasilisha maana ya ujumbe wa MC kwenye MT. Mfano mwingine wa matumizi ya ubunifu wa mwandishi wa Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* ni kama huu ufuatao:

**Mfano 42**

MC (*Ngaahika Ndeenda)* Herina: *Muume mũtondo–inĩ wa meehia*. (uk 55)

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Helina: Mtoke katika bahari ya dhambi. (uk 52)

Maoni yangu kutokana na mfano huu ni kuwa mtafsiri ametumia ubunifu wake kwa kutumia maneno tofauti na yale yaliyo katika Matini Chanzi kuwasilisha ujumbe kikamilifu. Katika mfano huu, maana halisi ya neno *'mũtondo-inĩ '* ni 'matopeni' au 'topeni'. Mtafsiri Kabugi anaamua kutumia neno 'bahari ya dhambi' kwa kutambua kuwa mazingira na utamaduni wa Lugha Pokezi ya Kiswahili unaambatana zaidi na bahari kuliko tope au matope. Ninakubaliana na uteuzi huu wa neno kwa kuwa ndilo neno linalokidhi kuwakilisha kwa usahihi wazo linalodhamiriwa na Waandishi Asilia. Huu ni ubunifu makusudi ambao unamfanya mtafsiri kuwasilisha ujumbe unaodhamiriwa na waandishi wa Matini Chanzi. Mtazamo kuhusu maana ya neno fulani unaweza wakati mwingine kutofautiana baina ya jamii mbili tofauti. Aidha, mtafsiri na mtafsiriwa wanaweza kuwa na mtazamo tofauti kuhusu neno. Mtazamo wa watafsiriwa (HP) na ule wa hadhira ya Matini Chanzi kuhusu maneno 'tope' na 'bahari' ni kinzani. Mtafsiri ameamua kutumia neno 'bahari' kwani kwa hadhira ya Kiswahili, kupotelea au kutokomea baharini kuna 'uzito' kuliko kutokomea au kupotelea topeni au matopeni. Kwa kutumia ubunifu huu, mtafsiri amefaulu kuwasilisha ujumbe sahihi na wa kweli kwa wafasiriwa ama watafsiriwa.

**4.5 Uziada kama Kiashiria cha Ukiushi**

Uziada hi hali ya mtafsiri kuongeza maneno au maelezo kwa nia ya kufafanua ujumbe uliokusudiwa na Mwandishi Asilia. Katika ukurasa wa100 na ukurasa wa 101 wa Matini Tafsiri, mtafsiri amekiuka kutoka kwa MC kwa kuongezea maneno ya ziada ambayo hayako katika MC. Hakukuwa na maneno hayo katika MC, kwa hivyo, hadhira ya Matini Tafsiri haitarajii maneno hayo kujitokeza. Maneno yaliyoongezwa katika ukurasa wa 100 wa MT:

**Mfano 43**

MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Gĩcaamba: Kwa kuwa kamba hukatikia pabovu. (uk 100)

Mtafsiri ameongeza maneno au maelezo ya methali hii kwa nia ya kufafanua maana ya ujumbe kuwa 'wanawake hupigwa na waume zao kwa ajili ya udhaifu wao'. Kupitia ukiushi huu wa kuongeza maneno ya ziada katika matini yake, mtafsiri anafanikisha na hata kuboresha mawasiliano kati yake na Hadhira Pokezi. Aidha, mtafsiri ameongeza neno 'tu' katika ukurasa wa 101 wa Matini Tafsiri japo halikuweko katika Matini Chanzi. Nia ya mtafsiri katika uziada huu ilikuwa ni kusisitiza na kutilia mkazo maana ya ujumbe uliodhamiriwa. Mfano huo umejitokeza ifuatavyo:

**Mfano 44**

MC (*Ngaahika Ndeenda)* Njooki: *Nĩ agaacoka!* (uk 109)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Njooki: Atarudi tu! (uk 101)

Mtafsiri Kabugi anataka kutilia mkazo matamshi ya Njooki kwa rafikiye Wangeci kwa kuonyesha kuwa ni ombi lake Njooki kuwa Gathoni, mtoto wa rafikiye Wangeci atarejea nyumbani siku moja. Gathoni alitoroka nyumbani alipokosana na babake baada yake kutungwa mimba na John Mũhũũni, mwana wa tajiri Kĩoi. Isitoshe, tunatambua matumizi ya uziada kama namna nyingine ya ukiushi katika Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* katika mfano ufuatao:

**Mfano 45**

MC (*Ngaahika Ndeenda)* Kĩgũũnda: *O na mĩaka mũgwanja ndĩathirire!* (uk 32)
MT (*Nitaolewa Nikipenda*) Kĩgũũnda: Oh, hata miaka saba haikuwa imepita! (uk 31)

Tunatambua kuwa matumizi ya neno 'Oh' katika MT ni maelezo ya ziada. Mtafsiri ameongeza maana ambayo haikuwa katika MC. Hata bila neno hilo, ujumbe kwenye MC ungekuwa umehawilishwa kwenye Matini Tafsiri. Huu ni ukiushi wa kanuni za kaida za uandishi wa tafsiri kwa kuongeza habari ya ziada. Kwa kutumia mbinu hii ya kuongeza maneno na maelezo ya ziada katika tafsiri, mtafsiri amefanikiwa kuwasilisha maana ya ujumbe wa Matini Chanzi kwenye Matini Tafsiri.Ukiushi huu wa kuongeza neno ‘Oh’katika Matini Tafsiri hujaathiri maana inayodhamiriwa na Matini Chanzi.

**4.6 Uaminifu wa Matini Tafsiri**

Uaminifu ni istilahi inayotumiwa katika tafsiri kurejelea utimilifu wa Matini Tafsiri katika kuwasilisha ujumbe ulioko katika Matini Chanzi (Shitemi (1997). Ni hali ya Matini Tafsiri kuwa na uwezo wa kuwasilisha kwa ufasaha na ukweli iwezekanavyo ujumbe ulioko kwenye Matini Chanzi. Licha ya kuweko aina mbalimbali za ukiushi katika Matini Tafsiri tuliyoishughikia, mtafsiri amedhihirisha uaminifu wa MT kwa MC. Haya yamethibitika kutokana na jinsi mtafsiri amewakilisha mpangilio wa matini, maudhui, wahusika, matumizi ya lugha na masimulizi katika matini yake. Yafuatayo ni maelezo ya kila mojawapo ya mambo haya: Kwanza, mtafsiri ameipanga matini yake kutoka mwanzo hadi mwisho kama vile waandishi wa Matini Chanzi walivyofanya. Tunadai hivi kwani kila matini ina vitendo vitatu. Kitendo cha kwanza kina sehemu moja. Kitendo cha pili kina sehemu mbili na kitendo cha tatu kina sehemu tatu. Maana inayoletwa na yote yanayotendwa na kuzungumzwa katika kila kitendo au sehemu katika MC inaleta athari sawa inayolandana na yote yaliyomo katika MT.

Pili, maudhui yote yanayozungumziwa katika MC kutoka mwanzo hadi mwisho yamewakilishwa katika MT. Athari inayosababishwa na maudhui katika Matini Chanzi ni sawa na ile inayotokea katika Matini Tafsiri. Mtafsiri amefanikisha hili kwa kuitumia maana kama kaida. Kwa hivyo, katika uwasilishaji wa maudhui yaliyoko katika MC, tunaona kuwa mtafsiri hajaihadaa, kuikosea au kuipotosha Hadhira Pokezi ya MT. Tatu, mtafsiri amewaumba wahusika wake kwa njia sawa na jinsi waandishi wa Matini Chanzi walivyofanya. Isitoshe, mtafsiri amewapa wahusika takribani wote majina yaleyale waliyopewa katika Matini Chanzi. Ni wahusika wachache tu ambao majina yao yameendelezwa tofauti na ilivyo katika MC kutokana na kanuni za uandishi za Lugha Pokezi ambazo zinahitilafiana na kanuni za uandishi za Lugha Chanzi. Wahusika katika MT wanawakilisha hulka, sifa na nafsi zilezile zilizo na wahusika hao katika MC.

Nne, lugha iliyotumiwa katika Matini Tafsiri hasa tamathali za usemi ndiyo ile ile iliyowakilishwa katika Matini Chanzi. Hata hivyo, mtafsiri ametumia ubunifu katika kuziwasilisha baadhi ya tamathali katika matini yake kwa sababu tamathali zingine kwa mfano methali na nahau hazitafsiriki kwa urahisi. Pale ambapo ubunifu haukufaa, mtafsiri amekiuka maana huku akizingatia utamaduni, mazingira na muundo wa lugha ya Matini Tafsiri yaani Lugha Pokezi.

**4.7 Hitimisho**

Katika sura hii, tumefafanua uhusiano uliopo kati ya dhana ya umbuji na dhana ya ukiushi. Tumechunguza na kujadili umbuji ulivyotumiwa na mtafsiri kama kiashiria cha ukiushi katika juhudi zake za kuhamisha ujumbe wa MC (*Ngaahika Ndeenda)* kwenye MT (*Nitaolewa Nikipenda)*. Tumeshughulikia aina nne za umbuji zilizotumiwa na mtafsiri Kabugi kwa kuzichambua na kuzitolea mifano katika matini zote (MC na MT) na

kufafanua jinsi ukiushi unavyojitokeza. Aina hizi nne za umbuji zimehusisha matumizi ya tasifida, uhamishaji wa moja kwa moja wa baadhi ya maneno ya Lugha Chanzi, ubunifu wa mtafsiri unaochochewa na umilisi dhabiti wa Lugha Chanzi na Lugha Pokezi na vilevile uziada. Licha ya changamoto mbalimbali anazokumbana nazo mtafsiri wa Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda*, tumeonelea kuwa alifaulu kwa kiasi kikubwa kuwasilisha maana na ujumbe wa Matini Chanzi kwenye Matini Tafsiri.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii imejaribu kuonyesha jinsi mtafsiri Clement Kabugi anavyokiuka baadhi ya kaida za uandishi alipokuwa akitafsiri *Ngaahika Ndeenda* hadi *Nitaolewa Nikipenda*. Ukiushi huu umebainika tunapoichunguza MT na kuilinganisha na MC. Tumetambua kuwa mtafsiri kwa kusudi, kwa kulazimika au kwa ubunifu wake amekiuka kaida za uandishi na hivyo kuandika maneno, vishazi na viakifishi ambavyo si visawe kamili vya virejelewa katika Matini Chanzi. Maana ya ujumbe imetumiwa kama kaida kuonyesha kuwa athari ya vipashio vyenye ukiushi inabaki kuwa sawa katika Matini Tafsiri na Matini Chanzi.

Katika sura ya kwanza, tumechunguza usuli na suala la utafiti. Tumeonyesha historia ya taaluma ya tafsiri. Aidha tumechunguza na kuthibitisha chimbuko la Tamthilia Tafsiri ya *Ngaahika Ndeenda*. Tumetambua kuwa tamthilia hii haikuibuka kama kazi ya ubunifu wa mtu binafsi au waandishi wawili pekee bali ilikuwa kazi ya jumuiya nzima ya kijiji cha Kamĩrĩthũ, maeneo ya Limuru. Hata hivyo, Ngũgĩ wa Thiong'o na Ngũgĩ wa Mĩriĩ ndio waliokuwa wasomi na kwa hiyo wakatwikwa jukumu la kuiandika tamthilia hii. Tumeweka bayana suala la utafiti na kuonyesha kuwa vipengele vilivyolengwa kuchunguzwa katika utafiti huu ni maneno, sentensi, vishazi, aya na viakifishi ili kuona jinsi vinavyokiukwa na mtafsiri. Aidha, tumechunguza sababu ya ukiushi kujitokeza katika Matini Tafsiri.

Katika sura ya pili, tumechunguza dhana na nadharia ya tafsiri, dhana ya ukiushi katika tafsiri na sababu mbalimbali zinazopelekea kujitokeza kwa ukiushi katika tafsiri. Baadhi ya sababu hizi ni; ubunifu wa mtafsiri, umilisi wake, uzoefu wake, hadhira anayoilenga na tofauti za kiisimu kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi. Katika sura ya tatu, tumeelezea kwa kifupi kisa cha tamthilia tuliyoishughulikia ya *Nitaolewa Nikipenda*. Tumejadili muundo wa Matini Chanzi na Matini Tafsiri. Tumeshughulikia aina mbalimbali za ukiushi zilizojitokeza katika Matini Tafsiri hususan ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kisintaksia na ukiushi wa kisemantiki. Tumefafanua maana ya ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kisintaksia, na ukiushi wa kisemantiki. Tumedondoa mifano kadha wa kadha ya ukiushi huo katika MT kwa kulinganisha na ilivyo katika MC. Aidha, tumeelezea sababu za ukiushi wenyewe kujitokeza.

Katika sura ya nne, tumeutalii uhusiano ulioko kati ya umbuji na ukiushi. Tumechunguza na kuelezea jinsi mtafsiri anavyotumia umbuji wake kukiuka maneno, nahau, vishazi na viakifishi vya MC katika mchakato mzima wa kuhawilisha ujumbe wa MC kwenye MT. Katika maelezo na uchanganuzi huu, tumetoa mifano kadhaa ya matumizi ya aina hizi za umbuji ambazo ni; matumizi ya tasifida kama kiashiria cha ukiushi, uhawilishaji wa maneno bila kuyatafsiri, ubunifu wa mtafsiri na uziada yaani maelezo ya ziada. Aidha, tumejadili jinsi ukiushi huu wa kiumbuji unavyojitokeza na vilevile kueleza athari ya maana ya ujumbe kwa Hadhira Pokezi ya Matini Tafsiri.

## 5.1 Mchango wa Utafiti

Katika sehemu hii, tasnifu imejadili mchango wa utafiti huu katika uwanda wa tafsiri.

### 5.1.1 Ukiushi katika Tafsiri

Utafiti huu umethibitisha kuweko kwa ukiushi katika Matini Tafsiri. Sababu mbalimbali zinizopelekea kujitokeza kwa ukiushi kumejadiliwa. Aidha, ubunifu kama kiashiria cha ukiushi umetathminiwa ili kuona jinsi mtafsiri huutumia ukiushi kukabiliana na changamoto za namna ya kutafsiri dhana ama neno fulani. Utafiti huu umechangia katika taaluma ya tafsiri kwa kuthibitisha kuweko kwa ukiushi na kufafanua ukiushi huo ulivyojitokeza. Hii ni muhimu ikizingatiwa kuwa kazi tunayoishughulikia ni tafsiri kutoka kwa lugha moja ya Kiafrika hadi nyingine yaani kutoka Gĩkũyũ hadi Kiswahili. Mifano arubaini na tano ya ukiushi uliopo katika Matini Tafsiri imechambuliwa na kufafanuliwa. Ingawa utafiti umethibitisha kuwa ukiushi umejitokeza katika Tamthilia Tafsiri, mtafsiri amefaulu kuwasiliana na hadhira yake kwa njia mwafaka. Hii ni kwa sababu mtafsiri amefaulu kuwasilisha maudhui na dhamira ya waandishi wa Matini Chanzi.

### 5.1.2 Aina za Ukiushi

Utafiti huu umechanganua aina tatu za ukiushi. Aina hizi za ukiushi ambazo zimejitokeza katika Matini Tafsiri ni ukiushi wa kifonolojia, wa kisintaksia na wa kisemantiki. Utafiti umechambua kila mojawapo wa hizi aina za ukiushi na kutoa mifano kudhihirisha dai hili. Mifano hii imejadiliwa na kufafanuliwa kwa kusudi la kuonyesha namna ukiushi umejitokeza na vile vile athari yake kwa Hadhira Pokezi.

Japo baadhi ya ukiushi umeojitokeza katika MT umekusudiwa, ukiushi mwingine umetokea kama makosa ya uchapishaji. Tunaonelea kuwa kuwepo kwa ukiushi katika MT hakujaathiri pakubwa uelewekaji wa ujumbe wa MT ambao tumeona kuwa unalingana na ule wa Matini Chanzi. Ukiushi unaojitokeza katika Matini Tafsiri ni wa aina mbalimbali. Hata hivyo, ukiushi wa kisemantiki na ukiushi wa kisintaksia umetamalaki kuliko ukiushi

wa aina nyingine yoyote mathalani matumizi ya tasifida na uhamishaji wa maneno ya MC kwenye MT. Aidha, ukiushi umetokea katika kurasa nyingi za MT japo si kurasa zote. Ukiushi huu umemwezesha mtafsiri kuwasilisha maana ya ujumbe wa Matini Chanzi kwenye Matini Tafsiri kwa njia mwafaka. Hata hivyo, ukiushi mwingine umepotosha maana halisi ya baadhi ya maneno kama yanavyodhamiriwa na waandishi wa Matini Chanzi kwa mfano kutafsiri neno 'ndala' (viatu) kama ‘magurudumu’ katika ukurasa wa 11 wa matini zote mbili.

### 5.1.3 Umbuji kama Kiashiria cha Ukiushi

Mchango mwingine ambao utafiti huu umetoa katika uwanda wa tafsiri ni kuthibitisha kuwa umbuji huweza kujitokeza kama njia ya kukiuka kaida fulani za uandishi. Katika aina hii ya ukiushi, mtafsiri hutumia njia tofauti kuwasilisha ujumbe wa Matini Chanzi kwenye Matini Tafsiri. Baadhi ya njia hizi ni matumizi ya tasifida, uhawilishaji wa maneno ya Matini Chanzi bila kuyatafsiri, ubunifu na uziada. Licha ya yote haya utafiti umebainisha kuwa mtafsiri amezuingatia uaminifu wake kwa Matini Chanzi.

Tumeona kuwa mtafsiri Kabugi amepanua mipaka ya yale yanayokusudiwa na waandishi wa MC kwa kuongeza maelezo au maneno ya ziada ili kukwepa miktadha ya utamaduni wa Hadhira Asilia. Anapoukosa msamiati unaofaa, anautohoa kwa kuupatia tahajia ya Lugha Pokezi kwa mfano 'trekta' (uk 47). Pale ambapo utohozi haufai, ametoa maelezo ya msamiati huo lakini kwa kuhakikisha kuwa maana ya ujumbe dhamiriwa imebaki kuwa sawa katika matini yake. Tunaona kuwa mtafsiri amepunguza viingizi katika kurasa mbili za mwisho katika MT. Haijaeleweka ni kwa nini amefanya hivyo. Ni maoni yangu kuwa upunguzwaji huu umeathiri maana ya ujumbe unaokusudiwa kuifikia Hadhira Pokezi ya MT. Tunadai hivi kwa kuwa kila kiakifishi kinachotumiwa katika fasihi tafsiri kina

uamilifu wake ulio tofauti na kiakifishi kingine chochote. Licha ya changamoto mbali mbali ambazo mtafsiri wa Tamthilia Tafsiri ya *Nitaolewa Nikipenda* anakumbana nazo, tunaonelea kuwa amefaulu kwa kiasi kikubwa kuwasilisha maana na ujumbe wa Matini Chanzi kwenye Matini Tafsiri.

Tumeshughulikia muhtasari wa tasnifu kwa kueleza yote yaliyochunguzwa na kujadiliwa kutoka sura ya kwanza hadi sura ya tano. Tumefafanua mchango wa utafiti huu katika taaluma ya tafsiri. Katika utafiti huu tumethibitisha kuwa ukiushi katika tafsiri ulijitokeza kutokana na tofauti za kiisimu, kitamaduni na kimazingira kati ya Lugha Chanzi na Lugha Pokezi. Aidha, tumetambua katika sura hii kuwa ukiushi mwingine umetumiwa kimakusudi na mtafsiri kama njia ya kuendeleza ubunifu.

Tumetambua kuwa ukiushi wa mtafsiri umejitokeza kwa namna mbalimbali mathalani ukiushi wa kifonolojia, wa kisintaksia na ukiushi wa kisemantiki. Tumethibitisha kuwa ukiushi umejitokeza katika baadhi ya sehemu za tamthilia wala si katika tamthilia nzima. Tumethibitisha vilevile kuwa ukiushi wa mtafsiri umeifaidi Hadhira Lengwa kwa kuuweka bayana ujumbe uliokusudiwa. Pamoja na hayo, ukiushi wa mtafsiri umemwezesha kuuwasilisha ujumbe wa Matini Chanzi kwa uhakika na uhalisi zaidi licha ya kwamba ukiushi huo umebadilisha maana ya baadhi ya maneno ya Matini Chanzi.

Imebainika katika sura hii kuwa ukiushi wa mtafsiri haujaathiri pakubwa maana ya ujumbe unaokusudiwa na waandishi wa Matini Chanzi kwa kuwa maudhui na dhamira katika matini zote mbili yamelingana. Kutokana na changamoto zilizomkabili katika mchakato mzima wa kuhawilisha ujumbe wa MC kwenye MT, mtafsiri atumia umbuji wake kwa

kuongeza na wakati mwingine kupunguza baadhi ya vipengele katika matini aliyokuwa akiishughulikia.

## 5.2 Mapendekezo

Kutokana na yale tuliyoyaona wakati wa uandishi wa tasnifu hii, tunapendekeza kuwa matini zilizohakikiwa kwa kukosolewa zichunguzwe upya. Uchunguzi huu uangalie ikiwa kilichokuwa kimeitwa ukiushi, makosa, upotovu, kasoro au udhaifu ni aina ya ubunifu uliodhibitiwa na utamaduni na mazingira ya Hadhira Pokezi. Tasnifu hii inapendekeza kuwa MT ziangaliwe kama kazi maalumu na toshelevu. Inawezekana kuwa ukiushi mwingine umetumiwa kimakusudi ili kuboresha mawasiliano kati ya Matini Tafsiri na Hadhira Pokezi. Hali hii itazifanya matini hizo kuwa na sura mpya kwa kuziona kama matini zilizoutoa mchango muhimu katika fasihi tafsiri. Aidha, tunapendekeza kuwa MT tuliyoichunguza ifanyiwe uchunguzi upya ili kuona ni kwa nini kulitokea makosa mengi ya tahajia na ya uchapishaji, kwa nini viingizi vingi vimekiukwa katika baadhi ya kurasa na kwa nini mtafsiri hakuyatafsiri majina ya wahusika na baadhi ya maneno ya Matini Chanzi.

Ni mapendekezo ya tasnifu hii kuwa iwapo ukiushi utajitokeza katika tafsiri, tahadhari ichukuliwe na mtafsiri ili ukiushi uliopo katika tafsiri usipotoshe maana iliyokusudiwa katika Matini Chanzi. Kwa kuwa ukiushi katika tafsiri hauwezi kuepukika kabisa, tunapendekeza kuwa mtafsiri aitilie maanani Hadhira Pokezi ya Matini Tafsiri kuhakikisha kuwa ukiushi huo hutaipotosha hadhira hiyo kwa kuthibitisha kuwa mawasiliano mwafaka yamepatikana kati ya MT na Hadhira Pokezi. Ni mapendekezo ya tasnifu hii kuwa tafsiri za kifasihi zitambuliwe kama sanaa muhimu inayoweza kuimarishwa zaidi. Tafsiri za kifasihi zinafaa zitafitiwe na kuhakikiwa katika miktadha ya uhakiki wowote ule wa

kifasihi, sawa na fasihi asilia ya lugha asilia. Ni mapendekezo ya tasnifu hii pia kuwa mapitio ya mara kwa mara yafanyiwe MT na MA au MC ili makosa ya kimaksudi au kiukiushi yaliyojitokeza yasahihishwe katika matoleo ya baadaye.

Kutokana na makosa ya tahajia na ya uchapishaji yaliyojitokeza kwa wingi, kwa mfano katika ukurasa wa 12 na 23 wa Matini Tafsiri, tunapendekeza kuwa katika kila toleo jipya la kazi ya tafsiri, makosa yaliyotokea katika matoleo yaliyotangulia yasahihishwe au yarekebishwe. Kila toleo jipya liondolewe makosa ya awali kwani kutofanya hivyo kutaendelea kushusha hadhi na kudumaza taaluma ya tafsiri na pia fasihi tafsiri kwa jumla.

Tasnifu hii inapendekeza vilevile kuwa haki ya mtafsiri ambayo kwa sasa imevizwa, itambuliwe kwa kumpa uhuru kukiendeleza kipawa chake na kwa kuiona kazi yake kama matini yenye sura ya kipekee. Inafaa mtafsiri atambuliwe na kupewa haki karibu sawa na Mwandishi Asilia kwa mfano kwa kuhusisha vitabu vya tafsiri katika mitala ya elimu ya fasihi shuleni. Hali hii itawapa motisha wasomi wenye ujuzi wa taaluma ya tafsiri ili waanze kutoa michango yao ambayo sasa hivi imedumazwa. Aidha, tasnifu hii inapendekeza kuwa ikiwezekana, mtafsiri anayeazimia kuitafsiri kazi asilia au fasihi tafsiri awasiliane na mwandishi au mtafsiri wa kazi hiyo aliye hai hasa kabla ya kukiuka chochote au kuongeza lolote la ziada. Hili litamjuza mtafsiri kiini cha Matini Chanzi au Matini Asilia kabla hajaanza kuishughulikia tafsiri husika. Mawasiliano haya yatamwezesha mtafsiri kuepuka udhaifu au kasoro katika matini yake ya mwisho bila yeye kutarajia. Mwisho, tumeona kuwa uchunguzi wa ukiushi katika tafsiri baina ya MC na MT tuliyoshughulikia ulifaulu. Haya yamedhihirika kutokana na mifano mbalimbali iliyotolewa kutoka matini zote mbili, kuilinganisha mifano hiyo na kutolewa kwa ufafanuzi wa kila mojawapo ya

mifano hiyo. Huu ni ushahidi kuwa ukiushi umejitokeza mtafsiri alipokuwa akiitafsiri Matini Chanzi kuelekea Matini Tafsiri.

**MAREJELEO**

Asher, R. E. & Simpson, J. M. Y. (1994). *The Encyclopaedia of Language and Linguistics*, Oxford: Pergamon Press Ltd.

Baker, M. (1992). In *Other Words*: *A Course Book on Translation*, London: Routeledge.

Bakhresa, S. K. (1992). *Kamusi ya Maana na Matumizi*, East Africa: Oxford University Press.

Batibo, H. M. (1989). *"Usahihi na Upotovu Katika Tafsiri za Kiswahili."* Katika (Makala za Kongamano la Kimataifa Kuhusu Matatizo ya Tafsiri Barani Afrika), Dar-es-Salaam: TUKI.

Benjamin, W. (1979). *TheTask of the Translator*. In Arendt H. (ed.) Illustrations. London: Fontana.

Cartford, J. C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*, London: Oxford University Press.

Cook, D. (1977). *African Literature, A critical* View, London: Longman Group Ltd.

Cotterell, P. & Turner M. (1989). *Linguistics and Biblical Interpretation*, London: Intervarsity Press.

Crother, J. (1999). *Advanced Learners Encyclopedic*, London: Oxford University Press.

Crystal, D. (1992). *Encyclopaedia of Language, Dictionary of Language and Linguistics, Oxford: Blackwell Publishers.*

Fawcett, P. (1964). *Conflict, Decision and Dissonance*. Stanford, CA: Stanford University Press.

________(1997). *Translation and Language: Linguistic Theories Explained*, Manchester: St. Jerome Publishing.

Gibbe, A. G. (1990). Jarida la Kiswahili (TUKI), Dar-es-Salaam: Education Services Centre Limited.

Gui, G. N. (1969). *Das Wesen des Ubersetzens ist Kreativ*. In: Babel 1945, pp 41, 4,129-139.

Hornby, A. S. (1990). *Oxford Advanced Learner's Dictionary*, Oxford: Oxford University Press.

Huddleston, S. R. (1976). *Defamilirization in Language & Literature*. London: Syracuse University Press.

Igendia, N. M. (2003). 'Uchanganuzi wa Mtindo katika Tafsiri za *"The Government Inspector"* na "*Mkaguzi Mkuu wa Serikali*"' Eldoret: Moi University (Unpublished M. Phil Thesis).

Johnson, F. (1935). *Kamusi ya Kiswahili*; *Kitabu cha Maneno ya Kiswahili*, Nairobi: Oxford University Press.

__________(1939). *A Standard Swahili-English Dictionary*, Dar-es-Salaam: Oxford University Press.

_________ (1939). *A Standard English-Swahili Dictionary*, Dar-es-Salaam: Oxfod University Press.

Jumpelt, R. W. (1961). *Die Aufagbe des übersetzung naturwissenschaftlicher und technisliteratur*, Berlin: Langeschidt.

Kagwa, F. & Waihiga, G. (2011). *Kamusi Fafanuzi ya Misemo na Nahau*, Nairobi: Printwell Industries Limited.

Kiango, C. (1995). *Uundaji wa Msamiati Mpya Katika Kiswahili*, Katika (Kioo cha Lugha) Vol 1 no. 1 pp 46 – 54.

Killam, D. & Rowe, R. (2000). *The Companion to African Literatures*, Indiana: University Press, Bloomington.

Kĩmani, M. N. (2010). *Mũciĩ ni Mũciĩ*, Nairobi: Nsemia Incorporated Publishers.

Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Usemi*, Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Larson, M. L. (1983). *Meaning-Based Translation*: *A Guide To Cross-LanguageEquivalence* Laham: University Presses of America.

Lawson, V. (1982). *Practical Experience of Machine Translation*, Amsterdam: North Holland Publishing Company.

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*, London: Longman Group UK Ltd.

Massamba, D. P. B. (1985). Jarida la Kiswahili, Dar-es-Salaam: TUKI.

Mathews P. H. (1997). *The Concise Oxford Dictionary of Linguistics*, New York: Oxford University Press.

Mbaabu, I. (1978). *Methali, Vitendawili na Mashairi ya Kimeru*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.

__________(1985). *New Horizons in Kiswahili: A synthesis in Development*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mkota, A. (2010). *Kamusi ya Methal*i; *Maana na Matumizi*, Nairobi: Printing Services Limited.

Mkota, A. & Sakara, F. (2011). *Kamusi ya Semi*, Nairobi: Printing Services Limited.

Mohamed, A. M. (2009). *Comprehensive Swahili-English Dictionary,* Dar-es-salaam: East African Educational Publishers.

Mwansoko, H. J. M. (1991). *Mitindo YaKiswahili Sanifu*, Dar-es-Salaam: Dar-es-salaam University Press.

____________ (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri,* Dar-es-Salaam: TUKI.

____________(1995). *Tahakiki na Uchapishaji wa Kamusi,* Dar-es-salaam: TUKI.

Newmark, P. (1981, 1982). *Approaches to Translation,* Oxford: Pergamon Press, UK.

___________(1988). *A Textbook of Translation,* London: Prentice Hall International, UK.

___________(1991). *About Translation*, Clevedon: Multilingual Matters Limited.

Ngũgĩ wa Thiong'o & Ngũgĩ wa Mĩriĩ (1980). *Ngaahika Ndeenda,* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

______ (1982). *Nitaolewa Nikipenda*. (Translated by Clement Kabugi), Nairobi: East African Educational Publishers.

_____(1982). *I Will Marry When I Want,* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Ngugĩ wa Thiong'o, (1980). *Caitani Mũtharaba-inĩ,* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Nida, E. A. (1964). *Towards a Science of Translation*, Leiden: E.J. Brill.

_________ (1982). *Principles of Translation as Exemplified by Bible Translation*: *OnTranslation Imitation and Parody*. Leiden E.J. Brill.

Ogechi, N. O. & Shitemi, N. L. (2008). *Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lughaza Kiafrika*, Moi University Press, Moi University.

Ohly, R. (1977). *Swahili Studies*: *A Supplement to Kiswahili*, Jarida la TUKI, Dar-es-Salaam: Printpak Limited.

Okot P'Bitek (1986*). Artist, the Ruler*. *Essays on Art Culture and Values*, Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Picken, C. (1983). *The Translators Handbook*, London: Aslib. The Association for Information Management.

Reiss, K. (1971). *Möglichkeiten und Grenzen der Übersetzungskritik,* Munich: Hueber.

Robinson, D. (1997). *Becoming A Translator*, New York: Routledge.

Ruhumbika, G. (1983), "Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili." Makala kwenye Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam: (TUKI).

Senkoro, F. E. M. K. (1982) *Fasihi*. Dar es salaam: Press and Publicity Centre.

Shakespeare, W. (1986). *The Merchant of Venice*, Oxford, UK: Macmillan Publishers Limited.

------------- (1969) *Mabepari wa Venisi* (Translated into Kiswahili by Julius Nyerere), Dar-es-Salaam: Oxford University Press.

Shitemi, N. L. (1997). '*Uaminifu Katika Tafsiri, Uhakiki wa Tafsiri za Ushairi wa Jadi wa Kiswahili*.' Moi University (Unpublished D. Phil Thesis).

Sicherman, C. (1989). *Ngũgĩ wa Thiong'o, A Bibliography of Primary and SecondarySources (1957- 1987),* England: Hans Zell Publishers.

Snell– Hornby, M. (1988). *Translation Studies, An Intergrated Approach*. Amsterdam: John Benjamins.

Snell, B. M. (1979). *Translating and Computer*, Amsterdam: North Holland Publishing Company.

Stratton, F. (1994). *Contemporary African Literature and thePolitics of Gender*, London: Routledge.

Taylor J. R. (1995). *Linguistic Categorization, New York:* Oxford University Press.

TUKI (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi: Oxford University Press.

TUKI (1985). *Jarida la Kiswahili*, Vitabu Vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili na Ryanga S.L. Dar-es-Salaam: TUKI.

__________ (2000). *English-Swahili Dictionary* / *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*, Mauritius: Book Printing Services Ltd.

Venuti, L. (1992). *Rethinking Translation*; *Discourse, Subjectivity, Ideology*, London: Routledge & Kegan Paul.

Vinay, J. P. & Darbelnet, J. (1995). *Comparative Styslistics of French and English, A Methodology of Translation*, Amsterdam: John Benjamins.

Wamitila, K. W. & Kyalo, F. (2002). *English-Swahili Dictionary*, Nairobi: English Press.

Wilkinson, J. (1992). *Talking with African Writers*, New Hampshire, Portsmouth: Heinemann Educational Books.

Wilss, W. (1982). *The Science of Translation*; *Problems and Methods*, Tubige: Narr; Tubige.

Zell, H. M., Bundy, C. & Coulon, V. (1983). *A New Reader's Guide to African Literatur*e, London: Heinemann Educational Books Ltd.

## KIAMBATISHO

Baadhi ya data ya Utafiti huu:

Gĩkũyũ (Matini Chanzi)Kiswahili (Matini Tafsiri)

| ***Ngaahika Ndeenda*** | ***Nitaolewa Nikipenda*** |
|---|---|
| *Gwa Kĩgũũnda Mũciĩ.*(uk 11) | *Nyumbani kwa Kĩgũũnda.*(uk 11) |
| Mũtongoria: ....*Arĩa matarĩ wako kana cieya.* (uk 15) | Kiongozi: …..Wasio na pa kujenga au kikata. (uk 15) |
| Kĩgũũnda: .....*nĩ ũhoro urĩa.* (uk 88) | Kĩgũũnda: ….kwa sababu ya ile habari (uk 82) |
| Wangeci :*……….Nĩ kĩ gĩtũmaga ũmĩrore ũguo* . *Ta ĩrĩ ya ĩka ngiri igana?* (uk 11) | Wangeci:…Kwa nini unaitazamatazama kwa furaha nyingi namna hiyo Kama kwamba ni ya ekari elfu moja? (uk 11) |
| Mũkũi: *Nĩ aagiria twake kanitha........* (uk 16) | Kiongozi:Hutuzuia kujenga kanisa.... (uk 16) |
| Kĩgũũnda: *Ngwendaga kũmenya kana no ũtuonere mbeeca.* (uk 91) | Kĩgũũnda: Ningetaka kujua kama unaweza kutukopesha pesa. (uk 84) |
| Wangeci : *Taitondii ĩyo ũmĩũragia ndũũ? Nĩ kĩĩ gĩtũmaga ũmĩrore ũguo.......* (uk 11) | Wangeci : Mbona unaifurahia hiyo hati ya kumiliki ardhi? Kwa nini unaitazamatazama kwa furaha nyingi namna hiyo. (uk 11) |
| Kĩgũũnda :.....*Kwaria nĩ kwendana,……..* (uk 48) | Kĩgũũnda :…..Mazungumzo ni mapenzi,…… (uk 44) |
| Mũtoongoria : *Caitani wa nduma-inĩ Nĩ araangwo!*(uk 16) | Kiongozi : Shetani wa giza Na akanyagwe! (uk 16 ) |
| Wangeci : …*Irũrũ ici kaĩ ciatuĩkire wĩra?* (uk 12) | Wangeci :…Hii pombe imekuwa kama kazi? (uk 12) |
| Mũtoongoria : *Arĩa matarĩ wako kana cieya,* (uk 15) | |
| Njooki: *Naa wewaririe mũno.* (uk 78) | Kiongozi : Wasio na pa kujenga au kikata (uk 15) |
| Gathoni: *Ngaahika Ndeenda.* (uk 24) | |

Kĩgũũnda: …*kũraathimithia ũhiki witũ na*

*Wangeci*. (uk 67)

Gĩcaamba*: Rekeei tũthiĩ,* (uk 78)

Njeethibeeri*: Rekia rũhiũ rũu.*(uk 106)

Wangeci*:Rekeei anjũrage arĩe nyama icio!*

(uk 112)

Kĩgũũnda: *Ti ithaga rĩene,*

*Rĩrĩa rĩerirworĩnogagia ngiingo.*

*Mũndũ ainaga na gatiirũ gaake.* (uk 11)

Kĩgũũnda: *Thĩĩna ndurĩ njaamba na*

*mũũgĩ ndooĩ ũrĩa akeerwo* (uk 13)

Wangeci: *Ningĩ mathanwa me kĩondo kĩmwe*

*matiagaga gũkomorania.* (uk 25)

*Kĩgũũnda: Kaĩ mũrũmĩrwo ndamenyaga*

*igĩthira-ĩ ?*

*Kaĩ ũũĩ kũruta nĩ gũcokia ?* (uk 26)

Gĩcaaamba: *Gũtirĩ wĩĩriraga agĩthiĩ ta*

*agĩcooka*.

*Wĩĩmenyerere ndũkoorwonĩ inya ũteng'ereire*

*inyaanya.*

(uk 67)

Gĩcaamba: *Na ya gwĩĩthuurĩra ndĩrĩ ihĩndĩ.*

(uk 78)

Gĩcaamba: *Ĩrĩ kũhũũma ndĩrĩ mũtĩ ĩtangĩgwaatĩrĩra.*

(uk 107)

Mũrĩĩu: *...Kana watuĩkire wohagwo na mũthuru ?*

Njooki: Na wewe nawe umesema sana. (uk 72)

Gathoni:Nitaolewa nipendapo.

(uk 23)

Kĩgũũnda: …...kuthibitisha ndoa yetu naWangeci. (uk 62)

Gĩcaamba: Hebu tuagane, (uk 72)

Jespheli: Weka kisu chini (uk 98)

Wangeci: Hebu mwacheni aniue ale nyama yangu! (uk 104)

Kĩgũũnda: Hii si nguo ya kuazima, Ambayo haisitiri matako.

Kila ndege huruka kwa ubawa wake.(uk 11)

Kĩgũũnda: Taabu ni laana; Tahadhari kabla ya athari. (uk 13)

Wangeci: Aidha, vyuma vikiwa katika gunia moja havikosi kugongana. (uk 24)

Kĩgũũnda: Kweli mpewa hajui akiba ikimalizika.

Chovya chovya humaliza buyu la asali? (uk 25)

Gĩcaamba: Majuto ni mjukuu. Jihadhari usiponyokwe na nne ukitarajia kupata nane. (uk 62))

Gĩcaamba: Na kipendacho moyo ni dawa. (uk 72)

Gĩcaamba: Mbio za sakafuni huishia ukingoni. (uk 99)

(uk 12)

Gĩcaamba: *Githĩ mũndũ tiwitũ na Ngai?*(uk 42)

Gĩcaamba: *Ngookĩra rĩrĩa Maara aateire nyina.*

(uk 96)

Gĩcaamba: Ĩ *ngaiyĩrwo na marũa.* (uk 48)

Gĩcaamba: *Ĩ ngwaria cia aruti a wĩra.* 49)

Mũkũi: *Coro!* (uk 117 – 118)

*Twathiiaga tũkeneete*

*Tũgacooka tũkeneete*

*Rũgeendo rwitũ rũraarĩ rwega*

*Tũgĩthiĩna tũgĩcooka.* (uk 76)

Gĩcaamba: *Angĩ macookaga kanitha magĩthikwo*

(uk 69)

Kĩgũũnda: *Kwĩĩragwo ũthuri wa gĩtonga*

*ndũnuungaga.*(uk 105)

Gicaamba: *Araabutirwo wĩra na* ............ (uk 42)

Gathoni: *Yĩ-ĩ!*

Gathoni: *Yũũũ!* (uk 23)

Njooki: *Naawe ingĩnyiita Kĩoi ũcio ũraaganwo*

*Na maya manyiitaga tĩĩriaamenya.* (uk 109)

Herina: *Muume mũtondo–inĩ wa meehia.*

(uk 55)

Kĩgũũnda: *O na mĩaka mũgwanja ndĩathirire!*

(uk 32)

Njooki: *Nĩ agaacoka!* (uk 109

Mlevi: …......Au umekuwa mkaa jikoni? (uk 12)

Gĩcaaamba: Si anakaribia kuwa marehemu? (uk 40)

Gĩcaamba: Nitaamka alfajiri na mapema. (uk 88)

Kĩgũũnda: *Toondũ nĩ guoka mbĩa hiũ.* (uk 103)

Kĩgũũnda: Kwa kuwa mambo moto moto yamezuka. (uk 96)

Gĩcaamba: *'taondoka kwa barua.* (uk 44)

Gĩcaamba: *'tasema ya vibarua*. (uk 45)

Kiongozi: Mbiu. (uk 109 – 110)

*Tulikwenda kwa furaha*

*Tukarudi kwa furaha*

*Safari yetu ilikuwa nzuri*

*Kwenda huko na kurudi*. (uk 70)Gĩcaamba: Wengine hurudi kanisani kwa hatima ya mazishi yao. (uk 63)

Kĩgũũnda: Watu husema mashuzi ya tajiri hayachukizi.(uk 98).

Gĩcaamba: Aliachishwa kazi na …................... (uk 40)

Gathoni: Yĩĩ–ĩ! (Japo mtafsiri hakuakifisha ifaavyo)

Gathoni: Yũũũũ– ũ! (uk 22)

Njooki: Nikimshika huyo Kĩoi anayesifiwa

Helina: Mtoke katika bahari ya dhambi.

(uk 52)

Kĩgũũnda: Oh, hata miaka saba haikuwa imepita! (uk 31)

Njooki: Atarudi tu! (uk 101)

Kwa hii mikono yangu ivurugayo udongo

Atakiona kilichomtoa kanga manyoya.

(uk 102)